ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe

15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himidi	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
31.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe

32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
51.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
52.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
53.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
54.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile

55.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

56.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

57.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

58.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

59. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

60.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

62.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

63.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

64.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

66.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

67.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

68.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

69.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

70.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

72.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

75.Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

76.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

78.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Thalathini na Nne – Tarehe 1 Agosti, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani kuhusu hotuba ya makadiro ya mapato na matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Hassan Hamad Omar (Kny:Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi naomba kuwasilisha mezani hotuba ya maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka 2012/2013. Naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 – Wizara ya Kilimo na Maliasili

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama kawaida siku hizi karibu siku zote tunapata wageni na wageni wetu kwa leo ni wageni kutoka Uongozi wa Serikali ya Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*SUZA*) ni wasomi wetu hawa, jumla yao ni 30. Naomba Serikali ya Wanafunzi kutoka *SUZA* wasimame.

Ahsanteni wageni wetu karibuni sana, wasomi wetu wajao na viongozi wa kesho, karibu kuona namna gani chombo chenu hiki kinavyofanya kazi kwa ajili ya wananchi. Ahsanteni sana. Wageni wetu tunakushukuruni.

Waheshimiwa Wajumbe, ninataka nidokeze jambo dogo kabla hatujaanza kuendelea na majadiliano ni kwamba Wizara hii ya Kilimo na Maliasili tutaendelea na mjadala mpaka saa za mchana, na ilikuwa leo kwa kweli tumalize hata kupitisha vifungu vyake. Lakini ni dhahiri kwamba itakuwa hapana muda hata ule wa kujitayarisha kwa ajili ya kutoa majibu muafaka kwa hoja na masuala mbali mbali ambayo Waheshimiwa Wajumbe mumemuhitaji Mhe. Waziri afafanue. Kwa hivyo ili Mhe. Waziri aweze kujibu hoja hizo vizuri, tutakwenda mpaka saa za mchana, ninategemea kwa Wajumbe ambao 11 waliopo mbele yetu watakuwa wanatosha kusaidia michango kwa ajili ya wizara hii.

Tukimaliza hao basi tunaakhirisha hoja hiyo mpaka kesho Mwenyezi Mungu akipenda asubuhi Mhe. Waziri aje afanye majumuisho. Lakini wakati huo huo tumuombe Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano ameniarifu mapema kwamba yupo tayari ili awasilishe hoja yake ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na pengine mwenyekiti atawahi itategemea na muda utakavyokuwa ili kesho mara tu baada ya kwisha kupitisha vifungu basi tuendelee na majadiliano ya wizara hii.

Hii tumeifanya kwa kumpa nafasi Mhe. Waziri apate kwenda kujitayarisha ili aje atoe majibu muafaka kwa hoja na masuala mbali mbali ambayo yatatolewa na Waheshimiwa Wajumbe katika michango yao.

Hii ilitusaidia sana wakati wa Waziri Mhe. Mohamed Aboud alipokuwa anatoa ile Kauli ya Serikali juu ya ajali ya meli. Maswali yalikuwa mengi tukaona tumpe muda aje ayajibu siku ya pili yake na ninafikiri ilisaidia sana kutoa majibu yaliyo muafaka na tukaendelea na hoja nyengine.

Kwa hivyo mutaona kama imepandanapanda kidogo lakini kwa madhumuni ya kumpa Mhe. Waziri nafasi ya kuja kujibu hoja vizuri. Baada ya hapo majadiliano yanaendelea.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninashukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii leo nikawa mchangiaji wa mwanzo hapa.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wa wizara hii kwa kutuletea hotuba hii mwanana kabisa yenye mwelekeo wa mapinduzi ya kilimo. Mhe. Spika, mimi nikianza mchango wangu katika wizara hii nianzie kwenye ukurasa wa 43, kwenye changamoto za wizara.

Kwa kweli Mhe. Spika, nilikuwa niwe na mengi sana leo katika wizara hii lakini Mhe. Waziri amenipunguza kasi kidogo kutokana na kuwa muungwana wa kuainisha zile changamoto zile zinazokabili wizara hii, kwa hivyo na mimi nimekuwa nimepunguzwa na kasi ya kuja kusema mengi. Maana Waswahili wanasema, “Muungwana akidondokwa na shuka huchutama hainami”. Sasa Mhe. Waziri hapa kachutuma kwa hivyo lazima nimpongeze kwa uungwana wake kuonesha zile kasoro ambazo yeye ameshaziona tayari. Kwa hivyo hii imenifanya hata ile michango yangu isiwe mikali sana au isiwe mikubwa sana, maana yake amekwishaieleza kwamba yeye ameshayaona haya matatizo.

Sasa kwa sababu amekiri hivyo na ameyaona, mimi nilikuwa namuomba tu Mhe. Waziri basi atakapokuja hapa atusaidie changamoto hizi alizoziona namna ataweza kuzikabili ili ziweze kuondoka changamoto hizi.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele changamoto ambazo alizozionesha Mhe. Waziri humu ni nyingi tu lakini mimi muhimu hizi ambazo niliziona na kutaka kuzichangia sana ni kukosa zile huduma za pembejeo, huduma za matrekta, kutofanyika kama ilivyokusudiwa na mambo kama hayo. Kwa kweli hivi vitu vilikuwa vipo ni vingi lakini ndio pale niliposema Mhe. Spika, inabidi Mhe. Waziri kama kanifunga kidogo.

Sasa nitarudi huku nyuma kidogo nije kwenye wizara yenyewe. Mhe. Spika, wizara hii ni moja kati ya wizara zenye wasomo wengi sana. Ukiangalia takwimu hapa zinaonesha Mhe. Waziri ana wasomo wengi sana lakini katika kuangalia kwenye ukurasa wa 18 wa kitabu cha hotuba kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi, niende kwenye utekelezaji wa malengo yenye nukta nne tatu, juu ya wafanyakazi hawa.

Mhe. Waziri ametoa maelezo hapa wafanyakazi waliofariki, walioajiriwa na nini, lakini nimeona kuna wafanyakazi wamekwenda likizo bila ya malipo, karibu wafanyakazi 34. Mimi kidogo nimeshtuka Mhe. Spika. Wafanyakazi 34 wanakwenda likizo bila ya malipo wanakataa mshahara. Sasa wasi wasi wangu bila shaka wamepata mshahara mkubwa zaidi ndio maana yake waende likizo bila ya malipo.

Sasa hii inanishtua kabisa kwa sababu wizara hii inafanana na Wizara ya Afya kwa kuwa na wafanyakazi wasomi wengi. Lakini tuligundua katika Wizara ya Afya tulikuta sisi wafanyakazi wanaoondoka au madaktari wetu wale huondoka wakenda nje ya nchi kwa kutafuta maslahi zaidi. Kule wao wanaondoka kabisa pengine hata hawaji na vitu kama hivyo lakini wameomba likizo bila ya malipo na wamepewa.

Mimi ninahakika katika wafanyakazi hawa 34 waliomba likizo bila ya malipo huwezi kukuta akina Mtando, huwakuti humu, wale wadogo wadogo ninajua wengi wao watakuwa ni wasomi. Kwa kweli wizara hii tunawahitaji katika sekta ya kilimo kwenye mambo ya utafiti huko, mambo ya kilimo na mambo kama hayo.

Sasa ninapata shaka Mhe. Spika, kwamba serikali itakuwa inasomesha sana kwa kutumia gharama kubwa, lakini wasomi wetu hawa wanaonekana wanatukimbia katika njia tofauti tofauti. Hapa inaonekana wametukimbia kwa njia ya kuchukua likizo bila ya malipo, kwamba watakwenda baadae anaweza akarudi, akaja akaongeza tena likizo kama hukumpa maana yake ndio hairudi imetoka hiyo.

Sasa mimi wasi wasi wangu sana ninafikiria upo kwenye maslahi ya watumishi hawa. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa hebu atusaidie kiini cha wafanyakazi hawa kuchukua likizo bila ya malipo wengi kiasi hiki ni nini, aje atusaidie ili tuweze kujua tatizo hasa ni nini. Isijekuwa ndio kama yale tunayokumbana nayo kwenye taasisi nyengine. Serikali inasomesha, ikishakusomesha watu wamekaa kule wanasubiri, wanasubiri vielee tu wao wachukue, lakini watu wanasema ukiona kinaelea kimeundwa.

Sasa serikali imekuwa inaunda lakini watu wanavidowea huko wavichukue. Mimi ninafikiria Mhe. Spika, Waziri wa Utumishi yupo hapa mwenyewe aangalie zaidi maslahi ya wasomo wetu hawa. Bila shaka kuna sababu zinazowafanya wakafanya haya.

Mhe. Spika, lakini si wasomi tu peke yake katika wizara hii. Wizara hii Mwenyezi Mungu kaijaalia kuwa na wataalamu wale wa uzoefu, mimi huwaita wenye *PhD* viza. Maana yake yapo mayai yaliyokuwa sawa na kuna mayai viza lakini yote yanatumika. Mayai ya kawaida unatumia katika siku za kawaida lakini kuna siku unakwenda mahala unaambiwa linatakiwa yai viza. Kwa hivyo ujue nalo hilo linatumika. Sasa wataalamu wale ni wazoefu sio wasomi kama hawa

wengine. Tena uzoefu wao unaweza ukakuta wakati mwengine hata huyo mtaalamu anakwama kwa mtu mzoefu.

Mhe. Spika, mimi nimetembea tembea kwenye wizara hii kidogo, ukenda mabondeni kule unawakuta wazee hawa, unamkuta mtu pale ana uzoefu akikwambia bwana mpunga huu mara huu hii hautoi kitu, hautoi kweli utafikiri ni mganga wa kienyeji labda anaagulia. Lakini ni uzoefu ndio uliomfanya vile, ana miaka 35 pale mabondeni, yupo pale. Kwa hivyo anakuwa mzoefu kuliko mwenye *PhD* ya kawaida, hii *PhD* yake viza inakuwa bora kuliko huyu wa huku. Lakini si mabondeni tu, hata kule msitu wa Jozani nimewahi kufika Mhe. Spika, nimetembelea nikakutana na mzee mmoja pala anakusomesha habari ya msitu ule wewe mwenyewe utashangaa na hana *PhD* yule. Sijui hata wewe Mhe. Spika, umewahi kuingia pale, maana ndio unakatiza kwendea Kae, sasa sijui kama uliwahi kuingia pale kwenda kupata utaalamu pale.

Ningekuomba kama hujawahi kufika pale Mhe. Spika, iingia siku moja ukapate maelezo ya msitu ule, kuna mambo mengi sana pale. Watu wanayajua ghibu, si kwa kutizama kwenye kompyuta wala vipi. Sasa wale ni watu muhimu sana. Sasa sijui Mhe. Waziri anatwambia nini juu ya watu hawa hasa kwenye maslahi yao, maana hawa ukiwatizama hawana tofauti na hawa wasomi. Wasomi kweli wana *PhD*, Masters, na digrii zao na mambo kama hayo lakini hao wenzangu mimi hawa, darasa la saba pengine wengine la nne kabisa lakini ule uzoefu wao uliokuwepo pale unamshinda yule mwenye *PhD*. Sasa hawa maslahi yao yakoje katika uzoefu wao huu.

Mhe. Spika, nilikuwa nigusie hapo kidogo kumuonesha Mhe. Waziri umuhimu wa wataalamu wetu bubu hawa namna wanavyofanya kazi. Hawa ni watu muhimu kwetu hasa ukizingatia kilimo chetu kinategemea wataalamu, lakini hawa kwetu sisi kule kwa wakulima wetu huwa ndio bora zaidi.

Maana hawa ndio huwa tunaogoleana zaidi kwenye mabonde au katika sehemu zile kuliko hawa wataalamu wa kutumia kompyuta. Kwa hivyo nilikuwa ninataka nimuoneshe Mhe. Waziri umuhimu wa watu hawa na namna gani atakuwa anawaenzi watu hawa.

Mhe. Spika, mimi nikiendelea mbele kweneye kitabu chake Mhe. Waziri hapa amezungumzia upimaji wa mashamba katika maeneo tofauti. Kwa kweli hili Mhe. Spika, limekuwa ni tatizo. Tumewahi kufanya ziara kule na tukakuta kwamba mashamba yetu mengi yanavamiwa ya Wizara hii na watu kwa kutokuwa na hatimiliki kwenye mashamba yale.

Maana watu siku hizi watu wajanja, mtu anajenga nyumba yake anamaliza anakwenda kuchukua hati. Wewe unakuja kumwambia mahali hapa ni shamba la kilimo, yeye ana hati na wewe kilimo huna hati, ni tatizo. Sasa kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri hapa kama ni sahihi kama haya maelezo yake, basi mimi nimpe hongera kwa kuweza kuandaa au kutayarisha hatimiliki za mashamba haya. Kwa sababu hili limekuwa ni tatizo kubwa na sisi tulikwenda kamati yetu tumeligundua hili na tuliwaagiza kwamba wafanye hivi. Tunashukuru kwamba hivi wamefanya.

Lakini katika hili suala la mashamba Mhe. Spika, mimi nilitaka niulize kidogo kulikuwa kuna shamba kule Pemba la mziwanda maeneo ya Micheweni kule. Tulikwenda na kamati ya *PAC* tukakuta kuna tatizo pale shamba la kilimo lile kapewa tu mtu binafsi bila ya kufuata utaratibu

wowote ule. Sasa kulikuwa kuna agizo la kamati ya *PAC* pale kwamba shamba lile lirejeshwe kwenye mikono ya Wizara ya Kilimo. Kwa hivyo nilikuwa ninataka kujua tu Mhe. Waziri sijui shamba lile limerejeshwa tayari au laa.

Lakini niendelee mbele hapo hapo Mhe. Spika, amezungumzia Mhe. Waziri hapa juu ya nyumba za wizara hizi zilizokuwepo katika maeneo tofauti tofauti. Lakini mimi nilikuwa ninataka kujua zaidi kwenye nyumba hizi za Mbweni, Mazizini ni nani wanaoishi katika nyumba hizi. Ni wafanyakazi wa Wizara ya Kilimo au wizara hii imezikodisha au vipi, nilikuwa nipate maelezo kidogo juu ya maeneo hayo.

Nikitoka hapo Mhe. Spika, nisogee mbele kidogo kwenye Karakana ya Matrekta Mbweni. Mhe. Spika, karakana hii ni muhimu sana kabisa katika dhana nzima ya mapinduzi ya kilimo. Kwa kweli Mhe. Spika, bila ya kuwe na karakana ile basi hii dhana nzima ya mapinduzi ya kilimo inawezekana ikawa kama ni ndoto.

Kwa sababu kama unavyojua tumehama kwenye kile kilimo cha kijembe kongoroka, tumeingia kwenye zana za kisasa. Kuna matrekta, majembe hayo ya kulimia lakini utakuta Mhe. Spika, kuna tatizo pale kidogo. Wafanyakazi maslahi yao yapo madogo sana wa sekta ile ya karakana yapo duni sana.

Ndio pale niliposema wizara hii Mwenyezi Mungu ameijaalia ina wasomi wengi lakini ina watu wa *PhD* viza wengi tena wazuri. Lakini hilo Mhe. Spika, na pale lipo. Kuna watu pale hawana hizo master digrii wala *PhD* lakini wana uzoefu wa kufanya kazi katika karakana ile. Mimi nina hakika Waziri mwenyewe ninafikiria ni shahidi kwamba kinachokwama katika karakana ile, wanachapa kazi, wazee wangu pale kuliko mchezo.

Mimi nimekwenda katika karakana na nimetembelea nimeona, nimejaribu kuwauliza uliza pale, nilikuta matrekta mengi yamepangwa pale nikafikiria yote ni mabovu. Nikasema haya hata mukiyamaliza lini, wakasema hapana, haya sio mabovu bwana, haya yamekaa yanasubiri muda wa kuingia mashambani tu, hapa yapo mazima yameletwa tushayafanyia service, yamekaa hapo yanasubiri tu. Wakanionesha namna gani wanavyofanya zile kazi. Kwa kweli Mhe. Spika, wanafanya kazi moja kubwa sana katika kusaidia sekta hii ya kilimo.

Lakini maslahi yao bado hayajaangaliwa vizuri. Kwa hivyo nilikuwa ninamuomba sana Mhe. Waziri ayaangalie maslahi ya wafanyakazi wale, kwa sababu wao wanafanya kazi pale mpaka usiku wakati mwengine, kwa sababu trekta limeletwa mchana lakini wanahitaji kesho lirudi tena shambani. Kwa hivyo wao wanajipinda wanafanya kazi kwa bidii kabisa, kuhakikisha kuwa linatoka katika siku ile.

Jana tu nimekwenda pale mimi, nimekwenda kukuta trekta zilizoletwa juzi, zimekwenda kwenye majaribio mashambani zimepata matatizo kidogo, unajua mashamba yetu hapa. Nikauliza vipi, wakasema haya yameletwa juzi lakini yamepata matatizo sehemu ya kuvunia ile. Wazee wanapangapanga wameshachonga vipuri na kila kitu, wanasema hivi sasa tunalifunga hili linarudi zake shambani. Kwa kweli wanastahili pongezi Mhe. Spika, kuwa na watu jasiri kiasi kile. Kifaa kimeletwa juzi hata mwezi haijafika tayari wameshakuwa na utaalamu nazo,

hawajapelekwa mwahala kwenda kusoma hawa, ni uzoefu tu. Uzoefu ndio unaowafanya kutengeneza kile kifaa ambacho Mchina mwenyewe yupo anatizama macho tu pale.

Mhe. Spika: Muda wako unayoyoma.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakubali muda unamalizika Mhe. Spika, lakini nilikuwa nitoe maelezo zaidi kidogo kwenye hili. Maana yake kuonesha uhodari wa watu wale na namna ambavyo tumewaacha hatuwatizami vizuri. Kwa hivyo mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri tukawatizama kwa jicho la huruma wafanyakazi wale ili waendelee kuwajibika vizuri zaidi.

Kwa sababu wenzetu huku kwenye sekta ya fedha wanapatiwa posho maalum zile. Wakikusanya wanaambiwa one percent ya kwenu, kwa hivyo wanakusanya zaidi. Sasa na hawa ambao wanaumiza akili zao katika kutengeneza haya, tuwawatizame na wao tuwape motisha, tuwatafutie chochote hawa Mhe. Spika, tuwape hawa.

Kwa hivyo ninamuomba sana Mhe. Waziri aangalie maslahi ya watu hawa. Lakini vile vile mashine zilizokuwepo pale zimeshakuwa ni za muda mrefu sana. Kwa hivyo wamekuwa wanabangaizabangaiza, zana zilizokuwepo pale ni duni. Ninamuomba sana Mhe. Waziri sasa hivi watu wameingia kwenye zana za kisasa, kwa hivyo tuwabadilishe. Tubadilishe zile zana ili na wenzetu hawa waweze kwenda na zile sana.

Lakini nimalizie kwamba ameonesha hapa Mhe. Waziri namna ya wafanyakazi wake wanavyokwenda kuwasomesha. Ningemuomba na kitengo kile cha matrekta awakumbuke wafanyakazi wale kupewa elimu zaidi ili waweze kufanya kazi zao vizuri zaidi.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi niunge mkono hoja. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, kwanza nishukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

La kwanza kabla ya kuchangia nitoe pongezi kwa Mhe. Waziri wa wizara hii kwa namna alivyowasilisha hotuba yake kwa ufasaha na kufahamika kabisa. Mhe. Spika, wizara hii ni wizara inategemewa sana na ndio pekee kwa maisha ya binadamu. Binadamu anahitaji kula na inategemea ni namna gani wizara hii inawajika katika kutekeleza shughuli zake ili wananchi wa nchi hii waweze kupata chakula bora na pia ni wizara inayotegemewa kwa kuweza kuzalisha mali za kutosha juu ya chakula na mengine kwa biashara na nchi za nje.

Mhe. Spika, sote tunajua kuwa Mwenyezi Mungu katujaalia neema kubwa katika nchi hii. Ni nchi yenye rutba sana kweli kweli, takriban kila sehemu yake mazao yanaota. Ni nchi iliopo katika ukanda wa joto, mabadiliko mazuri ya hali ya hewa yaliopo na ni nchi yenye ardhi yake yenye mbolea nzuri sana. Ni kwa sababu hiyo ukiangalia katika nchi hii ya Zanzibar mimea yote inaota na inastawi vizuri sana. Mtu akiingia pahala ambapo hapakulimwa lakini atakutia kila aina miti ipo pale. Mifenesi ipo pale, mipapai, miembe na kadhalika. Hii ni kuonesha kuwa ni nchi yetu ni nchi yenye rutba kubwa.

Mhe. Spika, jengine wizara hii ni moja kati ya wizara ambayo yenye wataalamu wengi na wa kila fani. Kwa maana hiyo Mhe. Spika, kama kungekuwa kuna umakini kabisa kwa wizara hii kutekeleza majukumu yake vilivyo na kuwa na uwezo wa kufanya hivyo, basi ilikuwa hakuna sababu ya kuagizia mchele mwingi kutoka nje wakati mpunga mwingi unaota hapa. Pia ilikuwa hakuna sababu ya kuagizishia nazi kutoka Bara, wakati minazi inaota vizuri sana hapa, na mpaka mingine tunaikata na kuifanya mbao. Vile vile ilikuwa hakuna sababu mahindi ya kuchoma kuagiziwa kutoka Bara wakati hapa yanaota vilivyo, wachilia mbali miti yenye matunda mazuri kama miembe, mifenesi na kadhalika.

Mhe. Spika, si hivyo tu, kwa sababu ya rutuba ya nchi hii Mwenyezi Mungu katujaalia kuwa na miti ya asili ambayo inafanya misitu, ambayo inaota yenyewe. Kwa mfano Jozani, Ngezi na kadhalika. Lakini sasa Mhe. Spika, kwa sababu ya kutokuwa makini katika kuwatumikia wananchi kupata lile wanalohitaji, basi wananchi wanaitumia ardhi hii vyenginevyo.

Kwa mfano, Mhe. Spika, kuna watu wengi tu wanaendesha maisha yao kwa kukata miti ovyo, miti ya misituni ambayo ni miti tunayoihitaji kwa mambo kadhaa. Tunajua miti inasaidia kuondoa gesi mkaa. Tulipokwenda kwenye Mkungumi tuliona. Miti inasaidia kuleta rutuba katika ardhi, miti inasaidia kupunguza joto kubwa sana, miti inasafisha hewa na palipo na misitu hapakosi mvua siku zote. Lakini tunapoingia misituni tukaikata ovyo kwa sababu ya umaskini wetu pamoja na kutumia misumeno ya moto, hii ni hatari tunaifanya na kwa kiasi fulani nchi hii tumeipeleka pabaya. Badala ya kutumia vizuri hii neema Mwenyezi Mungu aliyotupa katika nchi hii ya miti kuota ovyo, sasa tunaikata na kuitia katika jangwa.

Mhe. Spika, sababu ya sisi kushindwa kutekeleza wajibu wetu ipasavyo, na kwa sababu wananchi wetu wanahitaji kula, wanahitaji kuvaa na kadhalika, basi tunakuwa na ukulima wa kale ambao ni wenye kuharibu ardhi. Kwa mfano, kuna wakulima wanalima kwa njia ya urahisi kwa kutia moto kwenye mashamba, hii inasababisha kuondoa rutuba katika ardhi.

Mhe. Spika, kuna wakulima wengine, naona ndio wengi, juu ya uwezo mdogo pengine wa serikali au mipango ambayo haikukamilika vilivyo, basi mpaka leo wanatumia kijembe kongoroka. Hii inasababisha kufanya kazi kubwa sana na kusababisha uvunaji wa mazao kidogo, na hatimaye serikali kulazimika kuagiza chakula kutoka nje, wakati uwezo wa kukizalisha katika nchi hii upo.

Sasa basi Mhe. Spika, mimi ninavyoomba ni kuwa kwa maslahi ya nchi hii na lengo kufikiwa la kuwawezesha wananchi kupata chakula cha kutosha na chakula bora, kuiwezesha nchi hii kuweza kusafirisha chakula nje na kuiwezesha nchi hii kupunguza uagizishaji wa chakula, basi ni lazima tubadilike katika kupanga mipango ambayo haitekelezeki, vyenginevyo Mhe. Spika, itakuwa siku zote tunadidimia katika shimo la umaskini.

Mhe. Spika, tukiangalia mwaka jana au kipindi kilichopita palikuwa na hali na dhamira nzuri tu ya wizara hapa, kuwapatia wananchi mbolea ya kutosha tena ya bei rahisi, kuwapatia wananchi mbegu kwa bei rahisi, na pia kuwalimia kwa bei rahisi. Lakini baada ya wananchi kuitikia wito ule kwa tamaa kubwa sana, lakini kwa bahati mbaya Idara ya Kilimo ilishindwa kufanyakazi zake ipasavyo, na matokeo yake na kwa vile waliona kuwa hawakufanikiwa ipasavyo, basi wakaingiza katika kitabu hiki kwenye ukurasa wa 43 kama ndio changamoto ya wizara.

Mhe. Spika, naomba kwa ruhusa yako kusoma ili iweze kueleweka zaidi. Katika ukurasa huu unaeleza kama ifuatavyo; ‘‘kutokana na kiwango cha ruzuku kilichowekwa, pamoja na uhamasishaji juu ya matumizi ya pembejeo na faida zake, kumekuwa na mahitaji makubwa kuliko ilivyotarajiwa katika makisio. Hali hii imesababisha baadhi ya wakulima kukosa huduma ya pembejeo hizo kwa wakati’’.

Sasa Mhe. Spika, haya mambo tulieleza sisi tukawaweka watu wasubiri kwa hamu kubwa matrekta na kadhalika. Wakati ukapita na mpunga ni moja kati ya kilimo kinachokwenda kwa wakati, ikifika wakati wake wa kupumua kinapumua japokuwa hakikupata kitu kutokana na kuchelewa. Kwa hivyo, matokeo yake wananchi badala ya kuwa na tamaa ya mafanikio, basi wamebakia katika umaskini mkubwa sana kwa kuharibikiwa na vipando vyao, kwa sababu tu ya kutokufanyiwa shughuli za ukulima kwa wakati.

Pia katika changamoto wameeleza kuwa kulikuwa na baadhi ya matrekta ambayo yaliharibika na hayakutengenezwa, na haya yalichangia kukosekana upatikanaji wa ukulima kwa kiwango kilichotarajiwa.

Mhe. Spika, wakati tumewaahidi watu kuwa tutawalimia kwa kutumia matrekta na matrekta tunajua kuwa hivi ni vifaa lazima vinahitaji matengenezo. Kwa hivyo, unapoamua kufanya kitu ni lazima ujiweke katika hali ambayo popote pakitokea mabadiliko uweze kupambana nayo. Kwa hivyo, ilikuwa wizara ijue kuwa kwa sababu imeshaahidi watu kutumia matrekta, basi wajue kuwa matrekta yanaweza yakaharibika na ilikuwa kutengwe fedha za kutosha ili kuhakikisha kuwa matrekta hayo yametengenezwa kwa maslahi ya wananchi.

Kwa hivyo, natoa wito kwa sababu wananchi wameharibikiwa na kipando chao, na baadhi ya sababu ikiwa ni wizara yenyewe. Kwa hivyo, hakuna budi kuwasaidia wananchi hawa kwa kupata fidia kutokana na mazao yao yaliyoharibika, na ninasikitika hata hao waliotumia hii mbegu ya *nerika* iliyosifiwa basi haikuja vizuri kwa sababu ya kutofanyiwa shughuli zao kwa wakati muafaka.

Jambo jengine Mhe. Spika, ni kuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili ina wataalamu wanaofanya utafiti sana tu katika kuzalisha mbegu mpya. Kwanza naunga mkono kuwa uko mpango wa kudumisha hii miti ya asili, lakini kuna mpango mwengine wa kujaribu kuzalisha hii mbegu mpya.

Mhe. Spika, mimi naomba hili nizungumze hivi. Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu alipotuumba sisi pamoja na viumbe vyengine vyote tunaona tu tuko tunaishi, wale wanaondoka na wale wanakuja na kadhalika, lakini kuna kitu kinaitwa *balance of nature*. Mhe. Spika, kama ingekuwa kila kinachozaliwa kinakua na kuzaa, basi dunia hii isingekalika, kwa sababu kungekuwa na umati wa wadudu wengi tu, watu wangekuwa wengi tu, samaki wangekuwa wengi huko na kadhalika. Lakini Mwenyezi Mungu kajaalia vile viumbe vinapozaliwa pamoja na kuwa vinazaliwa na baba mmoja na mama mmoja, vinakua na mabadiliko yanayoitwa *variation*. Wengine wanakuwa na sifa ambazo zinawawezesha katika mazingira yale kuweza kuishi na kuendelea kuishi na kuzaa na kuzaana, na vyengine vinapoteza maisha njiani kutokana na kukosa baadhi ya sifa. Kwa

maana hiyo, siku zote ndio utaona kuwa kuna mambo ya asili yanabakia milele na milele, kwa sababu imeshapita mitihani hiyo ya maumbile.

Kwa hivyo, ushauri wangu kwa wizara, kwa vile nchi hii inaota kila aina ya mimea. Kwa mfano ukienda Ndijani kuna michungwa mingi sana tu, Makaani tunajua huko tena, Vitongoji tungule zinatafutiwa soko hivi sasa na mazao mengineyo. Mule mwahala mwenye vipando vya asili vilivyoota iwe ni miti au mimea, wajibu wa wizara ni kuchagua mbegu bora na kuiendeleza kuliko kubadilisha kila mara, kutafuta mbegu mpya ambayo kwa utaalamu wetu, kwa sababu mbegu zote zinazotafutwa hapa isipokuwa *nerika*, sijaona hata mbegu moja iliyokuwa na jina jengine, tunaambiwa tu aina 15 za mpunga na nyenginezo. Wakati chochote kinachovumbuliwa ikiwa ni kipya huwa kinapewa jina, halafu wataalamu kama Sheikh Saleh hapa huangalia kwa jina hili ni sifa zipi ziliopo.

Mhe. Spika, natoa mfano. Kuna wenzetu waliishughulikia hii tangawizi, lakini kwa sababu inatumika Zanzibar kwa wingi basi ikaitwa *Zanzibari officially* yaani *special* kwa Zanzibar. Kwa hivyo, ukisema hivyo ulimwengu mzima wanajua hii ni tangawizi. Duniani kulikuwa hakuna madini yanayoitwa Tanzanite, ilivumbuliwa ilikuwa haijulikani, ikaangaliwa ikaitwa Tanzanite hakuna jengine.

Leo ukisema *homosapiens* kila mtu atajua kwa kusikia binadamu ana sifa zake. Mfano ukisema *calamastungan*, basi mtu atajua mti huu sifa zake ni zipi una *q-classification*. Kwa hivyo, nawaomba wataalamu wetu wanapovumbua jambo walipe na jina ili ijulikane kuwa Mzanzibari kavumbua hiki. Lakini mambo ya kuchanganyisha tu na kubuni kuwa tumepata mbegu bora, inaweza ikawa haina *adept features* tukaja tukaondoa mbegu ya asili na matokeo yake tukaja tukafilisika. Tuache mtindo huu ambao hauelekei mtaletewa mbegu halafu mtaambiwa inaitwa sepideh, wakati Sepideh imekuja juzi, kwa sababu haina jina, siku mbili tatu inapotea watu wanahangaika.

Jengine Mhe. Spika, ninaloomba na hili naomba sana na tulipe mkazo wa hali ya juu, ni lazima Mhe. Spika, tuwe na mipango ambayo tunajua serikali hii kwa vyovyote kama tukilima na halafu tukavuna, tukapata chakula cha kutosha hapa, basi itakuwa serikali tunaiondolea mzigo mkubwa sana wa kuagiza chakula kutoka nje.

Sasa twende kwenye *soil analysis*, tukaangalie hali ya udongo wetu ulivyo, tukaangalie mbolea, sio sawa kuwa kila mahala tutumie *urea*, kuna ardhi nyengine inahitaji mbolea ya aina nyengine. Tukifanya hivi tutaweza kutoa mazao tofauti katika sehemu tofauti na *Inshaallah* tutafaidika na tutaisaidia serikali sana kubeba mzigo wa kuagizishia chakula kutoka nje, ambapo hii inatutia hasara kubwa sana.

Mhe. Spika, jambo jengine

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiwa na dakika tano tu.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Jambo jengine ninalotaka kuzungumza ni ufuatiliaji na tathmini. Mhe. Spika, wakulima wetu wanalima tu na tuna mabwana shamba hawa ambao wanapata mafunzo ya muda mfupi, lakini hakuna ufuatiliaji. Matokeo yake tunaona kuwa kazi kubwa

wanafanya na hasa kwa kujitegemea, mwisho wake tunaona wanavuna kidogo. Hii ni hasara kubwa sana ni lazima Mhe. Spika, tubadilike.

La mwisho Mhe. Spika, kwa sababu ya wakati hapana budi ni lazima tuwe tunavilinda na kuvienzi tulivyonavyo, tupambane na wale wote wanaouza misitu yetu kwa sababu ya kutafuta chakula na kadhalika. Serikali iendelee na uzalishaji wa mbegu ya misitu ili kurudisha ule msitu uliokuwa umeondoka.

Vile vile Mhe. Spika, ninaomba kwamba tuwe karibu sana na wakulima wetu, tusiwaachie kutumia ule ukulima wa zamani wa kutia moto mashamba, badala yake twende na utaratibu unaohitajika.

Mwisho kabisa Mhe. Spika, ninaomba kusema kwamba safari hii tuhakikishe kuwa ile ahadi tunayoiweka inatekelezeka, ili isitokezee kama mwaka jana watu kupata hasara kubwa sana. Mhe. Spika, nakushukuru sana, ahsante.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, na mimi nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka huu 2012/2013 kwa Wizara hii ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, kwanza nataka nimpongeze Waziri kwa kukitambua kituo changu cha *Matangatuani Agriculture Station* kuwa ni kituo cha utafiti rasmi kabisa cha kilimo. Kwa hivyo, nampa pongezi hizo.

Jambo la pili Mhe. Spika, ninalotaka kulizungumza ni kwamba hii Wizara ya Kilimo na Maliasili, inahitaji kubadilisha sera zake kwa sababu inaonesha kwamba sera zake katika kilimo ni zile zile za zamani, kwa hivyo inahitaji kubadilisha sera zake, kwa sababu sera ndio zinazotoa muelekeo wa jambo lolote. Kwa hivyo, wizara inahitaji kupitia sera zake.

Jambo la tatu, Mhe. Spika, tuelewe kwamba serikali binafsi inafahamu kwamba katika visiwa vyetu viwili hivi watu wengi wanajishirikisha katika masuala ya kilimo, ambayo tunaweza kusema asilimia kubwa ya watu wetu wanashiriki katika kilimo. Kwa hivyo, sekta hii ya kilimo inajumuisha kazi mbali mbali, na katika kujumuisha kazi hizo, tunafahamu kwamba watu wanategemea kupata maendeleo ya kilimo cha mazao ya chakula na maliasili ya misitu. Vile vile sekta hii ina mchango mkubwa sana katika ukuaji wa chumi wa Zanzibar. Katika sehemu ambayo serikali inategemea kukuza uchumi wake ni katika kilimo. Kwa hivyo, hii ni wizara mama, ni wizara kubwa, ina kazi kubwa na inategemewa kwamba ni wizara ambayo itakuwa na mwelekeo mzuri katika shughuli zake za kuinua uchumi wa nchi na mapato ya wananchi vile vile.

Kwa hivyo, wizara inajitayarisha katika suala hili kuweza kuwaimarisha wananchi walio wengi kwa kuwapatia ajira, kwa sababu tunategemea kwamba suala la kilimo ajira inapatikana. Lakini kwa hali ambayo niliyoizungumza mwanzo kama ni suala la kilimo na sera zake zibadilike, ni kwamba tukibadilisha sera na tuwe na mageuzi ya kilimo, bila ya kuwa na mageuzi ya kilimo sio rahisi kuwa na kilimo ambacho kitaweza kutufaa kwa wakati tulionao. Kwa hivyo, kama tunataka kuondoka katika kilimo cha asili, kwa sababu asilimia kubwa ya watu wetu bado

wanaendelea na kilimo cha asili, kwa kutumia nyenzo zile za kale. Kama tunataka tuondoke katika kilimo kile cha zamani cha asili, basi hatuna budi kufanya mageuzi ya kilimo cha wakulima wote wadogo wadogo na wakulima wakubwa, kwa mazao ya chakula na ya biashara, ambapo mazao haya ya chakula na ya biashara ndio yanayolimwa hapa nchini.

Kwa hivyo, wizara ina kazi kubwa sana katika kufanya mageuzi haya, mageuzi ambayo yatakuwa na uhakika, mageuzi ambayo yatakayokuwa na nyenzo za kutosha. Tukizungumza nyenzo tunazungumza nyenzo zote ambazo zinahitajika katika kilimo pamoja na vifaa mbali mbali, pamoja na kuwa na wataalamu, kwa sababu hawa watu wetu tunaamini kwamba wengi wao ambao elimu yao sio kubwa sana ya kuweza kuendeleza kilimo.

Mhe. Spika, kama tunataka kufanya mageuzi ya nchi hii ya kilimo, hatuna budi kuangalia wananchi wetu kwa wakulima wote wadogo wadogo na wakulima wakubwa katika suala zima la chakula na suala zima la mazao ya biashara. Kwa hivyo, wizara ina kazi kubwa sana ya kuhakikisha kwamba katika mageuzi haya, basi tunafanikiwa katika nyenzo zote pamoja na wataalamu, ambapo wataalamu ni suala muhimu sana katika kuwaongoza wakulima wetu.

Suala jengine Mhe. Spika, ni suala la ukaguzi wa mazao. Tunajua kwamba mazao ni lazima yakaguliwe. Mimi nataka niulize hapa katika ukaguzi huu wa mazao, ni hatua gani mpaka sasa hivi ambayo inachukuliwa katika kuyakagua mazao yetu haya, kwa sababu tunaona matunda yanaingia na vyakula chungu nzima vinaingia, hivyo hatujui katika suala la ukaguzi wa mazao haya, je suala hili bado linaendelea au limekatishwa njiani.

Mhe. Spika, suala jengine ni suala la kwamba sisi wakulima wa Zanzibar tunategemea zaidi ukulima wetu katika masuala ya mvua, na kama tunavyoelewa kwamba katika visiwa vyetu baadhi ya wakati tunapata upungufu mkubwa sana wa mvua, na tunategemea kilimo cha kumwagilia maji. Je, hatuoni kama sasa hivi kilimo hiki cha kutegemea mvua ni kilimo ambacho kama tunasema tuzalishe kwa wingi, tufanye kila kitu kwa wingi hatuoni kwamba kutegemea mvua hili suala ni gumu sana. Je, wizara itakuwa na mpango gani wa kuhakikisha kuona hali halisi kwamba kutokana na *hali ya hewa ukaa* ambayo ilitokezea kwa wingi sana katika nchi hii, joto limekuwa jingi, miti inakatwa na maeneo mengi sana yako wazi. Hapa tuulizane kwa hii mali asili je, ni taratibu gani ambazo mpaka sasa hivi zinachukuliwa ili kuhakikisha tunapunguza hewa ukaa kwa kupanda miti mingi kila eneo, sekta binafsi pamoja na serikali yenyewe kutilia mkazo, suala hili liko vipi mpaka sasa hivi.

Mhe. Spika, ili tuepukane na kilimo ambacho watu wengi, mimi naweza nikasema kwa upande wa jimbo langu na maeneo mengi ya Pemba yamekosa chakula kwa kipindi hiki, kutokana na hali ya ukosefu wa mvua. Mtu hawezi kunidanganya kwa Pemba upande wa Kaskazini akaniambia kuwa watu wamefanikiwa katika kilimo, sio kweli hata kidogo, hawakufanikiwa, kwa sababu kilimo cha watu wa Pemba ni kilimo cha mabondeni sana na sio kilimo cha tambarare. Kwa hivyo, wakulima wengi wamekosa chakula mara hii kutokana na joto na jua kali lililotokezea na mavuno ya mpunga yamekuwa madogo.

Mhe. Spika, je wizara hapa itafanya utaratibu gani ili kuhakikisha baina ya pande mbili kwamba wizara inahitaji kuwa makini katika kuongeza miti kwa wingi, uzalishaji wa miti kwa wingi ufanikiwe mvua ili tuweze kupata angalau sehemu nyengine, ili tuweze kulima kilimo cha

kutegemea kilimo. Pia naamini kuwa wizara hii pamoja na mambo mengine ya mageuzi ya kilimo, tunajua katika mageuzi ya kilimo tunahitaji watu wetu watekeleze kwa vitendo, na watakapotekeleza kwa vitendo ina maana ni kuwakomboa hawa wakulima katika kilimo duni. Sasa sisi tunafahamu kuwa watu wetu wengi sana mpaka sasa hivi wanaendelea na kilimo kilichokuwa duni.

Je, wizara katika suala hili la kuwatoa wakulima wetu hawa katika kilimo duni, ambapo tunaamini kwamba kilimo chenyewe ni duni na hakina tija na kuweka mazingira mazuri ya kuwawezesha wakulima wetu kuwaongeza mapato yao. Je, wizara hapa itawasaidia kiasi gani, kwa sababu asilimia kubwa ya watu wetu wanategemea kilimo duni ambapo tija yake ni ndogo sana. Kazi kubwa, miezi sita wanakaa mashambani, lakini matokeo yake mavuno yanakuwa ni kidogo. Je, wizara hapa imelifikiria kwa kiasi gani suala hili. Atakapokuja Mhe. Waziri kufanya majumuisho na mimi katika masuala naomba aweze kunisaidia.

Vile vile Mhe. Spika, tunajua kwamba wizara imejipanga katika usambazaji wa mbegu, mbolea na dawa kadhaa katika maeneo mbali mbali. Lakini je, wizara imejipanga vipi. Mimi ninataka kuzungumza kwamba wizara hii isizungumze kitu kwa jumla, hivi mnatuweka katika sehemu mbaya Wawakilishi. Hebu jaribuni katika kutoa taarifa zenu twende Kimkoa au Kiwilaya. Hebu tupeni taarifa kiwilaya, wilaya fulani iko hivi, wilaya fulani iko hivi na wilaya fulani iko hivi. Pale ndio tutaweza kujipima, kwa sababu na sisi ni lazima tujitathmini katika majimbo yetu. Lakini mkitupa taarifa za kiserikali za jumla jumla, hapa mnatuweka hoi, tunaomba taarifa zenu kwa mara ya pili angalau mgusie, kwa sababu tuna majimbo 50 na tunazo wilaya zetu, basi angalau mtuambie katika wilaya hii haina maendeleo namna kadhaa ya kilimo, ili tuweze kujipanga vizuri na tuweze kuzungumza na watu wetu vizuri. Huo ni kama ushauri ambao namshauri.

Mhe. Spika, ni pamoja na hivi vifaa vingine vya usambazaji wa mbolea, dawa na mambo mengine. Tunamuomba Mhe. Waziri ajue kuwa kuna baadhi ya sehemu wanakosa vifaa hivi. Kwa hivyo, ahakikishe kwamba zinapotolewa dawa za kuulia magugu au dawa za kusaidia mipunga kuja juu, basi dawa hizi ziweze kuwekwa kwa ukamilifu kabisa.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungumza ni kuhusu hawa wakulima ni lazima wapatiwe maelekezo, bila ya kupewa maelekezo wakulima hawawezi kufanya jambo lililokuwa zuri la maendeleo, ambapo maelekezo hayo ni ya utumiaji huu wa teknolojia ambazo zinatoa uzalishaji mzuri. Ni lazima tubadilike kutoka ile ya asili na tuingie katika mpango mpya wa maendeleo, ni lazima tuwaelekeze, tuwaelimishe na ni lazima tuwe na wataalamu wa kuwasaidia hawa kuweza kutumia hizi teknolojia mpya. Kwa sababu tunaambiwa sasa hivi tunataka kutumia teknolojia mpya na hali ya watu wetu bado wako duni katika uzalishaji na kielimu.

Kwa hivyo, hilo suala Mhe. Waziri alielewe kwamba hii teknolojia mpya ya kupata uzalishaji bora na kuweza kuziwezesha hizi sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kuimarisha soko la pembejeo za kilimo. Mambo kama haya utayafanikisha kwa kiasi gani Mhe. Waziri, kwa sababu ya hii teknolojia mpya. Mhe. Waziri uje utupe maelezo juu ya hili suala la teknolojia mpya ambayo unahisi hii itaweza kuwasaidia wakulima. Vile vile katika hizi sekta za binafsi ambapo watashiriki katika kuliimarisha hili soko la pembejeo za kilimo. Pia suala hili litasaidiwa kwa kiasi gani.

Halafu kuna suala zima Mhe. Spika, la usarifu wa mazao ya chakula. Hapa tunahitaji vile vile Mhe. Waziri, watu wetu elimu yao ni ndogo na uwezo wao wa kusarifu mazao bado ni mdogo. Je, Mhe. Waziri ni hatua gani atachukua ya kuhakikisha kwamba katika usarifu wa mazao ya chakula kutakuwa na hatua kadhaa wa kadhaa katika kuwasaidia watu hawa.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, dakika tano bado.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante. Kwa hivyo, Mhe. Spika, katika kupunguza umaskini ni lazima tuweze kutekeleza mambo yetu vizuri. Kuna hili suala zima la upungufu wa chakula na ziada ya chakula, ambapo sisi tunasema tunataka tupate chakula cha uhakika. Vipi tutaweza kupata chakula cha uhakika katika nchi hii, vipi tutajitosheleza katika chakula, na vipi tutaweza kusafirisha chakula tukapeleka nje. Je, imeshafikia hatua hiyo ya kuweza kusafirisha. Je, tunasafirisha kiasi gani cha chakula kupeleka nje, au uzalishaji wetu wa ndani, wananchi waliokuwa hawamo katika maeneo ya uzalishaji mkubwa, wananchi waliobakia wanafaidika kiasi gani kwa chakula kile ambacho kinazalishwa na wakulima wakubwa. Kwa sababu naamini katika chakula chote kinachozalishwa pengine mchele safi utakuwa labda tani 20, zinauzwa vipi hizi tani 20 au tani 30 zitakazopatikana zinauzwa kwa nani, mbona hatuoni uuzaji wa mchele ambao unaovunwa au wanauziana wenyewe au wanakula wenyewe. Mhe. Waziri akija kufanya majumuisho atueleze kwamba tumeanza kusafirisha tani kadhaa, au tumewauzia wananchi kadhaa.

Mhe. Spika, kwa kuwa unasema muda unakimbia mbio na dakika zenyewe kidogo, labda niendelee kwa maswali kidogo na muda uliobakia nitaweza kuzungumzia mengine. Nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwamba katika kunyanyua hali ya uzalishaji wa chakula Zanzibar, je ni wawekezaji wangapi walio ndani na wale ambao waliopatikana kutoka nchi za nje ili kusaidia mwelekeo wa chakula Zanzibar.

Mhe. Spika, katika elimu wanayopewa vijana kwenye usarifu wa mazao ya kilimo, ambayo ni sehemu ya ajira zao. Je, serikali inawawezesha kiasi gani kufikia malengo yao. Swali jengine, ni nini mtazamo wa serikali kwa siku za baadae.

Mhe. Spika, swali jengine ni kuwa Je, wizara yako imewawezesha kwa kiasi gani sekta binafsi katika kuimarisha soko la pembejeo za kilimo. Swali jengine Mhe. Spika. Je, Mhe. Waziri ili wakulima wawe wazalishaji bora, unahisi elimu ya teknolojia watakayopewa itachukua muda gani kuitekeleza kwa vitendo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo nataka nilizungumze ni hali ya matunda hapa visiwani. Sisi tunasema mbali ya chakula lakini tunahitaji kuwa na mboga mboga pamoja na matunda. Hivi kweli wizara hii ina msimamo wa kiasi gani katika suala la uzalishaji wa matunda, ni jitihada gani zimechukuliwa ili kuhakikisha kuwa nchi hii ina michungwa ya kutosha, milimau ya kutosha, midimu ya kutosha, nyengine tunatumia ndani ya nchi yetu na nyengine tukaweza kusafirisha. Haya ni majukumu ya Wizara ya Kilimo na Maliasili na Wizara ya Kilimo na Maliasili ina wataalamu wengi mimi nina hakika hiyo. Kwa hivyo, tuweze kujua kwa upande wa suala hili.

Mhe. Waziri atakapokuja hapa angalau aweze kutuelezea hatua zilizoweza kufikiwa juu ya suala la matunda, kwa sababu nahisi kwamba mpaka sasa hivi hatujaweza kujitegemea kwa matunda, matunda tunaagizia kutoka nchi za nje, hata mboga mboga tunaagizia kutoka nje. Hivi kweli hii wizara iko *very serious* katika mambo haya. Mimi naona ikiwa kama sisi tunataka kuuza sera zetu Zanzibar, ni mahodari sana wa kutengeneza sera, ni mahodari sana wa kupanga na kwa maelezo mazuri sana na utafurahi kwa maelezo. Lakini katika vitendo na utekelezaji hakuna kitu.

Kwa hivyo, ni miaka mingi tunazungumzia mambo haya ya matunda, sasa hivi kila kitu kwa jirani, mboga kwa jirani, matunda kwa jirani na mchele kwa jirani. Huu tulionao bado haujatosheleza tunachukua kwa jirani. Pia tunaagizia mchele kutoka nje, angalia fedha za kigeni ambazo tunazitumia Zanzibar kwa kuagizia michele kutoka nje. Ni kiasi gani cha pesa ambacho tunakitumia kununua mchele nje. Kwa nini hajatuambia Waziri kwamba tumeweza ku-*minimise number of* tani zinazotoka nje, sasa hivi tunaagizia tani kidogo kwa sababu ya uzalishaji wetu wa ndani. Haya ni mambo ambayo Mhe. Waziri ni lazima ayaelewe kwamba ni *give and take. Give and take* hapa Zanzibar hakuna.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, muda umekwisha.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: kilichokuwa ni *importation* hakuna *exportation.* Kwa hivyo, Waziri aje atusaidie sana katika suala hili. Mhe. Spika, nakushukuru sana na mimi naunga mkono hoja, ahsante.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii leo ya kuchangia kitabu hiki cha Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili. Vile vile namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kutuamsha salama na tukafika hapa.

Mhe. Spika, nikianza kuchangia mchango wangu katika kitabu chetu hiki ambacho kimeandikwa mapinduzi ya kilimo. Mhe. Spika, mapinduzi ya kilimo kwanza inataka sisi wenyewe tuwe na mapinduzi ya imani, tuwe na imani na tuwe na uzalendo, bila ya imani na uzalendo basi hatuwezi kuwa na mapinduzi ya kilimo.

Kwanza Mhe. Spika, nitakwenda katika kilimo cha mpunga. Wananchi wetu wengi wa Zanzibar kilimo chetu ni kilimo cha mpunga, lakini katika kilimo hiki kwa sisi wa Zanzibar tunahitaji mvua za Mwenyezi Mungu ambazo ni mvua za wakati, hatuna umwagiliaji maji kama wenzetu. Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba kwanza awatumie wataalamu wake kuwatangazia wakulima nyakati za kulima zinapofika, ili ahakikishe kuwa wakulima wanalima kwa wakati.

Pili Mhe. Spika, wakulima wetu wanachelewa au wanacheleweshwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili. Mkulima anatarajiwa alime wakati wa mwezi wa Oktoba, lakini mkulima yule halimiwi mpaka mwezi wa Novemba au mpaka mwezi wa Disemba na wakati wa Disemba kunakuwa na mvua kubwa, kwa hivyo mkulima anafeli.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili ahakikishe kwamba wizara yake wananchi wanalimiwa kwa wakati. Mhe. Spika, wakulima wetu ni wanyonge, huwa anaipata pesa kwa shida, sasa ikiwa hakulimiwa ule mpunga basi anakula hasara, na hatima yake hana cha

kukila tena. Pesa wizara inachukua lakini wakulima hawalimiwi, lini watazipata haijulikani, wazidai wapi, hajui mtu.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili hili jambo alitizame sana kwa wakulima wetu wanavyocheleweshwa wakati wa kulima. Serikali inawatangazia wakulima wa mipunga kuwa wana mbolea ya uhakika na nyingi. Lakini mbolea Mhe. Spika, haipatikani.

Mimi kwa kule kwetu Kaskazini kuna sehemu moja inaitwa Kwa Binti Said ambayo ndio kituo kimoja cha kilimo, lakini pale mkulima anayelima katika bonde lile la Kihemarini wakati anapotaka kwenda kununua hiyo mbolea, anaambiwa mbolea hapana. Sauti inayotumika katika Zanzibar hii, kila kitu utaambiwa kimechukuliwa na wakubwa. Sasa wakubwa hawa wakubwa gani? Kwa mfano, ukienda pale yule Afisa anayegawa mbolea akenda mwananchi akitaka mbolea anambiwa hapa mbolea tayari imeshachukuliwa na wakubwa. Sasa mkubwa gani hajulikani. *(Makofi)*

Lakini ukikaa muda mdogo utaona watu wanauziana vipakti Kinyasini pale. Kwa hivyo, hawa wakubwa wanazichukua mbolea za wananchi kwenda kuziuza kidogo kidogo. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri awaangalie hawa ni wakubwa gani wanaochukua mbolea na wananchi wakakosa. Hilo moja. *(Makofi)*

Jambo la pili ni kwamba Serikali inawatangazia wananchi dawa ya magugu. Kwa kweli dawa ya magugu hazipatikani na ninamuomba Mhe. Waziri suala hili aliangalie kwamba dawa zinauzwa kwa njia za magendo na wala wananchi au wakulima hawapati dawa. Kwa mfano, Serikali inauza dawa shilingi 6,000/= na mwananchi anauziwa shilingi 16,000/= na haya mambo yanatendeka Mhe. Spika. *(Makofi)*

Kwa hivyo, lazima wizara iwe makini, kwani wakulima wetu wanadhoofika wanakosa kulima, hawalimiwi mpaka watoe fedha kwa mlango wa nyuma na hili linatendeka na linadhoofisha wakulima wetu, kwani wakulima wetu ni wanyonge na lazima tuwaonee huruma. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende kwenye ukusara wa 16 kuhusu Utafiti wa Kilimo. Mhe. Spika, Maafisa wetu wa Kilimo, hivi sasa lazima wafanye utafiti katika ardhi ya maweni nayo itoe mpunga, kwani ziko sehemu za maweni zina dongo zuri tu la kutoa mpunga.

Kwa hivyo, nawaomba wataalamu wafanye utafiti mkubwa, ili watu wa maweni wapate kulima mpunga kama tulivyoambiwa kwamba ziko mbegu zinatoka mpaka maweni, lakini bado hatujazipa na watu wa maweni tumezingojea na tuliambiwa kwamba mwaka huu tutazipata na matokeo yake hatukuzipata. Kwa maana hiyo, namuomba Mhe. Waziri atufanyie mpango na sisi watu wa maweni tunaokaa kule Matemwe tuzipate mbegu za maweni kwa ajili ya kuendeleza kilimo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nisipoteze wakati wako mkubwa na waheshimiwa wajumbe wengi wamechangia jambo hili. Lakini namuomba Mhe. Waziri aangalie sana wakulima wa mpunga kwamba wanacheleweshwa na kutakiwa watoe fedha za chau chau na wengine hawana.

Kwa hayo, machache ahsante sana na ninaunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, tunashukuru. Sasa nimkaribishe Mhe. Hamza Hassan Juma na baadaye Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikazungumza machache, kwa ajili ya kumuongezea nguvu Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili, ili tuweze kupata chakula cha kutosha katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa kazi nzuri ambayo inafanyika, pia kwa kutuletea muhtasari wa Ripoti ya Utekelezaji wa Kazi zao za mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kwa ardhi ya kulima. Kwa kweli hatuwezi tukazungumza kilimo kama hatuna ardhi ya kulima na wala sioni mipango endelevu ya Serikali mpaka hivi sasa ya kuhifadhi ardhi ya kilimo. Mhe. Spika, hivi sasa ukienda Darajani pale hasa siku ya Ijumaa utawakuta watu wengi pale hasa akina mama wanakaa chini ya Msikiti na kuomba, mwenye kumgaia shilingi mia moja, nusu shilingi, senti kumi. Lakini tujiulize wale wote kweli walikosa kazi ya kufanya?

Mhe. Spika, wananchi hawa wengine walikuwa wakilima katika maeneo mbali mbali kwa bahati mbaya hawakuwahi kuajiriwa ndani ya Serikali. Lakini watu hawa waliamua kujitegemea kwa kutumia jembe kwa kulima. Sasa kwa kuwa Serikali bado haijaweka mipango mizuri ya kuhifadhi ardhi za kilimo, Mhe. Spika maeneo yao wanakwenda wenye nguvu, fedha, mbavu zao na kuyachukua maeneo yao na matokeo yake wao baadaye hawana kazi ya kufanya na kukimbilia Darajani kwenda kuomba.

Sasa Mhe. Spika, suala hili tusilifanyie maskhara hata kidogo. Kwa kweli tumeshuhudia katika Mkoa wetu huu wa Mjini na Magharibi maeneo mengi ambayo yaliyokuwa yakilimwa mpunga hivi sasa tayari maeneo yale yameshavamiwa na kuna nyumba za watu za makaazi.

Kwa hivyo, baada ya kumaliza mabonde ya Mkoa wa Mjini Magharibi wataelekea wapi? Wataelekea Kibokwa, Cheju pamoja na maeneo mengine. Sasa jambo ambalo ninaloliomba Mhe. Spika, ni kwamba Serikali iweke mpango maalum na siku zote tunazungumza masuala ya *Land Use Plan*, yaani hatuna Mpango Mahsusi ya Matumizi ya Ardhi.

Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Spika, ili omba omba wasiongezeke, basi tunaomba hayo maeneo ambayo yanayotumika kwa kilimo hivi sasa tuwaambie wananchi basi, Mhe. Spika tunayo ardhi nyingi *coral* ambayo sio *fertile* na siyo ya kilimo au haina rutba. Mhe. Spika, naiomba wizara na labda hili Mhe. Waziri aje anisaidie maelezo kama Wizara yake hili wameliona na kama wameliona watalilinda vipi.

Mhe. Spika, kuna maeneo mengi ambayo yamechukuliwa ambapo wananchi walikuwa wakilima hata eneo la Tomondo, yaani ukenda eneo la Tomondo hivi sasa limejaa majumba, lakini maeneo yale kwa muda mwingi yalikuwa ni maeneo ya kilimo.

Kwa mfano, hivi sasa Mhe. Spika, kuna bonde liko Kinuni, Mhe. Spika katika Bonde la Kinuni pale Skuli ya Kinuni, eneo lile Mhe. Spika lilikuwa zaidi linatumika katika kulima mpunga na mazao mengine. Hivi sasa eneo lile au bonde kwa mtu ambaye analijua na kuna wakulima wa pale niliwahi kukutana nao kipindi fulani na nilikwenda pale na kukagua lile eneo na kutoa angalizo kwa sheha, kwamba pale watu walipofika kujenga iwe basi.

Mhe. Spika, wananchi wale hawana kazi ya Serikali na kwa bahati nzuri wengine wamestaafu kazi zao kama vile wengine walikuwa majeshi na kazi nyengine mbali mbali, basi mpunga anaolima pale anautumia kwa muda wa mwaka mzima na wala dukani hakujui. Lakini leo Mhe. Spika bonde lile kama sikosei kama wakulima wamebakia basi labda wanne na pale.

Kwa hivyo, pale kipindi nilichokwenda kuna mama mmoja alikuja kunilalamikia kwamba mwenzake amepigwa na kulazwa hospitali, amepigwa na kulazwa hospitali kwa sababu yeye analima mpunga akaja mtu mwenye nguvu zake na kuteremsha gari za mawe.

Baada ya kazi hiyo, akamwambia hakikisha nakupa mwezi mmoja uvune mpunga wako nakuja kujenga, mwanamama akagoma, kugoma matokeo yake mawe yanateremshwa akenda kufanya fujo, akachezea vibao na kulazwa hospitali na kesi ilikwenda mpaka Kituo cha Kwerekwe. Kwa kweli hii ndio kadhia wanayoipata wazee wetu katika maeneo yao ya kulima.

Sasa kwanza namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atafute muda na kwenda kulitembelea lile Bonde la Kinuni, kwa ajili ya kuwahakikishia wananchi wa pale kwamba lile eneo litaendelea kuwa salama.

Jengine Mhe. Spika, tunazungumza sana ukulima katika maeneo ya mabonde ya mpunga pamoja na maeneo mengine. Lakini bado sijaona mikakati ya Serikali katika kushughulikia wakulima wanaolima vilimo vya maweni. Mhe. Spika, mimi kwetu na siku zote nasema kwetu Makunduchi mara Chaani, kwa sababu ndio mzaliwa, sasa na leo nasema Matemwe kwetu.

Kwa mfano, enzi hizo wazee wetu wa Matemwe kule akikupiga kibao Mhe. Spika, basi kaburini moja kwa moja kwa sababu nini, walikuwa na nguvu. Watu wa Matemwe walikuwa hawanuni chakula dukani na hayo maduka hayakuwapo na watu wanalima mahindi, mtama, mawele, mihogo, viazi vikuu pamoja na vitu vyengine, yaani watu walikuwa na nguvu sana.

Wanalima na mazao yanakaa hakiba kwa muda mrefu na Mhe. Abdi Mosi Kombo ameondoka hapa, lakini angeliniunga mkono katika hili, kwamba wazee wetu walikuwa na nguvu sana. Lakini leo hakuna kilimo kingi kama walivyokuwa wanapata kipindi hicho na mtama walikuwa wanalima mwingi sana.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hebu tufanye utafiti kwa nini mazao ya maweni nayo yameanza kupungua. Mhe. Spika, nadhani hilo tukifanikiwa tutaweza kuongeza kiwango cha chakula katika nchi yetu. *(Makofi)*

Vile vile kuhusu suala la mpunga. Mhe. Spika, tunashukuru sana jitihada pamoja na mipango ya serikali yetu. Lakini bado namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba awasimamie watendaji wake kwa kilimo cha mwaka huu cha mpunga Mhe. Spika tulifeli sana.

Katika kitabu cha Mhe. Waziri ameeleza kwamba wametafuta mbolea, wamelima na wametumia matrekta.

Lakini Mhe. Spika, nataka niseme kwamba niliangalia Bango Kitita la Wizara na bila ya shaka wametayarisha mwezi wa Januari na kuliwasilisha kwa Mhe. Rais nafikiri kwenye mwezi wa Machi na walisema kwenye Bango Kitita kwamba mbolea walinunua *hundred percent* tani 245 na kidogo.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati anatakapokuja aje anisaidie maelezo, kwamba kuna tani nyengine 200 ambazo ziliagizwa Tanzania Bara mbolea hii kwa taarifa tuliyonayo, mbolea hii ilifika hapa kama sikosei ilikuwa mwezi June kwenye tarehe 02 au 03. Lakini kwa bahati mbolea hii iliyonunuliwa Tanzania Bara, kwa hivyo sijui kama ndio hii ambayo imo kwenye Bando Kitita iliyoandikwa kwamba tayari imeshanunuliwa *hundred percent*.

Kwa maana hiyo, kama *hundred percent* ilinunuliwa na ikaoneshwa kwenye Bango Kitita kwenye mwezi Machi/Aprili, sasa hii iliyonunuliwa June, ina maana kuna mbolea ya ziada iliyonunuliwa kutoka Tanzania Bara.

Kwa hivyo, kwanza nataka katika lile Bango Kitita ile mbolea waliosema tani 245 na tani nyengine 300 za *UREA* na *TSP* zilitoka nchi gani na hizi tani 200 zilitokuja zilitoka nchi gani? Kwa nini nikauliza hivyo. Mhe. Spika, mbolea hii tumepata taarifa kwamba kwa wenzetu Bara kule mbolea hii ilileta matatizo na kwa bahati kuna baadhi ya wakulima waliopewa hapa mbole mipunga yao imeungua.

Sasa mimi nina wasi wasi pengine hii mbolea iliyotoka Bara ambayo iliyoleta athari kule na wenzetu kuwe Wizara ya Kilimo Bara walikubali na kusema wanakwenda kuifanyia utafiti je mbolea ile ilikuwa na matatizo gani. Kwa hivyo, kama mbolea ile iliyonunuliwa Bara na hapa wenzetu hawakuifanyia utafiti na kwenda kuwapa wakulima na mipunga yao ikaungua.

Mhe. Spika, hapa itabidi Serikali lazima ibebe dhamana, kwa sababu wananchi walijenga matumaini kwa kutegemea kwamba wanapewa mbolea na serikali na tunashukuru bei imekuwa ya chini kabisa, lakini baadaye mbole ile ile ikawa inauzwa bei kubwa kabisa. Mhe. Spika, naomba majibu katika hili na vyenginevyo nitakuja kuwa mgumu sana kwa hii taasisi inayoshughulikia masuala ya mbolea, lazima tupate maelezo ya kutosha.

Vile vile tunataka tujue hii mbolea iliyokuja kutoka Bara tani 200 hivi sasa iko wapi au wameshapewa wakulima wote na kama wamepewa ni mabonde yepi?

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo nataka kulizungumzia ni kuhusu Karakana ya Matrekta na mwenzangu ameisifu sana na wala mimi sitaki nipoteze muda mwingi kuisifu. Kwa kweli Mhe. Spika, pale tumekwenda kutengeneza wataalamu lakini tukashindwa kuwapa nyenzo. Mhe. Spika, wataalamu waliopo Mbweni kama walivyoeleza wenzangu ni wataalamu wazuri sana, lakini bado mashine wanazozitumie ni zile za enzi Said Baraghash. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba kwamba karakana ile ishughulikiwe na pia tuliitaka Serikali, kuwa Karakana ile isitumiwe kama idara, isipokuwa tulishauri iwe shirika, kwa sababu ikiwa shirika

basi karakana ile itaweza kujitegemea, kwani kwanza wanafanyakazi za kuingiza fedha nyingi lakini fedha zile wao wenyewe hawana uwezo wa kuzitumia. Vile vile hata hayo matrekta yanayoharibika Mhe. Spika, hao wakulima matrekta yanapoharibika, basi inabidi kuja kufanyiwa ukarabati pale.

Kwa hivyo, nataka nimuulize Mhe. Waziri kwamba Serikali ilikuwa imo katika mchakato wa kuangalia ile Karakana ya Matrekta Mbweni aidha wataifanya shirika au kitu gani, kwa sababu kuendelea karakana kuwa kama idara Mhe. Spika bado hatuwatendei haki wananchi wetu ambao ndio wakulima wetu wa hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, najua unaangalia *time* na nimeshasikia kwamba bado dakika zangu tano. Sasa nataka nizungumzie kuhusu Idara ya Misitu na hapa nitazuia fungu la Idara ya Misitu Mhe. Spika, tena kwa sababu maalum, kwani uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanyika hapa Zanzibar hasa ukataji wa miti unasababishwa na Idara ya Misitu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika idara hii nitakuja kuzuia fungu kwenye mapato naanza kumwambia kabisa Mhe. Waziri. Kwa kweli Idara ya Misitu haikusanyi kodi katika ukataji wa miti, ninavyojua mimi sheria zao ukikata mti, yaani mnazi umeupanda mwenyewe ukitaka kuukata unalipishwa ada karibu shilingi 3,000/= zamani ninavyojua mimi na hivi sasa nadhani ada imezidi atakuja kuniambia Mhe. Waziri.

Lakini tujiulize leo kuna minazi mingapi inayokatwa kwa siku Mhe. Spika kuna Vitanda vya Minazi hivi sasa kila pahala na kuna minazi mwengine hata haijabaleghe vizuri inakatwa, yaani ile mbao wakati inapochanwa basi ule mti bado haujakuwa mbao. Leo Idara ya Misitu iko wapi pia kuna mishelisheli na mifenesi inakatwa ovyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kama una shamba la mishelisheli na mifenesi siku moja fanya usafiri kama wiki tu umekwenda Dar es Salaam ukija unaukuta uwanja wa mpira msumeno wa moto umeshafanyakazi yake. Mhe. Spika, Idara ya Misitu bado haijafanyakazi yake, kwa hivyo tunataka Mhe. Waziri hivi sasa usikae juu ya kiti isipokuwa tunataka uwakurupushe Wakurugenzi wako na kila mmoja anawajibika kwenye maeneo yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Idara ya Misitu haifanyikazi yake vizuri na hivyo nitakuja kutaka maelezo ya kina. Kwa mfano, leo kila siku ukipita katika maeneo mbali mbali kuna magogo shehena kwa shehena yanapitishwa yanakuja mjini, Mhe. Spika lazima tuje tupate maelezo ya kina. *(Makofi)*

Vile vile katika hivi viwanda ambavyo vinatumia magogo asilia ya Zanzibar, je kuna utaratibu gani walioekewa, ili kuhakikisha kwamba wanakaguliwa na kujua kuwa yale magogo yanayopelekwa pale yanavyo vibali. Mhe. Spika, hili nitakuja kuhitaji kupata maelezo ya kutosha kabisa, vyenginevyo rafiki yangu, ambaye ni swahibu wangu Mhe. Suleiman Othman Nyanga kumpiga buti wewe mwenyewe utakuwa unaona haya, maana yake hana tabia ya kusema sana. *(Makofi)*

Lakini naamini katika jawabu zake watendaji wake, kwa sababu buti utafute pakupiga sio kwa mtu ambaye ni swahibu, mufti Mhe. Suleiman Othman Nyanga ni mufti. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namalizia ili usije kuniambia nikae kitako. Mhe. Spika, nataka nimalizie katika Miradi hii ya *TASAF*. Kwa kweli wananchi wetu kupitia Miradi ya *TASAF* wameibua miradi mingi ya kilimo katika suala zima la umwagiliaji maji. Lakini bado wakati mwengine wanakuja kukwama katika suala zima la usimamizi hasa kwenye masuala ya umeme pamoja na mitaro ya kupelekea maji katika mashamba. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika hasa katika yale maeneo ambayo wananchi wameibua miradi yao ya kilimo cha umwagiliaji maji, basi waweze kuwashughulikia.

Jambo jengine ambalo ni dogo kabisa ni kuhusu wasasi. Mhe. Spika, wasasi mumewatupa kwa sababu zamani mpaka kwenye redio unasikia vikorombwe enzi zetu. Mhe. Spika, kama ingekuwa inaruhusiwa basi ningepiga kikorombwe maana mimi ninajua nimeshawahi kusaka, lakini najua hutaniruhusu. *(Vicheko)*

Mhe. Spika, wasasi wametupwa. Kwa mfano, zamani tunajua ukuja pale Kibanda Maiti kuna muwembe mkubwa pale na mbwa wa kila aina unawakuta pale wanakwenda kusaka nguruwe na hivi sasa nataka nimuulize Mhe. Waziri wale nguruwe wamekwisha? Kima bado wapo na wanaharibu mazao ya wakulima, wasasi wanaomba fedha za kununulia marisao pia hawapewi, sasa hawa wasasi jamani au kazi yao basi tena.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri wakati atakapokuja aweze kutusaidia pia.

Mhe. Spika, unajua Jimbo langu la Kwamtipura, sasa mazingira ya Kwamtipura wasasi ndio kwao, sasa lazima nihakikishe kwamba ile taaluma yao inaendelea kudumishwa, ili isije ikapotea kabisa.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nataka nikushukuru zaidi kwa kumalizia Chuo cha Kilimo Kizimbani. Mhe. Spika, katika kitu ambacho ninachokiomba Mhe. Waziri akae na Waziri mwenzake wa Kilimo cha Tanzania Bara. Hivi sasa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete yeye ndio amekabidhiwa bango katika nchi za Kiafrika kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Bara la Afrika linajitegemea kwa kilimo anao mpango mzuri sana Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete.

Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri wetu wa Kilimo akae na Waziri mwenzake wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aangalie zile *programs* na Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete hivi sasa anataka kusomesha vijana karibu 200 kwa ajili ya utafiti tu wa kilimo na wala sio mambo mengine, yaani utafiti tu kwa sababu kilimo bila ya utafiti Mhe. Spika hatuna kilimo.

Sasa sijui chuo chetu hichi tunahusishwa vipi na wenzetu wa Jamhuri ya Muungano, kwa sababu kama tulivyosema kwamba bango au mwavuli wetu ndio wanao wao. Kwa hivyo, Mhe. Waziri akaingie kwenye mwavuli wetu ule ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukae, ili kile kivuli na wewe upate yale matunda kwa ajili ya ile neema itakayopatikana.

Tunashukuru Serikali ya Marekani kwa kuweza kukubali kuufadhili mradi ule na Mhe. Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete alikwenda katika Kikao cha *G8* akawasilishe ule Mpango wa Afrika, naamini na Zanzibar imo.

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nataka niseme kabisa kwamba kuna Idara hii ya Umwagiliaji Maji iliyopo hapa, idara hii haifanyikazi vizuri. Kwa hivyo, tunamuomba sana Mkurugenzi kupitia kwako Mhe. Spika akae na wafanyakazi wake kwa ajili ya kupanga nao kazi, kwa sababu tatizo liliopo pale Mhe. Spika kuna ubaguzi na mimi nasema hivi, kwamba kuna ubaguzi na kuna watu maalum yanapokuja mafunzo au semina ama chochote kile basi ndio hao hao, kwa maana hiyo hatutaki yale yameshakwisha. *(Makofi)*

Hivi sasa tunataka wafanyakazi wote tuhakikishe tena nitamuomba Mhe. Mwenyekiti wa Kamati safari hii atakapokwenda angalie wafanyakazi katika hii Idara ya Umwagiliaji Maji, wafanyakazi wangapi waliopo pale? Wangapi
wamepata mafunzo? Wangapi wamekwenda katika semina? Ili tunataka tujue hivi sasa wananchi wetu wafanyakazi kwa kuamini Serikali yao haina tena maskhara na inataka wananchi waweze kujitegemea. *(Makofi)*

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, pia naomba mafuta. Kwa maana hiyo, mtu mwenye kupewa fedha za mafuta katika fungu lake, basi mafuta ya idara ayaache kwa ajili ya kwenda kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya hayo machache na kushukuru sana na nitaunga mkono baada ya maelezo ya Mhe. Waziri ambayo naamini atanileta maelezo mazuri. Mhe. Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana na sasa tumkaribishe Mhe. Ali Salum Haji na baadaye Mhe. Farida Amour Mohammed.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, kwanza kabisa na mimi nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake. Lakini zaidi Mhe. Spika, shukurani zangu za pekee naomba nimpolekee Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa sababu ameonesha msukumo wa hali ya juu katika kutaka mafanikio ya Mapinduzi ya Kilimo. Kwa bahati nzuri Rais wetu ni msikivu, muelewa pia ni mstahamilivu. Lakini Mhe. Spika, pamoja na jitihada za Mhe. Rais wetu bado Wizara ya Kilimo na Maliasili ina matatizo ya hapa na pale.

Kutokana na hali hiyo, naomba sana niwapelekee ujumbe watendaji walioko juu, kwamba Baraza lako Tukufu la awamu hii lina mabadiliko makubwa na linafanyakazi kwa umakini ulio mkubwa sana. Sasa niwaombe kwamba tuwe tayari kubadilika.

Mhe. Spika, katika Wizara ambayo imebahatika kupata miradi mingi ya wafadhili basi ni Wizara ya Kilimo na Maliasili. Lakini ninachoonekana Mhe. Spika, kwamba watu au watendaji wetu bado hawajawa *serious* katika kusimamia hii miradi au mipango yao haiko endelevu. Kwa nini niseme hivyo Mhe. Spika. Mimi nataka nitoe mfano katika miradi kama miwili. Kwa mfano,

kuna Mradi wa *PADEP*, mradi huu ulifanyakazi Unguja na Pemba na uliongozwa na Mratibu wetu Dkt. Kassim Biwi ambaye hivi sasa amestaafu karibuni miaka 7.

Lakini kinachoonekana Mhe. Spika, baada ya mratibu huu kustaafu, huu mradi inaonekana ameondoka nao na wala hauonekani uendelevu wake na kama upo uendelevu wake basi Mhe. Waziri wakati atakapokuja basi atanielezea unaendelea vipi. Mhe. Spika, tukiachilia mradi huo, kwa sababu mradi huu umekosa ufanisi naanza kupata mashaka na miradi mingine. Kwa mfano kuna Mradi wa *ASSP* na *SDPL*, ambao uko ukingoni kumalizika, kwa bahati nzuri mradi huu unasimamiwa na Dkt. Zaki.

Mhe. Spika, mashaka yangu ni kama ule mradi wa mwanzo kwamba watu wetu hawana utaratibu mzuri wa kusimamia hii miradi, ili pale wafadhili wetu wanapoondoka na serikali kutia mkono wake kwa ajili ya kuzijali zile fedha za wananchi, kwa sababu tunachukua fedha za wananchi ambao ni wavujajasho tena ni wanyonge, lakini mwisho mradi hauna mafanikio.

Vile vile mradi huu pia una mashaka, ambapo kuna wajanja wa mradi huu wanajaribu kuzichukua hizi fedha na kuzitumia katika maeneo mengine na hususani katika safari za kikazi, ambazo zinaonekana mafungu yake yamemalizika. Kwa hivyo, niwaombe kuwa waadilifu katika hili na Mhe. Waziri wakati atakapokuja naomba anielezee juu ya kadhia hii.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nielekee katika Bodi ya kupitisha Tenda ya Wizara. Mhe. Spika, serikali imepitisha kwa nia nzuri tu uanzishwaji wa kuundwa kwa bodi. Lakini Mhe. Spika, kinachoonekana ni kwamba Bodi ya Wizara ya Kilimo bado imekumbwa na changamoto nyingi na watu wanaonekana kwamba wajumbe wale wameendekeza maslahi binafsi zaidi kuliko maslahi ya Serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, na hili nazungumza hata Katibu Mkuu analifahamu vya kutosha na tayari ameshajaribu kufanya vikao kuwaita Wajumbe wa Bodi katika hili. Kwa maana hiyo, nawaomba sana Wajumbe wa Bodi wasimuangushe Katibu wetu ndugu Afani Othman katika hili, kwa sababu amekuwa ni mtendaji tena ni msimamizi mzuri katika kazi zake, lakini kinachoonekana ni kwamba wajumbe bado hawajawa makini. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, nawaomba sana watu wa Wizara ya Kilimo kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba tubadilike.

Sasa naomba nielekee katika Kilimo cha Mpunga kwenye suala zima la *NERICA*. Mhe. Spika, ninavyozungumza kwamba bado hatujajipanga basi lazima tukiri kwa hilo. Kwa kweli mbegu ya *NERICA* kinachoonekana, kwamba tulipotaka kuanzisha mbegu hii tumekurupuka haraka sana na tukaanza kutumia *Slogan* ya kumtumia Mhe. Rais kwa haraka sana bila ya kufanya utafiti wa kutosha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, utafiti wa *NERICA* haukufikia ukingoni na kinachoonekana kwa wakulima wetu, kwamba mbegu hii tayari wameshaanza kutoa matatizo kwamba wanamashaka nayo. Kwa hivyo, na zile sehemu ambazo zimejaribiwa kufanywa majaribio ikiwemo sehemu ya Bambi, hii *NERICA* inatiliwa maji kila siku na inaonekana bado haioneshi kwamba ni mbegu iliyobora na

kama ilikuwa inatakiwa kufanyiwa utafiti Mhe. Spika Zanzibar ni kubwa, ilikuwa tufanye utafiti na maeneo mengine kwa mujibu wa hali ya hewa ya yale maeneo yalivyo. *(Makofi)*

Lakini tumekurupuka na kutangaza *NERICA* na kumuweka Mhe. Rais mbele na wala hakuna mafanikio ya hii mbegu na wakulima wanaona zile mbegu wanazozitumia wao za asili zina faida zaidi kuliko hizi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anielezee hasa utafiti wa *NERICA* ulianzia wapi na umemalizikia wapi na nini hasa kinachoonekana na faida ya *NERICA* zaidi kuliko faida ya mbegu za asili. *(Makofi)*

Sasa anataka niingie ukurasa wa 24 kitabu kimeonesha jinsi ya serikali ilivyofunga mikataba na wakulima katika kununua mbegu na baadhi ya mbegu kununuliwa Tanzania Bara. Mhe. Spika, nataka niseme kwamba katika muongo tunaokwenda nao bado kuna malalamiko ya watu ambao wamefunga mikataba na Serikali katika kuuza mbegu, kwa sababu mbegu hazijenda kununuliwa na watu hawa wanapiga kelele.

Kwa kweli hapa sisi wengine tunapata mashaka, kwa sababu mbegu anayo mkulima ndani na mkulima yule mnyonge tutegemee nini? Tutegemee atakaa na mbegu wakati Serikali haikuja kununua, atakula mbegu yake. sasa atakapokula mbegu yake Mhe. Spika, ndipo Serikali itakapokurupuka Tanzania Bara kununua mbegu na hichi ndicho wanachokitafuta, kwa sababu wanapokwenda Tanzania Bara kuna mambo yao hapa yanajificha ya kupata maslahi yao.

Mhe. Spika, tunapotoa maelekezo basi tunaomba sana tuyafuate, tunaambia wakulima, tunafunga nao mikataba tutanunua mbegu, basi twende kwa wakati, ili wale wakulima wetu wasije wakazimaliza mbegu zao na wajanja wachache wakatafuta zile njia nyengine.

Mhe. Spika, nazungumza hili kwa ushahidi wa kutosha waliofunga mikataba wapo, mbegu ziko ndani na wameanza kula mbegu zao na Serikali bado haijenda kununua mbegu hizo.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo naomba nizungumzie dawa ya kuulia magugu. Kwa bahati njema sana Serikali yetu inaonesha kwamba inahitaji kuwasaidia wananchi wake, lakini bado nasema hatujipangi vizuri na wala hatukielewi hasa tunafanya nini, kwa sababu kama tunajipanga vizuri Mhe. Spika, unajua kwamba safari hii tunategemea wakulima idadi fulani watalima na kwa idadi hii tutahitaji dawa ya lita fulani, lakini hilo halipo.

Matokeo yake Mhe. Spika, Wizara imekwenda kununua dawa ya ***Hansulini*** kutoka China lita 20,000. Lakini kinachoonekana ni kwamba lita 20,000 zile hazikuwa zinakwenda sambamba na idadi ya wakulima. Kwa maana hiyo, wakulima wetu wameuziwa dawa kwa njia ya ulanguzi badala ya kuuzwa shilingi 6,000/= dawa hiyo iliuzwa kwa shilingi 22,000/= na maduka ya *PADEP* na wizara bado imekaa kimya wananchi wanalanguliwa pamoja na kupata tabu, matokeo yake faida halisi ya kuwasaidia wanyonge haionekani Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa sababu najali muda zaidi nakwenda kwenye *point direct*, sasa naomba niende kwenye ukurasa wa 38 kuhusu suala la umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, hapa nimshukuru sana Mkurugenzi wa Idara hii katika eneo hili kidogo jitihada zinaonekana lakini kuna changamoto ambazo zinawakabili. Niiombe Wizara basi ijitahidi ili kuondosha changamoto ambazo zinawakabili katika Idara hii na kuweza kuzidisha miundombinu ili matatizo yaweze kuondoka kwa haraka.

Mhe. Spika, na mimi naomba nitoe indhari kama walivyotangulia wenzangu, tuseme kwamba safari hii Wawakilishi wako tumekuwa karibu kufuatilia matatizo ya wananchi na kujawasemea katika chombo hichi cha sheria. Mhe. Spika, nina ushahidi wa kutosha kwamba bado suala la umwagiliaji maji lina upendeleo kwa wakulima wetu. Ninaeleza hivyo na naomba sana waangalie bonde la Mtwango *block* Nam. 1 na *block* Nam. 2 wakulima wanalalamika kwamba ndio limepewa kipaumbele katika umwagiliaji maji, hili ni tatizo.
Mhe. Spika, block hili limepewa kipaumbele kwa sababu ambazo zile wenyewe tunazijua ni *block* la watu fulani fulani, mambo haya yamepitwa na wakati Mhe. Spika. Hakuna mtu aliyekuwa juu kuliko mtu mwengine, wananchi wote wana haki sawa katika kupata fursa katika nchi hii.

Mhe. Spika, naomba niende ukurasa wa 31 maliasili. Mhe. Spika, Mwenyekiti wangu alizungumza kwa uchungu sana Mhe. Hamza Hassan Juma. Kwa sababu sisi Kamati yetu ni Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa ikiwemo Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ambayo inashughulikia na masuala ya mazingira. Tunapata tabu sana katika suala hili. Serikali inapoteza gharama kubwa sana katika kuhifadhi mazingira. Niwaombe watu wa Maliasili wajaribu kufuatilia maeneo yanayochimbwa mchanga yameonekana hayana usimamizi mzuri na watu wanachimba mchanga ovyo, matokeo yake kuharibu mazingira ya nchi hii. Hapa ni maombi tu ya kuiomba Wizara kuweza kujitahidi zaidi katika kuhifadhi masuala ya mazingira.

Mhe. Spika, nimalizie kwa kumtaka Mhe. Waziri atakapokuja anipe maelezo ya mgogoro uliokuwepo kati ya Wizara ya Kilimo na Shirika la Umeme. Mhe. Spika, kuna mgogoro Bungi katika kituo chetu cha Redio tulipoanza ujenzi wa mnara. Shirika la Umeme wanataka kupeleka umeme pale, wanataka kuchukua baadhi ya eneo moja, lakini Wizara ya Kilimo wanasema kwamba hapa hamchukui kama mtachukua miembe isikatwe na eneo jengine ambalo linaonekana lipo Shirika la Umeme wanasema sisi huko hatwendi. Hapa Mheshimiwa pana mvutano na Katibu hili analifahamu na tayari taasisi mbili za serikali zimeanza kuandikiana barua. Serikali tayari imeshaanza kutupa gharama katika kujenga mnara ule. Wananchi wanahitaji mnara ule umalizike kwa haraka ili tupate mawimbi ya redio katika nchi yetu.

Mhe. Waziri atakapokuja namuomba anisaidie lile tatizo la mvutano limeishia wapi kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar katika kuona hii kazi ya kupeleka umeme katika mnara wa redio inafanyika kwa haraka.

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, nitaunga mkono hoja hii baada ya kupata maelezo ya kutosha. Ahsante naomba kukaa.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuzungumza machache katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo na Mali Asili. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa hazina ya uhai ya kunisimamisha mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa na afya njema.

Pia nimpongeze Mhe. Waziri, jinsi alivyowasilisha hotuba yake nzuri kwa umakini na kwa muda unaofaa.

Mhe. Spika, niende moja kwa moja katika mchango wangu; naomba niende katika Idara ya Kilimo kama wenzangu wengi walivyoanza. Serikali yetu ina mipango mizuri lakini utekelezaji wake kiasi fulani unakuwa wa kusuasua. Serikali katika mpango wa kuendeleza Mapinduzi ya Kilimo, iliahidi kutoa ruzuku za pembejeo za kilimo na matrekta. Lakini kwa bahati mbaya sana hayo yote hayakuwezekana.

Kwa mfano, matrekta yapo mengi, lakini utaratibu uliotumika katika kupeleka matreka ndani ya mabonde yetu kwa wakulima haukuwa mzuri, haukuridhisha. Matrekta watu wamechangishwa pesa kwa kupelekewa matrekta na wamekubali, lakini matrekta yale hayakufika mpaka msimu wa kulima umepita. Kwa bahati mbaya watu wale wamekosa hata chakula chao wenyewe sikwambii cha biashara. Mambo haya yametokezea wazi na yanaonekana katika Wilaya yangu ya Wete hasa katika majimbo mawili ya Ole na Kojani; maeneo ambayo yalikuwa yanatoa mpunga kwa wingi mara hii Mhe. Spika, ni ya kwenda kuhaniwa, hayana hata chakula cha kula na watoto wao. Wamekosa tija hawakupata chochote kutokana na ucheleweshwaji wa matrekta hayo.

Nimuombe sana Mhe. Waziri, akisimama hapa atueleze hasa ili wananchi wetu na wakulima wetu waelewe. Wana utarabibu gani mzuri wanaoupanga kwa ajili ya kufikisha matrekta katika maeneo ya wakulima ili wakulima wetu wote wapate na wao. Hii azma iliyoletwa na viongozi wetu wa serikali pamoja na Mhe. Rais kwa kupata Mapinduzi ya Kilimo ili watu wote waneemeke. Isiwe ni maeneo fulani wanapata kulimiwa, maeneo fulani hayajapata, hilo ni baya Mhe. Spika.

Katika Idara hiyo hiyo ya Kilimo, Serikali yetu ya Mapinduzi ina matatizo ya kudharau pengine mambo yale ya kuendeleza. Kwa sababu mie kila siku nikisimama hapa katika kuchangia nasema jambo zuri linaigwa na jambo baya tunaliacha. Nakumbuka katika awamu za nyuma serikali yetu ilikuwa na mpango mzuri katika kuendeleza michipuo ya kilimo katika skuli zetu. Kulikuwa na mchipuo wa kilimo katika Skuli ya Sekondari ya Fidel Castro, kulikuwa kuna mchipuo wa mazao ya baharini Lumumba. Hapa Fidel Castro palitoa wataalamu wazuri wa kilimo ambao kuwa huko juu nina imani kama wapo sasa hivi. Kama Naibu Katibu Mkuu, Afisi Mdhamini Pemba, hawa ni wataalamu wetu wazuri mno ambao kuwa wangezalisha zaidi wataalamu ili kufikia hatua ile tuliyoikusudia ya kilimo kufanikiwa. Lakini kwa bahati mbaya sana haya yametupwa na haya hayakuendelezwa.

Naomba niishauri serikali Mhe. Spika, katika hili la Mapinduzi ya Kilimo. Kwanza naishauri serikali mchipuo wa kilimo urudi tena ndani ya Skuli zetu. Pia kuanzishwa ile mitaala ya kilimo katika skuli zetu za Sekondari, ili tukianzisha katika skuli zetu mitaala na michipuo ya kilimo kama awali kwa kutoa wataalamu tutakuwa hatuhitaji sana wataalamu kutoka nje, wataalamu wetu watatoka humu humu na watatusaidia. Hawa waliopo ni wataalamu wazuri lakini ni wachache Mhe. Spika.

Mhe. Spika, kwa kuendelea nije kwenye mazao ya kilimo. Nataka niende moja kwa moja kwenye jimbo langu la Ole ni Wilaya nzima ya Wete lakini nianze ndani ya jimbo langu la Ole. Kwa sababu ndani ya jimbo langu la Ole linazalisha sana matunda ya embe, embe huzaliwa mpaka ikashindikana ikawa hazina watu wa kuzitumia. Embe hizi zinazozaliwa kwa wingi ndani ya Jimbo la Ole na Wilaya ya Wete kwa jumla, yamekumbana na matatizo mawili makubwa mno.

Mhe. Spika, tatizo la kwanza ni wadudu waharibifu wa embe hizi. Nashukuru Wizara ya Kilimo imejitahidi sana kuleta mitego ya kutegea wadudu wale wa embe. Lakini ni bado, bado sana Mhe. Spika. Nawaomba wataalamu wa Wizara ya Kilimo, waumize vichwa watathmini hawa, wafikiri nini cha kufanya ili kuondoa tatizo hili. Pindipo likiondoka tatizo hili la wadudu ndani ya embe hizi basi nakuhakikishia ndani ya Kisiwa chetu hichi cha Pemba au Zanzibar kwa jumla umasikini kwa kiasi fulani utatuondokea. Ni zao kubwa na tunazalisha sana na ni neema kwetu. Lakini itakapozaliwa embe hizi asilimia 80 zinatawaliwa na wadudu, huwezi hata kuitia mdomoni, unaona tabu hata kula embe wakati wa usiku ni balaa.

Mhe. Spika, tatizo la pili lililokumba zao hili ni soko. Hayo machache yanayotokea yakawa bado angalau wale wadudu hamna basi pia hakuna soko la kuuzia embe hizi. Kwa hivyo naiomba Wizara hii kwa kuondosha tatizo hili angalau itafute wawekezaji, ndani ya nchi yetu hii, hasa kisiwa cha Pemba ambao kuwa hili zao muhimu linatoka pale na kwa wingi. Sisi tunanunua soda hapa au juice zile za vichupa za embe, kichupa kiduchu ambacho kuwa hata mtoto mchanga anakimaliza kwa shilingi 800/-. Je, ingelikuwa kuna muwekezaji akawekeza katika viwanda angalau vidogo vidogo, katika hili, tungeneemeka ndani ya nchi yetu, matatizo madogo madogo pia yangetuondokea.

Naomba sana Mhe. Spika, katika hili iishauri serikali, itafute muwekezaji aje hapa ndani ya nchi yetu kwa kuwekeza katika suala hili. Lakini pia wataalamu waumize vichwa sana katika kuondoa tatizo hili la wadudu hawa, sio kuleta mitego ile miwili mitatu, haitusaidii Mhe. Spika.

Mhe. Spika, wenzangu wamezungumza sana katika kilimo cha Maweni. Ni hakika katika kilimo cha Maweni Pemba, Kaskazini kuna Wilaya ya Micheweni wenzetu kila anayesimama hapa anasikitika Wilaya ya Micheweni shida, njaa, dhiki, kila balaa lipo Wilaya ya Mcheweni. Mimi nataka niseme kwamba Wilaya ya Micheweni ina ardhi nzuri tena yenye rutba. Wilaya ya Micheweni kuna kipindi watu walikuwa wana kikundi chao walikuwa wakipanda vitunguu. Mhe. Spika, kitunguu kilichokuwa kikitoka pale ulikuwa huamini kama kinatoka Micheweni. Tatizo lililokuwepo pale ni miundombinu ya maji. Naiomba wizara ifuatilie,ifanye utafiti, ijue katika ardhi ile kitu gani hakipatikani na nini tatizo ili kuwasaidia wenzetu hawa katika Wilaya hii ya Micheweni.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nataka nije katika uchumi wetu wa taifa ambao ni karafuu. Huwezi kuwa na karafuu mpaka uwe na mikarafuu. Wizara ya kilimo imetoa maelezo mengi kuhusu uatikaji na upandaji wa mikarafuu na hata ndani ya kitabu chetu hichi kinaonesha Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dokta Ali Mohammed Shein, akizindua upandaji wa mikarafu Kitaifa katika kijiji cha Mikindani huko Pemba.

Nataka niiombe wizara na nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie katika hali hii ya kupanda mikarafuu katika kila eneo atupe tathmini ni mikarafuu mingapi iliyopandwa, mingapi imeshika na mingapi haikushika ili tujue tatizo ni nini katika upandaji ule ili watu wetu wazidi kupata moyo katika kuendeleza zao letu hili.

Mhe. Spika, sitaki nichukue muda wako mwingi kwa sababu kuna wengi wanaotaka kuchangia ingawa na wengi wameshachangia. Kwa niaba ya wanawake wenzangu wa Wilaya ya Wete naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai kuweza kukutana hapa asubuhi hii. Pia nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii. Tatu nimshukuru Mhe. Waziri wa Kilimo na watendaji wake wote kwa kazi ngumu wanazozifanya, nawashukuru na nawapongeza sana.

Pamoja na changamoto zilizokuwepo lakini pia tunapata tamaa kidogo. Niseme pale Mhe. Waziri katika Idara ya Kilimo alipotwambia wakulima tutapata mbegu za mahindi, mtama, kunde. Mimi nasema napongeza kwa hatua hiyo. Pia nimuongeze Mhe. Waziri tuweze kupatiwa na dawa. Kwa sababu mara nyengine mahindi hushambuliwa sana na wadudu kwa hivyo tukipewa hizo mbegu basi pia tufikiriwe kupewa na dawa ambazo zinaweza zikatusaidia.

Mhe. Spika, mimi niseme kwa kweli Wizara imejipanga kutupatia mbegu hizi tukalima badala ya kuvuna mpunga tukaweza kupata mazao mengine mbadala, basi nasema tunaweza tukawa na chakula kingi cha kutosha, tukaweza kujiwekea hakiba.

Mhe. Spika, niende katika ukurasa wa 26 taasisi hii ya utafiti. Niseme na wao wanajitahidi lakini bado wanahitajika kuongeza bidii yao. Mimi nilisema wangefanya utafiti katika suala zima la uvunaji wa maji ya mvua. Kwa sababu kama tunavyoona mvua zetu zilivyo kwa miaka hii, saa nyengine zinakuwa hazitoshelezi. Tungeweza kufanya majaribio madogo madogo ya kuona uvunaji wa maji ya mvua ili tukaweza kujikwamua pale inapokuwa mvua hazikuwa za kutosha.

Mhe. Spika, niende katika Idara ya Misitu, wenzangu wameeleza hapa lakini na mimi nataka nichukue jukumu la kusema kama Idara hii kwa kweli ina jukumu kubwa la kusimamia upandaji wa miti, lakini pia kusimamia zoezi zima la ukataji wa miti ovyo. Idara hii naiomba iwe makini sana kwa sababu isipozingatia tutabakia na jangwa.

Mhe. Spika, niwaombe watu wa Idara hii pale wanapotoa vibali, basi wawe pia na ufuatiliaji. Kwa sababu unaweza ukatoa kibali mtu pengine anataka kwenda kukata mti pengine, mti huo anaokwenda kuukata upo kwenye chanzo cha maji. Hii inaweza ikatusababishia madhara mengine. Pia kuweka ulazima wa kumwambia yule mtu anayetaka kukata mti basi awe tayari ameshaotesha mti mwengine ambao utaweza kufidia ule alioukata.

Nikitoka katika idara hiyo niende katika Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe. Mhe. Spika, mimi nilipata matumaini mazuri, Wizara hii ilipokuja kutuwasilishia ule Mswada mwaka jana wa kuona kwa kweli tutajipanga katika uzalishaji mwingi wa chakula na baadae tuweze kupata chakula cha ziada. Lakini bado naona suala hili halijatiliwa maanani sana. Mhe. Spika, njaa inapokuja huwa haiagi, unaweza mwaka huu ukavuna mazao mazuri, lakini kama huna mpango

wa kujiwekea hakiba ya chakula mwakani ukalima pengine usifanikiwe na kile ulichonacho hukukihifadhi vizuri ikawa tayari tumekabiliwa na njaa.

Mhe. Spika, mimi nalisema hili kwa ushahidi maalum. Mwaka jana ulipokuja Mswada huu niliwahi kuchangia kwa kuona tunalima sana mahindi. Mahindi haya huwa hatujiwekei utaratibu au wizara yenyewe haichukui juhudi ya kuhamasisha labda wakulima kuona mazao haya wasiyavune mabichi tu kwa ajili ya biashara ya uchomaji wa mahindi. Ila wawashauri sana wananchi mengine mahindi wayakaushe ili weweze kuwa na hakiba kwa kuhofia pale tunapokuja kukosa mazao.

Mhe. Spika, mimi hili nilitaka nikazie sana. Bado tatizo linaonekana kubwa na sio kwamba hatutaki labda mkulima asiweze kuuza mazao yake, lakini pia fikra ya kujiwekea hakiba iwepo. Sidhani kama mtu anaweza akala mahindi ya kuchoma manne matano akasema ameshiba. Lakini naamini akipata nusu kilo ya unga wa sembe anaweza akashiba. Kwa hiyo Mhe. Spika, nataka nimuombe Mhe. Waziri elimu hiyo ni muhimu kuitoa kwa wananchi wake hasa akizingatia anatuhimiza sana juu ya suala la kilimo.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nataka niende katika idara hii ya umwagiliaji maji. Kwa kweli na mimi idara hii naiona bado haijawa makini. Lakini pia niseme labda umakini wake kutokana na fedha za kutosha. Niiombe serikali iweze kuingiza pesa za kutosha ili mradi huu uweze kukamilika. Kwa sababu naamini tukiwa na mashamba haya ya kumwagilia maji, naamini tunaweza tukajikomboa kwa kiasi kikubwa kuweza kupata chakula cha kutosha, shamba lile la umwagiliaji mwaka mmoja mnavuna mara tatu.

Mimi nimewahi kulima katika shamba hizi nilipokuwa nipo Pemba mwaka mmoja mnavuna mara tatu. Suala hili likitiliwa kweli maanani na likapewa kipaumbele na likatengewa fedha za kutosha naamini uagizaji wa chakula japo hauwezi ukakidhi kwa asilimia 100 lakini tunaweza kupunguza.

Kwa hiyo namuomba sana Mhe. Waziri suala hili liweze kushughulikiwa na kupewa kipaumbele. Tunatengeneza ghala lakini kwa sasa hatuna mpunga wa kutosha. Kwa hiyo hizo ghala tunazozitengeneza sijui tutaweka nini. Naamini tukiweza kulishughulikia suala hili la mpunga vya kutosha la umwagiliaji, tunaweza tukapata chakula cha kutosha na kweli tukaweka hakiba. Naomba sana hilo Mheshimiwa aweze kulishughulikia.

Mhe. Spika, niende katika zao hili la biashara ambalo hapa tunasema zao la biashara ni karafuu. Mwenzangu Mhe. Saleh Nassor Juma, jana hapa alisema jamani katika utafiti kweli ufanye utafiti wa kuona kwamba mikarafuu inafanyiwa ya kuwa mifupi ili iweze kuchumika vizuri, na sio kuiacha ikawa mirefu baadae inashindikana hata kuja kuliokoa hilo zao la karafuu.

Pia mimi niseme uchumi ambao nimeuzoea ulikuwa ni huu wa karafuu zao la biashara, lilikuwa ni karafuu lakini pamoja na nazi. Hapo zamani ilikuwa ikitajwa na nazi. Mimi naomba suala hili na hapa Mhe. Waziri katika kitabu chake ametuonesha jinsi alivyoupa umuhimu mkarafuu wa kwamba hata ufanyiwe sensa aijue idadi ya mikarafuu ambayo tayari imeshapandwa. Lakini hakuonekani juhudi ya kuwa iko sensa nayo itahesabu minazi mingapi tumeipanda. Tukizingatia hivi sasa nazi tunanunua kutoka Tanga. Mimi nakuomba sana Mhe. Waziri wataalamu wako

watakapofanya sensa hii ya kwenda kuhesabu miche ya mikarafuu basi pia wasisahau na miche ya minazi. Zao la mnazi linatuondoka kwa kasi, minazi mingi tumeshaikatakata. Sasa ifanyike juhudi ya makusudi pia kupanda mengine mipya.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nimalizie mchango wangu kwa kumuuliza Mhe. Waziri katika bonde la Mtwango kuna visima vimechimbwa ili wakulima waondokane na tatizo la maji katika shughuli zao za kilimo. Lakini hadi leo visima hivi havifanyi kazi, sababu hasa ni nini? Huku si kupoteza fedha za nchi bure, visima hivi vitaanza kufanya kazi lini. Baada ya hayo machache Mheshimiwa kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono hotuba hii kwa asilimia 100, ahsante sana.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Pili nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya na kuweza kusimama hapa, na kuweza kutoa michango yetu mbali mbali kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, mimi moja kwa moja nianze katika kitabu hiki ukurasa wa 4-5 ambao unazungumzia mchango wa upatikanaji wa ukuaji wa sekta ya kilimo. Katika kitabu hiki sana katika masuala ya kilimo kumezungumziwa suala la karafuu, pamoja na suala la mpunga zaidi. Mimi katika kumbukumbu zangu hapo zamani kulikuwa kuna mazao mbali mbali ya viungo kwa mfano kulikuwa kuna tangawizi, ilikuwa inalimwa sana na watu wa Wizara ya Kilimo walikuwa wakiyashughulikia sana mazao haya, kuna manjano, pilipili manga, pili pili hoho na pilipili nyengine ambazo hizi zamani zilikuwa wakulima wetu wanazilima nyingi na zilikuwa zinaingiza kipato kwao wao lakini vile vile na kwa serikali kuu.

Mhe. Spika, ushauri wangu katika hili tutakapokuwa tupo kwenye karafuu tu, haya mazao mengine ya viungo kama tangawizi na manjano ambayo kule Kaskazini Unguja hasa katika jimbo la Mhe. Mtando inalimwa sana manjano. Kulikuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuendelea kufanya utafiti katika mazao haya. Lakini vile vile serikali kuyatafutia soko la uhakika kama ilivyofanya kwa upande wa karafuu.

Mhe. Spika, jengine niangalie katika kitabu hiki hiki ukurasa wa 5-7 hali ya uzalishaji. Katika kipengele hichi Mhe. Waziri katika hotuba yake amezungumzia tathmini ya mazao ya namna gani yanavunwa kwa mwaka. Kwa mfano mwaka 2010 tumeoneshwa kuna tani 3112, ambapo mwaka 2011 kuna tani 3281 ambazo zimevunwa za mahindi. Lakini kwa uzoefu tulionao kwa Zanzibar sijawahi kuona kwamba mahindi ya wakulima yanaletwa sehemu moja yanapimwa au viazi vikuu vinaletwa Marikiti pale vinapimwa na vinajulikana ni tani ngapi. Lakini humu katika tathmini tunaambiwa kuna tani ngapi tani ngapi. Atakapokuja Mhe. Waziri hebu atueleze kwamba tathmini hii inapatikana vipi.

Vile vile tukiendelea mbele katika ukurasa wa 7-10 kumezungumziwa muelekeo wa bajeti ya Wizara ya Kilimo 2010 -2012. Katika maelezo yake Mhe. Waziri katika hotuba hii anazungumza wazi kwamba huduma za kilimo zitaimarishwa kwa mfano matrekta, mbegu, pamoja na mambo mengine mengi tu ambayo kwa ajili ya kuimarisha kilimo cha mpunga. Mhe. Spika, lakini mwaka huu tunaoumaliza hivi sasa tumeshuhudia katika maeneo mengi sana mbegu za mpunga ambazo zilizokuwa zikitolewa na serikali kwanza hazikuwafika wananchi wenyewe. Zilikuwa

zinauzwa kiholelaholela kwa watu wengine mbali. Hizo zilizofika zimefika wakati ambao wameshachelewa, watu wamebakia kutwanga na kupika wali. Kwa hiyo jambo hili limepelekea kwa kiasi kikubwa sana kukosekana kwa ongezeko la uzalishaji wa zao la mpunga katika maeneo mengi. Lakini pia suala la dawa na mbolea nalo pia halikufika kwa wakati.

Mhe. Spika, pia matrekta yalipelekea watu kuchelewa kulima kilimo cha mpunga kutokana na kwamba serikali iliweka utaratibu wa kulima ekari maalum kwa pamoja. Tukiangalia hili kwamba kuna baadhi ya wakulima wao wenyewe waliweza kuchangia hiyo huduma iliyotakiwa wengine walichelewa. Wale ambao walitoa pesa zao mwanzo pia na wao walichelewa kupata hiyo huduma. Jambo ambalo lilipelekea wao wenyewe moja kwa moja kuchelewa kuanza kilimo. Bahati mbaya tulifikia hatua ambayo mazao kwa mwaka huu ni madogo sana.

Mhe. Spika, humu katika kitabu nimeona kwamba wizara inasema kwamba itajitahidi kwa hili. Lakini hili sio la kusemwa tu hili linatakiwa lisimamiwe ikiwa kweli tuna nia ya kufanya Mapinduzi ya Kilimo. Kwa hivyo kila kitu lazima tuhakikishe tunakwenda kama kinavyopangwa au kinavyozungumzwa.
Mhe. Spika, tukiendelea katika kitabu hiki ukurasa wa 8 hapa tulizungumza suala la ujenzi wa maghala ambapo anatafutwa mshauri muelekezi kwa ajili ya ujenzi wa maghala ya chakula. Lakini mbona mimi nakumbuka haya maghala katika nchi hii tunayo, sasa tunataka kujenga maghala mapya au pengine kuyafanyia marekebisho yale ambayo yapo. Mimi nakumbuka maghala ya hakiba yapo. Mhe. Spika, labda aje atueleze hapa pengine kama maghala yale pengine hayafai au kama pengine yameuzwa au yana matatizo gani na ndipo tukataka kuanzisha maghala mengine.

Mhe. Spika, vile vile niende katika Chuo cha Kilimo cha Kizimbani. Pamoja na malengo mengine Chuo hiki kwa mwaka 2012/2013, kimejipangia kuchukua wanafunzi 130 wa Cheti na wanafunzi 20 wa kiwango cha diploma. Mhe. Spika, hivi sasa tunaelekea katika Mapinduzi ya Kilimo, leo Chuo cha Kilimo cha Kizimbani ambacho ndio kinatoa hao wataalamu wa kilimo kinachukua idadi ya wanafunzi 130 wa cheti na wanafunzi 20 wa Diploma, hapa kweli ndio tuna nia thabiti hasa ya kuweza kufanya haya mapinduzi ya kilimo, wanafunzi hawa ni kidogo.

Mimi nadhani hivi sasa umefika wakati wanafunzi wote ambao wanamaliza skuli wawe na taaluma inayohusiana na masuala ya kilimo, wawe wanajua kuhusu kilimo. Labda Mhe. Spika, mimi ningelishauri Wizara ya Kilimo ingelikaa na Wizara ya Elimu au pamoja na serikali kwa ujumla, haya masuala ya kilimo yangeliingizwa katika mtaala wa elimu, kwa hapo ingelisaidia sana katika kuhakikisha kwamba watu wengi wanajua namna gani ya kulima kilimo kilicho bora hata kama hatoajiriwa katika serikali lakini ataweza kujiajiri mwenyewe katika masuala haya ya kilimo.

Mhe. Spika, mimi namuomba Waziri kwamba idadi hii ya wanafunzi kwa mwaka tunayochukua katika Chuo cha Kilimo cha Kizimbani ni kidogo mno, tuongeze idadi angalau ili tuoneshe ile dhamira yetu ya kufika katika Mapinduzi ya Kilimo.

Mhe. Spika, katika Chuo hichi cha kilimo mwaka jana waliomba milioni 500, Chuo hiki na walipewa milioni 495 yaani hawakutoshelezewa zile pesa ambazo walizitaka mpaka tunaingia katika bajeti hii kuna milioni 495 ndio zilizopatikana.

Mwaka huu pia Chuo hiki kimeombewa milioni 500 hizi ni pesa kidogo sana kwa kuendesha Chuo cha Kilimo cha Kizimbani. Chuo hiki ndio tunachokitegemea tupate hao wataalamu, tupate mambo mbali mbali kwenye Chuo hiki, leo kinakwenda kuombewa milioni 500 zitasaidia kitu gani hizi. Mimi naomba hii milioni 500 kwa Chuo cha Kizimbani ni kidogo sana angalau wangelipata milioni 700 wangeliomba. Mhe. Waziri labda hapa uje utueleze kwa nini pengine mkaomba kiasi kidogo kama hiki cha fedha.

Mhe. Spika, vile vile katika Wizara kwa ujumla kuna wafanyakazi 36 ambao tunaambiwa kwamba wamechukua likizo bila ya malipo. Hili ni tatizo kubwa, kuna siku Wizara ya Kilimo kutakuja kuwa hakuna mfanyakazi hata mmoja, wote wamechukua likizo bila ya malipo. Tukija kujiuliza tatizo kitu gani hakuna asiyejua haya yanatokana na masuala ya maslahi duni, hawa watu ni muhimu sana kwa hivyo ni lazima tuwatizame mishahara yao.

Chuo hiki wafanyakazi wake au Wizara hii kwa ujumla wafanyakazi wake mishahara yao midogo, na hawa watu ni wataalamu mno, wazuri na wanafanya kazi kwa bidii kubwa. Hapa Mheshimiwa ungeliwaangalia kwa jicho la huruma zaidi hao. Zaidi hawa wanaangaliwa katika maposho tu. Maposho hayatawasaidia huko baadaye, wangeliangaliwa hasa katika masuala ya mishahara.

Mhe. Spika, vile vile katika Idara ya Mipango, kifungu 0401 Ununuzi wa zawadi. Mwaka uliopita kifungu hiki kiliombewa shilingi laki 6, lakini mpaka mwaka huu kimeombewa shilingi milioni 7. Naona hii ni idadi kubwa sana ya fedha, Mhe. Waziri atakapokuja atupe majibu mazuri ya hapa, atueleze na atupe ufafanuzi wa kutosha hasa ili turidhike. Kwa sababu kutoka laki 6 mpaka milioni 7 ni pesa nyingi sana hizi. Kwanza zawadi hizi ni zawadi gani, sijui kama ni Eid el Fitri au zawadi wa Pasaka hizi, kwa hivyo aje atwambie zawadi zipi na hizi na atwambie tunafanya kitu gani.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niangalie Idara ya Uhakika wa Chakula na Lishe kifungu kidogo 220408. Katika kifungu hiki mwaka jana kiliombewa shilingi laki tano, lakini mwaka huu kinaombewa shilingi milioni sita na hapa pana gepu kubwa sana kutoka mwaka jana hadi mwaka huu na hizi ni gharama za umeme, sasa sijui *TANESCO* wameongeza tena bili hapa au *ZECO* au wameongeza wenyewe bili kubwa zaidi ya hii au kuna kitu gani ambacho kimefanywa ambacho kimepelekea kuongeza gharama hii.

Mhe. Spika, baada ya hayo ninakushukuru.

Mhe. Omar Ali Shehe: Ahsante Mhe. Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuendelea kutupa uhai wake na hatimae tukaweza kuja hapa leo na tukatekeleza majukumu yetu ya kazi.

Mhe. Spika, Wizara hii tunayoijadili hii leo ni wizara iliyopewa jukumu la kusimamia maendeleo ya kilimo katika nchi yetu. Na hapana shaka kwamba umuhimu wa kilimo kila mmojawetu anaufaham kwamba kama tutakiimarisha kilimo huenda tukaimarisha uchumi ya nchi yetu kwa maana ya kuongeza pato la taifa. Tutakapoimarisha kilimo Mhe. Spika, hata

huenda tukaepikana na tatizo lile linalowakabili wananchi wetu wa mfumko wa bei unaotokana na uagiziaji wa bidhaa hasa za chakula kutoka nje ya nchi.

Lakini Mhe. Spika, iwapo tutaendelea kilimo basi lile suala linalotukabili katika nchi suala la ajira kwa vijana wetu basi kwa kiasi kikubwa tutakuwa tumelipatia ufumbuzi wake. Na katika kuelekea huko kuimarisha kilimo katika kuelekea katika nyanja hizo kuongeza uchumi wa nchi, kupunguza mfumo wa bei na ajira ndio serikali ikaja na ile dhana ya mapinduzi ya kilimo ni dhana nzuri ambayo kama kweli tutaweza kuitekeleza kwa vitendo basi mapinduzi ya kilimo katika nchi yetu inawezekana na hivyo kufikia katika lengo ambalo tumelikusudia.

Mhe. Spika, dhana ya mapinduzi ya kilimo maana yake ninakusudia katika suala zima la uzalishaji zaidi kwa mazao ya chakula na mazao ya biashara na ili tufike pahala tuzalishe zaidi maana yake tunategemea teknologia ambayo uzalishaji wa siku hizi unategemea ardhi ndogo lakini yenye uzalishaji mkubwa na uzalishaji huo basi uwe na mazao yenye ubora. Kwa hivyo hiyo ndio zana halisi ya mapinduzi ya kilimo, tufike pahala tuzalishe zaidi mazao ya chakula, mazao ya biashara na tutumie ardhi ndogo lakini kwa kweli yenye uzalishaji mkubwa.

Sasa Mhe. Spika, ili fufikie katika hatua hiyo, ni lazima serikali kupitia bajeti yake ielekeze sehemu kubwa majeti yake katika suala zima la kufanya utafiti katika mbegu bora. Hatuwezi tukawa na mapinduzi ya kilimo kama ikiwa hatuna suala zima linalohusiana na utafiti wa mbegu bora. Lakini vile vile ili tufikie katika hatua hiyo lazima tuwe na matumizi sahihi ya mbolea. Maana si suala la kutumia mbolea tu unaweza kutumia mbolea badala ya kuleta tija ikaleta balaa zaidi. Tuwe na matumizi sahihi ya mbolea, lakini chengine kwa kweli tunatakiwa ielekeze bajeti yake katika suala zima la udhibiti wa magonjwa yanayopelekea kuathirika kwa mimea pamoja na matunda.

Sasa hiyo kwa ujumla Mhe. Spika, ndio inayotekeleza dhana ya kilimo, tutakapofika pahala hapo, bajeti yetu ikalenga katika maeneo hayo ile dhana ya kilimo kwa kweli ndipo itakapoaguka. Na yote kwa yote basi suala la msingi katika hali hiyo ni suala zima la kutoa huduma kwa wakulima pamoja na elimu kwa wakulima. Tutakapofika pahala wakulima wetu wakapata huduma zilizo bora wakulima wakapata elimu iliyokuwa nzuri kwa kweli ile dhana ya kilimo tukafika pahala tukaitekeleza.

Sasa basi leo tunajadili bajeti ya wizara hii, mpango wa serikali katika suala zima la kuiwezesha wizara hii kutekeleza majukumu yake. Waziri amekuja kutuomba tumuidhinishie shilingi bilioni kumi na mbili pamoja na bilioni mbili kwenye maendeleo. Kwa ujumla serikali inaomba bilioni kumi na nne ukiacha mbali, hapa sitozungumzia fedha za wafadhili kwa sababu siwezi kuzungumzia fedha za wafadhili, wafadhili wana mashaka yao wana hiari yao. Kwa hivyo sisi tutajadili kile ambacho kinatokana na sisi, kwa hivyo kwa ujumla serikali itataka kuidhinishiwa bilioni kumi na nne, kumi na mbili zikiwa za matumizi ya kawaida na bilioni mbili hizo zitaelekea kwenye maendeleo.

Mimi Mhe. Spika, kwanza nisikitike hapa kwamba bilioni kumi na mbili zinakwenda kwenye matumizi ya kawaida, ni bilioni mbili tu zitokanazo na serikali ndio zitakazokwenda kwenye kilimo. Sasa namna hiyo tutaona ni kiasi gani tunafanya mzaha katika mambo. Tunachukua bilioni mbili kwenda kuzifanyia mageuzi ya kilimo lakini bilioni kumi na mbili zinakwenda

katika matumizi ya kawaida, sasa hiyo ni namna gani bado hatujawa na umakini wa kufanya mageuzi ya kilimo hatujawa na umakini hata siku moja.

Mathalan nimefanya utafiti mdogo sana ofisi kuu Pemba wao wametengewa 1,844,000,000/= na hapa nataka nitoe malalamiko yangu kwamba jana tuliangalia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tumeona katika mijengeko ya kibajeti katika wizara hii utaona kila Idara ina bajeti yake Pemba lakini hili hatukuliona katika bajeti ya kilimo. Sijui kwa nini ikawa hivyo kwamba wao fedha zinazopelekwa kule ni za jumla jumla tu, lakini zile Iidara moja moja fedha zao zote zitatoka Unguja hilo ni pungufu hiyo ni kasoro kubwa. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri kwa nini hakufanya hivyo na hilo litapelekea zaidi Pemba kukosa huduma muhimu kwa sababu wao wakitaka chochote katika suala zima la maendeleo lazima waagizie Unguja. Kwa nini wizara nyengine zikaweza wizara hii isiweze.

Kwa hivyo katika 1,844,000,000/= hizi zinakwenda Mhe. Spika, katika shughuli zinazohusiana na uendeshaji wa Ofisi. Idara ya Umwagiliaji ni milioni mia sita na ishirini lakini katika hiyo tutaona kwamba yote katika hayo fedha hizo zinakwenda katika running cost za wizara. Katika Idara hii ya Umwagiliaji pengine tunaweza tukasema vitu ambavyo vinaweza kumgusa mkulima, maana yake Mhe. Spika, tulifahamishwa kwamba bajeti bora ni ile ambayo inamgusa mwananchi na tukizungumzia masuala ya kilimo tunamgusia mkulima.

Kwa hivyo angalau unaweza ukasema kwamba mafuta na vilainishaji pengine ukiachia mbali magari haya ya wakubwa lakini milioni kumi imetengwa na matengenezo na zana pengine hizo zende kwenye matrekta pengine sina uhakika ni milioni saba. Kwenye milioni sita na ishirini hizo zinakwenda kwenye sijui ununuzi wa makapet, sijui kwenye mambo ya vitafunwa viburudishaji na nini na ununuzi wa mapazia.

Idara ya Uendeshaji na Utumishi ni milioni mia tisa na thalathini na nane hapa moja kwa moja mambo ya utawala. Idara ya Uhakika na Chakula ile ni kama Idara tu lakini hapa hatugusii suala zima linalohusiana na ule uhakika kwa sababu Idara hii kazi yake ni kama kuratibu tu kama kuna sera kama kuna nini, lakini uhakika na chakula unatoka kwenye production ambao hawa sio wanafanya production hawa. Idara ya Kilimo pale ndipo tunapodhani pale ndio patakuwa na uzalishaji kwa sababu hapa kwenye mahusiano moja kwa moja kwenye wakulima. Wao angalau hapa wao wametengewa elfu tano mia moja na hamsini na tatu milioni, mimi sishangai na hawa kila wakipewa pesa nyingi, kwa sababu hawa ndio wanaokwenda kwa wakulima moja kwa moja.

Huduma za kilimo zimepanda hazina tatizo zikiwa pamoja na mbolea na mambo mengine, matengenezo ya zana hatuna matatizo nayo ambayo shilingi milioni mia mbili hamsini. Mafuta na vilainishaji vimepanda sana mpaka kwenye mia tatu na kumi na sita hatuna matatizo kwa sababu hawa ndio tunaotegemea watutengenezee matrekta yetu, hawa ndio tunaotegemea watufanyie kila kitu. Kwa hivyo hili mimi sina tatizo nalo.

Idara ya Misitu na Maliasili ni shilingi elfu moja mia mbili sabiini na tisa milioni, Idara ya Mipango na Sera mia saba arubaini na nane milioni. Taasisi za utafiti wa kilimo mia saba na sita. Kwa hivyo Mhe. Spika, ninachotaka kukieleza hapa kwamba kati ya milioni kumi na nne, milioni kumi na mbili zinakwenda katika masuala mazima yanayohusiana na utawala. Kitu ambacho kwamba moja kwa moja kinaleta hofu kwamba ile dhana ya kuwa na mapinduzi ya

kilimo itakuwa ni ndoto katika nchi yetu kwa sababu hata bajeti allocation nayo vile vile hairuhusu kwamba tuwe na mapinduzi real ya kilimo.

Mhe. Spika, katika bajeti ya maendeleo kuna program kumi na moja ilipanga sasa utaona program moja kwa moja zilizopo ambazo kutoka kwenye serikali zilizopangwa ni bilioni mbili, ni dhahiri tutaona katika Baraza hili kwamba hakuna kitakachokuwa. Programu kumi na moja na siku zote tunapiga kelele katika Baraza hili kwa nini hatuweki vipaumbele vichache, kwa sababu kutegemea wafadhili katika bajeti hii wafadhili nao wana matatizo yao, wana hiari yao kutoa na kuto kutoa wala hawalazimiki wanavyotaka wenyewe tu. Lakini tungelichukuwa program kwa mujibu wa uwezo wetu tulionao wa bilioni mbili ambazo hizo zitatoka ndani ya mfuko wa serikali. Lakini leo imepangwa kutekeleza hizi programu kumi na moja kitu ambacho moja kwa moja utaona kwamba hazitekelezeki.

Kwa hivyo Mhe. Spika, na kinachoonekana maana yake katika Wizara kongwe kati ya Wizara kongwe ni Wizara ya Kilimo. Lakini kadiri unavyosoma kitabu hiii cha bajeti inaonekana kana kwamba suala la kilimo ndio kwanza tunalianzisha leo katika nchi hii. Kadiri utavyosoma utaona kana kwamba ndio tunaanza leo. Ukisoma ile bajeti ya mwaka jana kuna kitu kinachoitwa training tunakwenda kwenye mafunzo ndio kwanza tunawasomesha watu wetu. Maana yake hatujaingia katika hatua yoyote ile kwanza tuwachukuwe watu wetu tuwapeleke Bara huko kwenye kusoma, tunawachukuwa watu wetu tuwaweke kwenye vikundi vya ushirika kuwasomesha.

Hizi bajeti za miaka ya nyuma zilikuwa zikifanya kazi gani. Maana yake leo tulikuwa hatudhanii tena masuala ya kuwasomesha watu hapa kazungumza pale Mhe. Farida kulikuwa hapa kuna vyuo vya kilimo, Fiedel Castro ilikuwa ni Skuli ya Michepuo iliyokuwa iki-deal na mambo ya kilimo tu, Lumumba Uvuvi na vitu vyengine. Sasa leo yote inaonekana kwamba hakukuwa na sustainability ya kuendeleza kitu hichi, leo ndio tunaanza upya kuwasomesha watu wetu Bara na sehemu nyengine.

Kwa hivyo Mhe. Spika, bado narudia kwamba tuna kazi kubwa sana ya kufanya na Serikali katika hili kwa kweli lazima ijipange upya kwa sababu kilimo katika nchi yetu kina umuhimu mkubwa. Kwa sababu tutapoimarisha kilimo kama nilivyotangulia kueleza kwamba hali ya pato la taifa itaimarika. Lakini vile vile kwa sababu sehemu kubwa ya wananchi wetu ni wakulima tutaondosha yale mambo ya kuagizia kwa sehemu kubwa sana tutapunguza na hivyo mfumko wa bei utatoweka, lakini ajira kwa wananchi wetu itapatikana.

Leo tuna programu hii ya umwagiliaji utakapokwenda katika maduka yote utaukuta mchele kutoka Mbeya, utaukuta mchele kutoka Mwanza sijui kutoka Shinyanga lakini leo tuambiwe duka moja tu utakaokwenda ukakuta mchele kutoka Bumbwisudi konzi moja tu. Ukulima wao Mhe. Spika, sehemu zote sisi tushakwenda ukulima wao hautofautiani na ukulima wetu. Leo hapa mtu atalima mwaka mzima lakini anachoambuliwa magunia sita magunia yenyewe ni mapepe matupu hamna kitu, njaa juu ya njaa. Tufike pahala angalau tuseme ukifika Darajani pale kuna maduka mawili alau utaukuta mchele wa Bumbwisudi upo pale. Ukenda Chake Chake utakuta mchele ule unaotoka kwenye irrigation ya Makombeni ndio at least tunataka tufikie hapo. Lakini leo tunafika pahala hiyo nerika yenyewe tulioambiwa ukiitupa popote hata humu

ndani ya Baraza ukiitupa nerika inaota. Leo Mhe. Ali Salum anatwambia nerika inakuwa ni tatizo, nerika inakuwa nerika hakuna chochote.

Kwa hivyo Mhe. Spika, nasema kwamba tufike pahala serikali ikae kitako na ilizingatie sana suala la kilimo. Na mimi nataka niwaombe wajumbe wenzangu kupitia kamati hebu tujaribu kuisaidia sana Wizara maana yake bado mimi siamini hata hizi fedha Mhe. Spika, hizi ambazo ni za programu ya maendeleo utapokwenda kuzifanyia ukaguzi, basi sehemu kubwa utakuta ni mambo ya semina, mambo ya safari. Na kama alivyosema Mheshimiwa kwamba hizo kesi na vilio vilioko basi utaambiwa ni Mkurugeni tu ndie anaekwenda hawa wapiga debe wote wafanyakazi wa kawaida kama ilivyotolewa kwenye umwagiliaji hakuna chochote, hata watendaji wa kawaida hawapelekwi kwenye mafunzo. Kwa hivyo Mhe. Spika, tutaendelea kubakia katika hali hii kila miaka na hakuna maendeleo yoyote tutayofikia katika kilimo.

Mimi natoa wito kwa serikali katika hili kwanza serikali ninaiomba sana ikiwezekana tuangalie hata huu mfumo wetu wa bajeti maana yake inavyoonekana tunarithi tu mambo kwa sababu kuna vifungu Mhe. Spika, havitumiki na havina maslahi yoyote katika Wizara. Lazima viondoshwe vifungu hivyo fedha zile tuzipeleke katika sehemu nyengine. Kwa hivyo ninaiomba serikali ikae ifikirie namna bora ya uandaaji wa bajeti.

Lakini jengine Mhe. Spika, kuna suala zima linalohusiana na mabadiliko ya hali ya hewa, sasa hivi wakulima wetu wanapata tabu sana kwa sababu ile miongo ya kawaida tuliyoizoea kwamba ikifika mwezi fulani mpaka mwezi fulani ni Kiangazi, ikifika miezi fulani ni Masika, hakuna tena kitu kama hicho. Kwa hivyo ninaiomba Wizara iwe karibu sana na kuratibu mambo haya na kuwaeleza wananchi kwa sababu wananchi wetu wanapata matatizo kwa kutojua tu miongo inavyokwenda kwa sababu sasa hivi hali ya hewa imebadilika.

Lakini la mwisho Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kutoa ushauri, ninaiomba Wizara tutulie mkazo sana juu ya mazao ya matunda pamoja na mazao ya viungo.

Baada ya hapo Mhe. Spika, ninakushukuru. Ahsante sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri. Lakini kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na pia nimpongeze Katibu wake pamoja na watendaji wake kumsaidia kufanya kazi zake vizuri ili kufanikisha kazi zake.

Mhe. Spika, mimi naanza kwa kupewa pole wakulima kama alivyosema Mhe. Waziri anawapa pole wakulima kutokana na uharibifu wa mazao. Lakini niseme Mhe. Spika, kuwapa pole wakulima si suluhu isipokuwa Mhe. Waziri awatafutie neno la kuwapa zaidi yaani kuwaridhisha wakulima wale ili wajue kwamba sisi tumepewa pole lakini hatukupata tiba, lakini waziri kaweza kuwaridhisha wakulima wale kwa kuweza kujua nini waziri katufanyia.

Mhe. Spika, lakini niiombe wizara ichukuwe juhudi kubwa sana ili wakulima kuwapa motisha na sio kuwapa pole tu, lengo hasa la wakulima hawa ni kulima na kupata tija ya mazao yao.

Mhe. Spika, pia nije kwenye elimu. Elimu kwa wakulima pia ni ndogo hawapati elimu kama ilivyo, wakulima wanahitaji kupata elimu ili waweze kujua vipi tunalima na vipi tunafanya. Lakini Mhe. Spika, pia mabadiliko ya hali ya hewa na miongo hivi sasa watabiri imekuwa ni kidogo, Mhe. Spika, utabiri umekuwa ni kidogo ndio maana wakulima wanashindwa kujipanga kwa kutokuelewa hizi kama ni mvua za vuli au mvua za masika ili waweze kupanda vilimo vyao. Ninamuomba Mhe. Waziri hili aliangalie sana kuhusu utabiri watabiri wetu sasa hivi wamekuwa ni kidogo wananchi wamekuwa hawaelewi vipi wakati huu tulime wa mvua za masika au wakati huu ni mvua za vuli. Mhe. Spika, ni lazima wananchi kujua mabadiliko ya tabia ya nchi na wananchi wanahitaji waelimishwe zaidi kujua mabadiliko haya ya tabia ya nchi.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Misitu, Mhe. Spika, ukataji wa miti ovyo kama alivyosema wenzangu ni tatizo kubwa sana hili la ukataji ovyo la misitu, sababu kubwa inayosababisha mvua kutoweka kwa ukataji wa miti ovyo. Kwa hivyo Mhe. Spika, ninaiomba Idara hii ipange mikakati kuwaelimisha wananchi kupunguza ukataji wa miti ovyo na pia kuwaelimisha kupanda miti katika sehemu zao wananchi wanazokaa.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya Kilimo, Idara hii ya kilimo tuseme kwamba kilimo ni uti wa mgongo Mhe. Spika, na kilimo ni tegemeo la wazanzibari wote. Lakini Mhe. Spika, wananchi au wakulima wetu wamechoka kulima kwa mikono na kutumia kifua. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri awaonee huruma wakulima wetu kwa kuwapatia matrekta ili walime kwa kuweza kuburuga na waweze kuendeleza kilimo chao.

Pia Mhe. Spika, nije katika mbegu za asili. Mhe. Spika, kwa kweli mbegu za asili sasa hivi zimetoweka na tunapatiwa mbegu ya miezi mitatu ambayo mbegu ya asili huwa ina tija zaidi kulikoni hata hii mbegu ya hivi sasa. Kwa sababu mbegu hii unatumia miezi mitatu na ukiangalia tija ni kidogo. Kwa mfano mbegu ya ringa, kinazini, mvivu kwa nongwa, kibawa, kaniki mbegu hizi zote Mhe. Spika, hivi sasa zinaanza kupotea. Ninamuomba Mhe. Waziri apange mikakati ili mbegu hizi zisimalizike kwa ghafla.

Lakini vile vile kukomaa kwa ardhi, kukomaa kwa ardhi kunatokana na ukulima wa papo kwa papo ambayo ardhi ile siku zote inalimwa hapo hapo na ukiangalia mazao yanashindwa kunawirika. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri kutafuta wataalam zaidi kufanya utafiti wa ardhi ili wananchi wetu waweze kulima kwa ufanisi.

Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo iwapo serikali haikujipanga vizuri kuwaelimisha wakulima wetu kilimo cha mpunga kutokana na wananchi kujishughulisha na kilimo cha mwani, Mhe. Spika, kilimo hiki kitaanza kutoweka. Kwa sababu hivi sasa wananchi wengi wanajishughulisha na kilimo cha mwani kulikoni hasa kilimo cha mpunga. Kwa sababu wanaona kila wanapolima kilimo cha mpunga hakiwaletei tija wanaona bora wajishughulishe zaidi na kilimo cha mwani.

Mhe. Spika, nikija katika Chuo cha Kilimo Kizimbani. Chuo kinategemewa kujengwa bweni la wanafunzi, pamoja na kujengwa bweni la wanafunzi Mhe. Spika, Mhe. Waziri aangalie hasa suala la malazi kwa wanafunzi wetu sasa, hususan kwa wanafunzi wa cheti ambao sasa hivi wanarundikana katika chumba kimoja wanaolala watu kumi, sasa hivi wanalala watu 15. Ninamuomba Mhe. Waziri aliangalie sana suala hili pia Mhe. Spika, Chuo kinategemea

kuanzisha Diploma kwa wanafunzi wa kitado cha sita, lakini wapo wanaomaliza cheti je Mhe. Waziri watasaidiwa vipi ili kujiunga na Diploma.

Vile vile Mhe. Spika, ninamuomba Mhe. Waziri atakapoanzisha Diploma na labo iwepo ili wanafunzi wetu waweze kujifunza kwa vitendo. Mhe. Spika, ninakushukuru. Ahsante.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kupata fursa asubuhi hii ya leo kuweza kuchangia na mimi machache katika Wizara hii ya Kilimo na Maliasili. Mhe. Spika, mimi napenda nianze ukurasa wa tano unaohusiana na hali ya uzalishaji. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametueleza katika kitabu chake kwamba katika mazao kama majimbi na viazi vikuu kulikuwa kumepatikana tani 6443 mwaka 2010 na mwaka 2011 tani 4940 hii inaonekana kwamba kuna upungufu wa uzalishaji.

Sasa mimi nataka Mhe. Waziri aje atuelezee hapa upungufu huu hasa unatokana na nini, unatokana na maeneo ya kilimo kutumika vyenginevyo badala ya kilimo ama kuna nini hasa kinachopelekea mpaka uzalishaji umekuwa unapungua kwa kiasi hicho.

Pia Mhe. Spika, nielezee suala la upungufu wa mvua. Sisi tunaamini kwamba mvua hasa iatokana na kuwepo kwa miti na misitu na kama wizara hii ni msimamizi mkuu wa rasilimali hii ya miti na misitu na inaonekana kwamba wananchi wengi wamekuwa miti hii wanaivuna na kiholela, sasa juhudi gani za wizara mpaka ambazo mpaka sasa hivi imeweza kuchukua au mikakati yao hasa ni nini juu ya udhibiti wa ukataji ovyo wa miti ili hii mvua isiwe sasa inazidi kupungua na kukosa mazao.

Pia Mhe. Spika, mimi nizungumzie suala la minazi, minazi hapa haikuoneshwa kwamba kama ilivyo mazao kama karafuu na mengineyo kama ni zao la biashara. Na tunaamini kwamba minazi ilikuwa ikichangia sana katika zao la biashara lakini minazi hatukuipa kipa umbele. Sasa je thamani ya hii nazi imepungua, haja ya kuwa hii minazi haipo, kwa hivyo Mhe. Waziri atakapokuja hapa mimi nimuombe atuelezee kidogo kwa sababu sioni mikakati yoyote inayooneshwa huku kwamba kuna mikakati ya kuimarisha zao hili la minazi.

Na mwisho Mhe. Spika, nataka nizungumzie matrekta ya jamii. Mimi katika jimbo langu la Bumbwini kuna matrekta ya jamii na hata katika jimbo la Donge vile vile yapo. Matrekta haya walipewa wananchi, wananchi hawa wamefanya shughuli zao za kilimo lakini mwaka huu wakati wa kilimo cha mpunga kwa kuwa matrekta yalitakiwa yajumuishwe pamoja na ya serikali hadi hivi sasa matrekta haya hayajarudishwa kwa jamii. Sasa mimi Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje anambie sababu gani hasa matrekta haya kutokurejeshwa kwa wananchi ama serikali imeshayachukua wenyewe ndio imeshayadhibiti tena. Na pia matrekta haya tangu yamechukuliwa hakuna hata senti moja ambayo wananchi wale wamerejeshewa kwa kufanyiwa kazi katika kipindi cha kilimo kilichopita.

Sasa Mhe. Waziri uje uniambie hapa pesa za wananchi hawa za matrekta zimeingia katika mfuko upi? Na matrekta haya bado wananchi wanayaona baadhi ya maeneo yanakwenda kulima, sasa hivi wanaanza kulima kunde lakini wenyewe hawajarejeshewa kilio kikubwa kiliopo hapa. Suala kubwa matrekta haya lini yatarudi na fedha ambazo yalifanya kazi lini wananchi hao watapatiwa.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, naunga mkono hoja mia juu ya mia.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe tulijipangia kwamba tumalize michango kwa leo kati ya saa sita hadi saa sita na nusu ili tumpishe baada ya hapo Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kuweza kuwasilisha hoja yake ya makadirio. Kwa hivyo kuna baadhi ya waheshimiwa wajumbe watakosa nafasi ambao ni Mhe. Subeit Khamis Faki na Mhe. Mussa Ali Hassan. Ninajua itakuwa imewaumiza lakini watafanya utaratibu ili kuweza pengine kutoa michango yao kwa maandishi.

Kwa hivyo tumebakiwa na nafasi mbili ambayo nafasi moja inachukuliwa na Mhe. Abdalla Mohammed Ali na baadae Mhe. Hamad Masoud.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi asubuhi hii kunipatia fursa kusema machache kuhusu hotuba iliyopo mbele yetu, ninakushukuru kwamba na wewe siku hizi umekuwa mtaalam kidogo kwamba juzi ulitupangia mambo ya vitoweo lakini leo na kesho unatupangia mambo ya chakula na ndio utaratibu ilivyo siku hizi tunanua kiteweo mwanzo baadae ndio unatizama kitoweo ulichonacho ukale wali au nikale muhogo maendeleo kidogo.

Mhe. Spika, mimi ningeanza kama walivyoanza wenzangu kuangalia baadhi ya vifungu na mimi vimenikera kidogo kwani vifungu hivi vimenenepa zaidi sijui asilimia elfu au asilimia ngapi, hasa tukenda kwenye uhakika wa chakula na lishe fungu la umeme kutoka laki tano mpaka milioni sita. Na fungu la ununuzi wa zawadi vile vile kutoka laki sita mpaka milioni saba. Sasa labda Waziri angekuja akatwambia hii imesababishwa na nini zaidi.

Lakini jengine Mhe. Spika, ninachokifaham kwamba serikali mwaka huu ilijitolea na ikapunguza bei za pembejeo, mbolea, matrekta na mengineyo. Sasa sijui wizara au serikali katika zoezi hili imetumia kiasi gani ya fedha na je utaratibu wao katika mwenendo huo zimetosheleza mwaka huu au zilihitajika ziongezwe zaidi.

Nikindoka hapo Mhe. Spika, nakwenda katika kitengo cha matrekta. Hivi sasa serikali inatoa mishahara kutokana na vyeti ukiwa una diploma una kiwango fulani, ukiwa na shahada ya chuo kikuu unakuwa mshahara kiasi fulani. Wenzetu hawa mafundi walioko katika kitengo cha matrekta wengi wamemaliza FTC yaani wamemalizia Mbweni tena miaka iliyopita. Sasa mishahara yao inategemea vile vyeti vyao vya FTC, lakini utaalam walionao ni utaalam mkubwa sana kiasi kwamba matrekta yaliyolala miaka sita, saba nyuma wameweza kuyakarabati na hivi leo ndio yanayotumika katika kusafisha mabonde ya Mtwango na Kilombero.

Sasa mimi ningeomba tu wizara ikaliangalia hili kwamba hawa na wao wawekwe katika grade ya wataalamu kwani utaalamu wao hauwezi kupatikana bure bure au sehemu zote tu yoyote ile. Kwani ni utaalam mkubwa naweza kuwafananishana hao watu labda wenye shahada ya Chuo Kikuu kwa ule utaalam walionao. Sasa waziri angeangalia katika hao watakaoekewa scheme maalum basi na wao wakaangaliwa kwa jicho la huruma.

Lakini katika hilo leo tunakwenda na sayansi na teknolojia, wale waliopo pale mafundi wamesoma miaka sabiini na thamanini na teknolojia inayokuja hivi sasa ni ya kileo kwa hivyo wao utaalam wao hauwaruhusu. Jana tu au juzi tulipewa taarifa kwamba kuna ma-*havester*, ma-

havester hawa nina wasiwasi kwamba wataalam wetu waliopo hawawezi kuyakarabati. Kwa hivyo, ningeliomba hawa wataalamu kidogo tulionao na wengi wamekaribia kustaafu basi wakapatiwa utaalamu wa zana ambazo zinakwenda kimaendeleo tuliyonayo hivi sasa.

Mhe. Spika, sasa kidogo nije katika Kitengo cha Uhakika wa Chakula na Lishe. Nafikiri serikali ilikuwa na nia nzuri sana ya kuona kwamba tuna umuhimu wa kukianzisha chombo hiki, kwani linapotokea baa huwa hatupewi taarifa kwamba siku fulani litatokea na litatokea vipi. Lakini cha kushangaza ni kwamba tunasema tu katika makaratasi kuwa tuna kitengo cha chakula na lishe, na lengo letu ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na chakula cha hakiba, lakini hadi hii leo hatuna hata kilo moja tuliyoiweka tukasema kwamba likitokea janga fulani tunaweza tukajiokoa kwa namna moja au nyengine.

Sasa mimi napenda kusema kwamba, ikiwa lengo lilikuwa ni hilo basi tusisubiri mabanda hayo yakamalizika, baadhi ya mabanda yapo sasa hayo mabanda yaliopo tungeanza kuweka hicho chakula cha hakiba ili litakapotokea janga angalau tukajua tunakimbilia wapi. Lakini tukiendelea kukaa na sheria tu, mwisho wake sijui itakuwa ni nini kwa sababu ukienda huko shamba ukiangalia hayo mabanda yenyewe yamo katika hali isiyoridhisha. Sasa ningeomba kama tulivyotunga sheria basi na utekelezaji wake ukaanza mara moja.

Sambamba na hilo ni kuwa pia tumeanzisha sheria ya Idara ya Utafiti au Utafiti wa Mambo ya Kilimo. Nayo hii naona pia itabakia katika makaratasi, na nikiangalia hii ni moja katika sehemu muhimu sana katika maendeleo ya kilimo. Lakini leo nina wasiwasi kwamba wataalamu hatuna mpaka hivyo vifaa vya kufanyia utafiti pia havipo. Sasa ikiwa tuko makini kweli basi mazao yetu yanaharibika sana, hivi sasa tuna embe ambapo ilikuwa ni zao moja tunalolisafirisha kupeleka nchi za nje, tumeshindwa kusafirisha kutokana na kwamba zinasumbuliwa au zinaharibiwa na wadudu, lakini utafiti hatunao hatujui nini la kufanya. Mimi ningeomba ikiwa tumeanzisha sheria basi na utekelezaji wake ukaanza mara moja ili na matunda yake tukaanza kuyaona haraka sana.

Mhe. Spika, niende kidogo katika Idara ya Kilimo. Idara hii kila nikiangalia naona wizara zaidi inajilenga katika zao la mpunga, zao ambalo nahisi upatikanaji wake unakuwa ni mgumu sana. Kama tulivyopewa taarifa kwamba mwaka uliopita mazao hayakupatikana kama ilivyotarajiwa, na hii inatokana na sababu nyingi ambazo hatuna uwezo nazo. Sasa mimi ningependa kusema tu kwamba, kwa nini twende moja kwa moja katika kuangalia zao moja tu la mpunga, kama ni hivyo basi tuyaangalie na haya mazao mengine ambayo kuimarika kwake ni rahisi. Tuna mazao ya muhogo, viazi, na ndizi chakula ambacho nafikiri wengi tunakipendelea, lakini hivi sasa hakuna utafiti wowote uliofanywa kuhusu muhogo sijui kuna *cassava mailbag* hawana dawa, ukienda kwenye ndizi migomba inakauka hakuna utafiti wowote. Lakini huko ambako tunakupelekea pesa nyingi sana nako hakuna faida inayoonekana.

Sasa mimi nashauri tu, kwamba na mazao haya nayo tungeyapa kipaumbele, huenda labda yakawa mkombozi wa hili zao la mpunga, kufanya hivyo kutasaidia sasa angalau kuwa na uhakika kwamba mpunga haupo lakini tuna mazao mengine yangeweza kufanya na kazi ya mchele.

Lakini juu ya hayo ni kwamba pia tumejiingiza zaidi katika zao la karafuu; zao ambalo nalo ni *seasonal,* kuwepo kwake na kutokuwepo kwake hakuna uhakika ni zao la kubahatika tu mwaka lije mwaka lisije. Kuna mazao mengine madogo madogo ambayo yanahitaji nayo yaonekane ili kuwapatia wananchi ajira na kuwapatia fedha nyingi wananchi. Hivi sasa kuna utafiti unaoonesha kwamba kuna baadhi ya mazao ambayo yana bei zaidi na uzalishaji wake ni rahisi zaidi, lakini wananchi hawajahamasishwa kuhusu mazao hayo, tunalohamasisha ni zao la karafuu ambalo kupatikana kwake hatuna uhakika Mungu apende aseme mikarafuu izae, hakuna mikarafuu haizai. Lakini kuna vilimo tofauti ambavyo vinaweza vikamuongezea mwananchi tija. Sasa haya nafikiri wizara nayo ingejipanga ikaona sasa kuna haja ya mazao haya nayo kuyapa kipaumbele, wananchi wangelipata ajira na wangepata fedha.

Hii manjano kuna habari zinasema kilo moja inaweza kufika hata shilingi 40 elfu, lakini wananchi hata taarifa hizo hawana. Hapo nyuma tulianzisha kilimo cha upandaji wa hiliki lakini pia kilimo hiki Mhe. Waziri kimeachwa nyuma hivi sasa hakiulizwi na wananchi waliona matunda yake. Sasa nahisi wizara kuna haja ya kuhamasisha watu katika upandaji wa vilimo kama hivi ili wakaanza kufaidika moja kwa moja kuliko kutegemea hili zao la karafuu.

Mhe. Spika, nije kidogo katika Kilimo cha Umwagiliaji. Nia ipo kwamba sasa tunataka kuingia katika kilimo cha umwagiliaji maji, lakini imekuwa ni kipindi kirefu sana wananchi hawaoni chochote. Ukienda katika mashamba unaona miundombinu tu, lakini hakuna miundombinu yoyote iliyomalizika. Ukienda shamba moja utaambiwa hapa tushaweka ekari fulani, ukienda shamba jengine tushaweka ekari fulani, lakini hata shamba moja ambalo unaweza ukenda ukaambiwa aa hapa mwaka huu tayari tunaanza kuzalisha na matunda yake tunayaona. Sasa hii inarudisha nyuma. Ningelipenda wizara ikaangalia kwamba *phase* hii tunakwenda pahali fulani matokeo yake wananchi wanakuja kujifunza pale, na ile tija itakayoonekana itamu-*encourage* kila mwananchi kuona alaa kumbe kilimo hiki kina faida. Lakini leo serikali au wizara ime-*inject millions of money* katika miradi tofauti ambapo hata mradi mmoja haujazalisha, sasa hii haiwa-*encourage* wananchi na sisi hatuoni.

Ningependa kuona kwamba, kama wanakwenda katika bonde la Makombeni, basi bonde la Makombeni limalizike waanze ile kazi wananchi waone faida, lakini leo Makombeni ni *two years now* kila ukenda umeme haupo, ukarabati huu haujapatikana, sijui kile bado, kwa hivyo unaweza kukuta *more than hundred millions* zishatumika lakini *production zero,* tunafika mpaka wale wafadhili wanaona aa, kuna haja hivi sasa sijui ya kuingiza pesa hapa, hakuna matokeo yake mradi miaka mitatu haujamalizika wanaamua kwenda zao. Sasa hili nafikiri wizara nalo ingeliangalia, kama tunakwenda katika eneo moja *phase* fulani basi tumalize tujue tunamaliza hapa tunakwenda katika sehemu nyengine.

Lakini jengine Mhe. Spika, ni udhibiti wa dawa. Dawa nyingi za kuulia magugu au ya mashamba zinakuwa katika mikono ya maduka binafsi, sasa sijui haya maduka binafsi yanapitiwa yakaangaliwa haya maduka kwamba yana *expiring date*. Kwa sababu ukipita katika mashamba unakuta mpunga umepauka matokeo yake kumbe dawa aliyochukua kutia katika shamba lile imeshapitiwa na wakati. Sasa mimi ningeomba wizara haya maduka ikayaangalia ikapita katika maduka ikaona zile dawa, sio wananchi kwenda kujinunulia tu ikawaruhusu moja kwa moja matokeo yake tija haipatikani.

Lakini la mwisho Mhe. Spika, ningependa niulize sijui kuna sheria yoyote inayohusu kupea kwa mazao. Hivi sasa ukienda sokoni unakuta mazao mengi hayajapea lakini unayaona yako sokoni, matokeo yake mazao yale hayamsaidii chochote mwananchi, unakwenda sokoni huridhiki wewe kulinunua kwa sababu halijapea, matokeo yake yanaharibika ovyo. Sasa sijui niulize je, kuna sheria yoyote inayoelekeza kwamba zao mpaka lifikie kiwango fulani ndio linatakiwa kuletwa sokoni au kutumika au laa, kama si hivyo basi kungekuwa na sheria ndogo ndogo. Unakuta nazi huko unamuuliza hii nazi au dafu? Hujui kakusudia kukuuzia nini. Sasa haya ni uharibifu na sisi tunaambiwa tusifanye isirafu.

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Kilimo na Maliasili. Mhe. Spika, kwa kuheshimu muda wako na ili twende na wakati kama ulivyopanga, basi mimi nina machache tu katika mchango wangu.

Mhe. Spika, kilimo ni maji na ndio maana kuna mradi maalum wa umwagiliaji maji lakini huo ni programu ya serikali. Nilitaka nizungumze zaidi kwenye Jimbo langu la Ole na kama Wajumbe watakumbuka Jimbo langu la Ole lina maziwa karibu thelathini, mwahali ambamo maji yanakaa kwa muda wa mwaka au miaka miwili inategemea mvua. Wakulima ambao wanazunguka maziwa yale ni zaidi ya elfu moja, naamini kabisa Wizara ya Kilimo hili wanalifahamu.

Mwaka jana wananchi wa jimbo la Ole walianzisha kilimo cha vitunguu tena cha kubahatisha bahatisha tu walivuna zaidi ya tani mbili. Sasa naomba Wizara ya Kilimo na Maliasili kwanza hili walifahamu lakini walichukue sasa kama *case study* wawasaidie hawa wakulima, tena ikiwezekana wote ambao wana mashamba kando kando ya maeneo yale ambayo maji yanakaa kwa muda wa miaka miwili au mitatu. Naamini kabisa wakiichukua hii kama ni *case study* jimbo la Ole likishirikiana na la Kojani, likishirikiana na jimbo la Wawi kwa sababu kote huko maeneo haya yapo tunaweza tukatoa vitunguu na suala la kuagizia vitunguu kutoka *main land* likawa halipo, nina hakika kabisa. Sasa hii ni moja katika lile ambalo nilitaka leo Wizara ya Kilimo niwaachie.

Jengine Mhe. Spika, ni *extension services*, kilimo kama huna hawa watu wanaopita mabwanashamba hata ukawa na miradi kiasi gani na ukubwa gani hicho kilimo hakitakuwa. Najua wapo lakini hawatoshi, tuna Chuo cha kilimo Mhe. Spika, kama tutakuwa na watu wanaofanya shughuli hizi za *extension services* kama zamani, mimi nina hakika kabisa wakulima wetu popote walipo wangekuwa wanapata huduma wasingelalamika sana, na nina hakika kabisa mambo mengine madogo madogo wala hapa yasingetajwa.

Katika mambo ya utafiti katika Wizara ambayo kwenye miaka ya 1980 – 1990 ilikuwa na wataalamu wengi tena waliobobea ni wizara hii, wengine wameondoka lakini naamini waliopo wanatosha Mhe. Spika. Wataalamu wetu hawa sijui kwa nini hawako *active* kama walivyokuwa zamani. Wakati wizara hii katika awamu ya saba inaanzishwa waziri wa mwanzo wa wizara hii katika awamu ya saba ni Mhe. Mansoor Yussuf Himid; na haya Mapinduzi ya Kilimo hii ndio *slogan* ambayo yeye ameivalia njuga na kwa kweli sote tunajua kwamba namna ambavyo kilimo kilikuwa kina *pick up*. Kwa hivyo, mimi namshauri tu mwenzangu Mhe. Waziri wa Kilimo kasi

ile ile ambayo aliikuta kwa Mhe. Mansoor kwa sababu watendaji ni wale wale basi yeye nafikiri aongeze mara mbili.

Mhe. Spika, kilimo kinachukua asilimia zaidi ya 80 ya wananchi wetu ndio kazi yao, ingawa bajeti yake ndogo sana maana yake ni huo uwezo mdogo tu wa serikali, lakini Wizara ya Kilimo kwa bajeti ya shilingi bilioni kumi na moja kama ni miradi basi ni kidogo sana. Nasema ni kwa sababu uwezo mdogo wa serikali, lakini ingekuwa ni uwezo mkubwa basi asilimia 80 ya wananchi wa Zanzibar wanaotegemea kilimo basi iwe na bajeti kubwa zaidi ya asilimia 20 ya bajeti ilikuwa iende kule na nyengine kubwa kama hivyo iende kwenye elimu.

Katika utafiti Mhe. Spika, naomba Wizara ya Kilimo mambo mawili wayafuatilie na kwa ukaribu sana, kwanza ni mafunza katika matunda. Mhe. Spika, utakuta miembe imezaa matunda yapo ya kutosha lakini hayafai kitu, hakuna mtu yeyote anayenunua embe yenye funza. Kwa hivyo zile zinaanguka, zinaharibika hakuna la kufanya. Sasa *research* katika kufanya najua siku hizi kuna vikopo hivi na dawa, lakini hata hivyo bado havijakidhi haja. Katika kupunguza umasikini utafiti huu mimi nasema uendelezwe vyenginevyo miembe hii hatimaye itang'olewa, itakatwa au watu watajenga sawa sawa na Mhe. Hamza alivyosema, utakuta muembe una miaka 50 unang'olewa mtu anajenga kibanda. Kwa kweli inaumiza sana, lakini itaendelea kung'olewa kama kila embe inayozaliwa inakuwa na funza, mtu haitaki sasa miembe ya nini. Kwa hivyo Wizara ya Kilimo katika haya ishughulikie kwa makini sana.

Lakini jengine Mhe. Spika, ni suala la hiyo hiyo miembe. Jimbo la Ole lina miembe zaidi ya 20 elfu inayozaa na kuna miembe mingine utakuta hasa ikifika Septemba yaani haya majani huyaoni kwa maua ni pambo la kutosha, lakini miembe hiyo hiyo mwisho wake utakuta embe zinazopatikana basi si hata asilimia 20 ya yale maua ambayo umeyaona. Sasa hili vile vile ni vyema Wizara ya Kilimo nalo wakalivalia njuga kilimo ndio uhai.

Mhe. Spika, kama nilivyokwambia Mapinduzi ya Kilimo yamekuja na kasi nzuri na wananchi wamehamasika kupita kiasi, yoyote anayepita katika ukanda wa Mashariki ya Pemba kuanzia Chambani unakwenda zako mpaka Kiungoni wananchi walivyolima mpunga mwaka huu kwa kuitikia na kutekeleza sera hii ya Mapinduzi ya Kilimo Mhe. Spika, huwezi kuamini. Ni wito ambao umeitikiwa kikamilifu, lakini sasa kila unapopita wananchi wanalia mipunga imekuwa mifupi, imeungua, haikuvunwa. Sasa na hili vile vile nasema jukumu lote hili ni la Wizara ya Kilimo, wananchi wanaitikia wito wamepata pembejeo japo mbegu nyengine hazikutosha, lakini hakuna atakaevuna.

Juzi wananchi wa Jimbo la Ole wananiambia Mheshimiwa tumeshalima na hali ni kama hiyo nini shauri, kwani sisi hatuwezi kusaidiwa kwa sababu hali kama hii ni njaa, tumelima tukiamini kwamba tutavuna hakuna aliyevuna. Wenzetu Bara huko hali kama hii wanasaidiwa chakula, hivyo kweli serikali yetu haijafanya utaratibu huo? Mimi sikuwa na jawabu, lakini kwa sababu suala la chakula, suala la kilimo liko wizara hii basi kwanza ni vyema Mhe. Waziri na watendaji wako ukanda ule mpite kama hamjapita, tena kipindi hiki kabla watu hawajaanza kulima. Kwa sababu watu wakianza kulima hamtaona athari iliyopo sasa hivi bado mipunga mwengine iko vile vile, inasikitisha unaweza ukalia ukatoka machozi na mtu ameuza pengine mpaka alichokuwa nacho kununua hiyo mbolea na pembejeo nyengine kama dawa za magugu lakini hatimaye hakuna hata robo atakayorudisha.

Mhe. Waziri wa Kilimo na watu wako wapite kule waone ile hali nafikiri wataweza kuona kwamba kweli kuna haja ya watu hawa kusaidiwa kwa namna moja au nyengine, na msaada huo ndio tukawaambia wao kwamba kweli tuliharibikiwa kumbe na kilimo chetu basi serikali inaweza ikatufikiria. Si lazima wapate kila wanachokitaka lakini hata ile kuwaambia tu wananchi mmefanya hili lakini mambo yako hivi, yako hivi mtu anataka *recognition* aone kwamba kitu alichofanya kwa kuitikia serikali basi na serikali inamthamini, sisemi wapewe mamilioni au wapewe magunia ya mchele lakini nasema utaratibu wa mtu kum-*recognize* mkulima ili mwakani akafanya zaidi ya alivyofanya tena kwa moyo kabisa.

Mhe. Spika, la mwisho kabisa katika ukurasa wa 43 kuna changamoto za wizara. Changamoto hizi ziko sita lakini mimi nazungumzia changamoto ya pili. Mabadiliko ya hali ya hewa; kuongezeka kwa kiwango kikubwa cha mvua za vuli zilizonyesha kwa muda wa miezi miwili zilipelekea kuchelewa kwa kazi ya ukulima wa matrekta na kusababisha huduma za matrekta kutofanyika kama ilivyopangwa kwa baadhi ya maeneo.

Mhe. Spika *ukupigao ndio ukufunzao*, hili mwaka huu limetokea lakini hatusemi halitatokea tena, mvua za vuli ni baraka lakini zile mvua kwa sababu zilikuwa ni za muda mrefu watu wengi hawakuweza kulimiwa, na kama hukuweza kulimiwa ni kwamba wewe mwenyewe hutaweza kulima eneo lile ambalo lilimwe na trekta. Sasa ni vizuri niwakumbushe Wizara ya Kilimo kwamba, kama hili limetokea mwaka huu vile vile linaweza likatokea tena mwakani na mwaka wa mwakani, sasa wajiandae ili hata kama litatokea mwakani kama lilivyotokea mara hii basi wawe na njia nyengine. Kwa sababu ukishajua changamoto ni hii lazima utafute ufumbuzi wake. Lakini mwaka huu limetokea hilo na mwakani *statement* ikaja ikawa hii hii tena, sidhani kama watatufahamu au mwaka wa mwakani. Ni vizuri sana wakajipanga mapema ili mwaka huu limetokea mwakani likitokea kuna njia ya ku-*counter* hili ili nao wakulima wasivunjike moyo katika masuala haya hasa ilivyokuwa limejulikana.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ole naunga mkono bajeti ya wizara hii kwa asilimia zote. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nilitangulia kusema mapema kwamba Mhe. Waziri aliniomba kwamba apate muda ajitayarishe kwa ajili ya kufanya majumuisho kesho. Kutokana na ufinyu wa muda tukasema basi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ianze kuwasilisha hotuba yake. Kwa hivyo, kesho tunategemea kufanya majumuisho asubuhi mara baada ya kumsikiliza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Hivyo tunasitisha majadiliano haya na kuendelea kesho asubuhi pamoja na majumuisho. Tunaendelea na Wizara ya Miundombinu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2012/2013 – Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii naomba sasa Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili na hatimae kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kutokana na mabadiliko yaliyotokea *paragraph* ya 96 ya kitabu chetu itakuwa haimo. Hii imetokana na tatizo la uchapishaji, kwa hivyo baada ya *paragraph* ya 95 itafuata *paragraph* ya 97.

Mhe. Spika, kwa jila Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma na ukarimu naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ili liweze kupokea, kuzingatia, kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki cha Baraza la Wawakilishi kinachojadili Bajeti ya Serikali ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii pia kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dr. Ali Muhammed Shein kwa ushauri na muongozo mzuri anayoipatia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, ushauri na miongozo hiyo imesaidia sana kuongeza ufanisi wa kazi na kasi ya utekelezaji wa majukumu ya wizara yetu. Aidha, namshukuru Mhe. Rais kwa kuanzisha utaratibu mpya wa kukutana na Wizara za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kujadili taarifa za utekelezaji wa mpango kazi kwa kila robo ya mwaka (Bango Kitita) kuona utekelezaji wa bajeti zinazopitishwa na Baraza lako Tukufu. Nakiri kwamba utaratibu huu umeifanya Wizara yangu na nyenginezo kutekeleza mipango yake ya kila siku kwa uangalifu, ufanisi na uwazi zaidi na kwa kuzingatia bajeti iliyowasilishwa kwa kila idara husika. Utaratibu huu ni mpya na umeleta mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, napenda nimpongeze Makamo wa Kwanza wa Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad na Makamo wa Pili wa Rais Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa jinsi wanavyomsaidia Mhe. Rais katika kumshauri na kutekeleza majukumu aliyowapa. Aidha, ushirikiano wa viongozi hawa kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano umetufanya tuweze kutekeleza kazi zetu kwa ufanisi, uwazi na kujiamini zaidi. Maoni na busara zao zimekuwa zikisaidia sana katika kuhakikisha kuwa maamuzi ya wizara yanakwenda sambamba na matakwa ya serikali kwa manufaa ya Wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, napenda pia nikupongeze wewe binafsi kwa hekima, umahiri na busara zako unazozitumia katika kuliongoza Baraza lako tukufu ambalo limekuwa likifanya maamuzi muhimu na magumu almuradi tu maamuzi hayo ni kwa manufaa ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya wizara yangu pamoja na wananchi wote wa Zanzibar, naomba nichukue nafasi hii kuwapa pole wale wote walioguswa kwa namna moja au nyengine katika ajali ya *M.V. SKAGIT*. Aidha, ajali hiyo ni janga jengine kubwa lililoacha kovu lisiloweza kusahaulika.

Mhe. Spika, naomba Mwenyezi Mungu atupe moyo wa subira majeruhi wapone upesi na tushirikiane katika kukabiliana na changamoto zingine kuhusiana na usalama wa safari zetu za baharini. Mhe. Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo, wizara yangu tunahakikisha kwamba taratibu na sheria zilizopo kuhusiana na usalama wa usafiri wan chi kavu na baharini zinafuatwa kwa vitendo, na kama kuna mmiliki yoyote wa vyombo vya baharini hawezi kutoa ushirikiano wake naomba abadili msimamo huo. Tunahakikisha suala la uchakavu wa vyombo vya baharini tunalipa kipaumbele maalum ili kukabiliana nalo.

Mhe. Spika, napenda kumpongeza Mhe. Omar Yusuf Mzee, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na watendaji wake wote kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha tarehe 13 Juni, 2012 ambayo ilieleza na kufafanua kwa kina hali yetu ya kiuchumi, Mipango ya Maendeleo ya nchi yetu na malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi kijacho cha mwaka wa fedha 2012/2013. Aidha, hotuba hiyo ilitoa mwelekeo wa kuimarisha Miundombinu katika usafiri wa baharini, angani na nchi kavu. Pia nampongeza Mhe. Waziri kwa mara ya kwanza ameanzisha mfumo mpya wa bajeti uitwao "*Programme Based Budget - PBB*" inayotumia mfumo wa programu ambayo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni miongoni mwa Wizara tano zinazoanza majaribio ya mfumo huo.

Mhe. Spika, naomba nitoe shukurani zangu za dhati kwa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mwakilishi wa Jimbo la Kitope kwa maoni, hoja, mapendekezo na maelekezo ambayo yamesaidia sana Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika utekezaji wa shughuli zake za kila siku. Aidha, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa ushauri wao kwetu na tunawaomba muendelee kuwa karibu na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa lengo la kutushauri, kutukosoa na kutuelekeza na hatimae tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Spika, nataka kwa makusudi na kwa dhati niipongeze Kamati Teule chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Omar Ali Shehe na wajumbe wake wote kwa taarifa yao ambayo iliwasilishwa vizuri katika kikao cha Baraza kilichopita. Ni taarifa iliyoitanabahisha Serikali na watendaji wake, lakini iliyobainisha changamoto kadhaa katika sekta mbali mbali za wizara walizopata kuzifanyia kazi. Taarifa hii itaisaidia sana Serikali katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika, napenda kumshukuru sana Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano Mhe. Issa Haji Ussi Gavu, Mwakilishi wa Jimbo la Chwaka kwa kusaidiana na mimi katika utekelezaji wa

majukumu ya wizara. Umahiri na usimamizi wake wa kazi umesaidia sana kuyapatia ufumbuzi masuala mengi tuliopanga kuyatekeleza. Vile vile, nawapongeza Katibu Mkuu Dr. Vuai Iddi Lila, Naibu Katibu Mkuu Nd. Msanif Haji Mussa, Wakurugenzi wote, watendaji wa taasisi na wafanyakazi wote wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ushirikiano na kwa kadri walivyojitahidi kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa shukurani zangu za dhati za kipekee kwa mtangulizi wangu Mhe. Hamad Masoud Hamad pamoja na wananchi wake wote wa Jimbo la Ole anaowawakilisha na nawaomba wote kwa pamoja kuwa wavumilivu sana kwa yote yaliyojitokeza.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 4,255,000,000 kwa kazi za kawaida na shilingi 9,387,598,000 kwa kazi za maendeleo. Aidha, wizara ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 1,757,990,000.

Hadi Machi 2012 jumla ya shilingi 4,523,028,711 zilipatikana kwa matumizi ya kazi za kawaida, sawa na asilimia 106 na shilingi 5,630,995,276 kwa kazi za maendeleo sawa na asilimia 60. Aidha, wizara ilikusanya shilingi 2,385,386,648, sawa na asilimia 136. (Kiambatanisho namba 1.)

UTEKELEZAJI WA KAZI ZA MAENDELEO NA ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2011/2012 NA MALENGO YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013, Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeandaliwa kwa kufuata muongozo wa Bajeti ya Serikali ambao unasisitiza utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II). Vile vile, bajeti hii imezingatia maoni, maelekezo na miongozo ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wakati wa kuwasilisha na kujadili utekelezaji wa mpango kazi wa kila robo mwaka ya bajeti ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, majukumu makuu ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ni kujenga, kuitunza, kuimarisha na kuendeleza miundombinu na kutoa huduma za usafiri na mawasiliano kwa ujumla wake. Katika kutekeleza hilo, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imepewa jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa usafiri wa baharini, nchi kavu na anga ambao ni salama, nafuu na wenye kukidhi matakwa ya watumiaji. Sambamba na hilo, Wizara pia inajukumu la kuratibu na kusimamia masuala ya mawasiliano hapa Zanzibar.

Majukumu hayo ya Wizara yanatekelezwa kupitia taasisi zifuatazo:
1. Ofisi Kuu Pemba.
2. Idara ya Mipango, Sera, na Utafiti.
3. Idara ya Uendeshaji na Utumishi.
4. Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara.
5. Idara ya Usafiri na Leseni.

6. Idara ya Mawasiliano.
7. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.
8. Mamlaka ya Usafiri Baharini.
9. Shirika la Meli na Uwakala.
10. Shirika la Bandari.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika**,** Ofisi Kuu Pemba inaratibu na kusimamia shughuli za Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa upande wa Pemba.

Katika kipindi cha 2011/2012 Ofisi kuu Pemba iliweza kutekeleza kazi zake za uratibu wa matengenezo ya barabara, utoaji wa leseni na ukaguzi wa magari, uimarishaji wa huduma katika kiwanja cha ndege, pamoja na kusimamia masuala ya utumishi na uendeshaji wa Ofisi Kuu. Utekelezaji wa miradi ya maendeleo utaelezwa kwa ufasaha zaidi katika maelezo ya sekta husika.

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha 2011/2012 Ofisi Kuu Pemba ilikadiriwa kutumia jumla ya Tsh 1,065,000,000 kwa kazi za kawaida na kukusanya jumla ya Tsh. 98,980,000 kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato.

Hadi Machi 2012 fedha zilizoingizwa ni Tsh. 879,966,277 sawa na asilimia 83 na ilikusanya jumla ya Tsh. 87,628,623 sawa na asilimia 89.

Malengo kwa Mwaka 2012-2013

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi Kuu Pemba inatarajia kutekeleza majukumu yake ya kazi za kawaida na kuratibu kazi za maendeleo kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika, katika mwaka 2012/2013 Ofisi Kuu Pemba inakadiriwa kukusanya jumla ya Tsh 42,500,000 na inaombewa jumla ya Tsh 1,356,800,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika**,** majukumu makuu ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa Sera na Mipango ya sekta za Usafiri na Mawasiliano. Idara pia inaratibu kazi zote za maendeleo za Wizara zikiwemo kubuni, kutayarisha na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Idara ina jukumu la kubuni na kufanya tafiti katika sekta za usafiri na mawasiliano. Ili kutekeleza shughuli za utafiti, Idara inakusanya takwimu mbali mbali zinazohusiana na sekta za usafiri na mawasiliano.

Mhe. Spika**,** katika kipindi cha 2011/2012, Idara iliendelea na utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Taifa wa Usafiri wa Zanzibar (Zanzibar Transport Master Plan). Katika kipindi hicho, Wizara imekamilisha

taratibu za kumpata mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu wa mageuzi ya mfumo wa taasisi za Wizara (Institutional Reform), ilikamilisha sheria ya uanzishwaji wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Sheria ya Usimamizi wa Viwanja vya Ndege, iliendelea na matayarisho ya Sheria ya uanzishwaji Mamlaka ya Barabara, Sheria ya Shirika la Meli na Uwakala, ukamilishwaji wa taratibu za kuifanya Mamlaka ya Baharini (ZMA) kujitegemea na uandaaji wa Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mhe. Spika, Idara imeendelea kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya sekta ya usafiri wa barabara, sekta ya usafiri wa anga na sekta ya usafiri baharini. Aidha, Idara imekamilisha kazi ya usanifu na utayarishaji wa zabuni wa barabara za kuingia mjini (Zanzibar Town Entry Roads). Idara pia imekamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za ujenzi wa barabara ya Chake-Chake,Wete kwa Pemba na upembuzi yakinifu ya barabara za vijijini- Unguja.

Mhe. Spika**,** katika mwaka 2011/2012 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilipangiwa kutumia jumla ya Tsh 150,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi Machi 2012, Fedha iliyoingiziwa kwa kazi za kawaida ni Tsh 91,000,000 sawa na asilimia 61.

Malengo kwa Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa 2012/2013, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuhakikisha kuwa Mpango Mkuu wa Usafiri wa Zanzibar (Zanzibar Transport Masterplan) unaendelea kutekelezwa. Idara itaendelea kuratibu na kufuatilia miradi ya maendeleo, utayarishaji wa sheria na kanuni mbali mbali za udhibiti wa sekta za usafiri wa baharini, nchi kavu na anga. Idara itakamilisha Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na kuimarisha kitengo cha utafiti ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika**,** kama nilivyoahidi katika bajeti iliyopita, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti itaratibu uanzishwaji wa Vyuo maalum vya kufundisha wataalamu wa fani ya Ndege na fani ya Ubaharia hapa Zanzibar (Establishment of Zanzibar Civil Aviation Academy and Zanzibar Maritime Training Institute). Naomba kutamka mbele ya Baraza lako tukufu kuwa kazi hii imeanza kutekelezwa kwa kuanza na uundwaji wa Kamati za kuratibu shughuli hizi. Kazi za kamati hizi zinaendelea kufanyika/kutekelezwa.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti inaombewa jumla ya Tsh 250, 000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, jukumu la kusimamia na kutathmini shughuli za uendeshaji na maendeleo ya watumishi wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano linasimamiwa na Idara ya Uendeshaji na Utumishi.

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2011/2012 Idara imetekeleza na kusimamia masuala ya kiutumishi na uendeshaji ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kuimarisha mazingira mazuri ya kazi kwa kuhakiksha upatikanaji wa vifaa vya kutendea kazi ili kuwawezesha wafanyakazi kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kushirikiana na Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea na kazi ya kutayarisha muundo wa utumishi wa Wizara na kuhakisha kuwa wafanyakazi wanapangiwa majukumu yao ya kazi (job description) kwa mujibu wa elimu zao na kupandishwa vyeo kila wanapostahiki.

Mhe. Spika, jumla ya wafanyakazi 43 wamepatiwa mafunzo mbali mbali ndani na nje ya nchi kwa viwango tofauti (Kiambatanisho Nam.2). Aidha, Wizara kupitia Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeendelea na jitihada za kuwaelimisha wafanyakazi wake umuhimu wa kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI kwa kutoa mafunzo kwa njia ya semina na mikutano kwa wafanyakazi wake. Vile vile Idara imeratibu upatikanaji wa mafao ya wafanyakazi 80 waliostaafu kwa mujibu wa sheria za utumishi Serikalini.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2011/2012 Idara ya Uendeshaji na Utumishi ilipangiwa kutumia jumla ya Tsh 632,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Fedha halisi zilizotolewa katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012 ni Tsh 680,606,500 sawa na asilimia 108.

Malengo ya Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika**,** Idara itaendelea kutekeleza masuala ya kiutumishi na Uendeshaji ya Wizara. Idara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora itakamilisha muundo wa utumishi (Scheme of service) wa Wizara ambapo wafanyakazi watapandishwa madaraja hatua kwa hatua na kupangiwa kazi kwa mujibu wa taaluma walizonazo. Aidha, Idara itasomesha wafanyakazi kozi mbali mbali kwa mujibu wa mahitaji ya Wizara.

Katika mwaka 2012/2013, Idara ya Uendeshaji na Utumishi inaombewa jumla ya Tsh 1,279,000,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

SEKTA YA USAFIRI WA NCHI KAVU.

Mhe. Spika**,** Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina jukumu la kuwapatia wananchi huduma bora za usafiri wa barabara kwa kuendeleza ujenzi na utunzaji wa barabara, madaraja na pia

kusimamia vizuri zaidi masuala ya usalama barabarani. Majukumu hayo yanatekelezwa na Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara pamoja na Idara ya Usafiri na Leseni.

Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara

Mhe. Spika**,** hadi kufikia mwezi Machi 2012 Wizara kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara imezifanyia matengenezo barabara kadhaa za mjini na vijijini Unguja na Pemba kwa kutumia mfuko wa barabara. (kiambatanisho Nam.3a)

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 5,000,000 kutokana na mapato mengineyo na ilitengewa jumla ya Tsh 1,004,418,000 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida.

Hadi Machi 2012 jumla ya Tsh 3,200,000 zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 64 na fedha zilizotolewa kwa kazi za kawaida ni Tsh 866,095,055 sawa na asilimia 86 ya makadirio.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara inakusudia kuendelea kutekeleza na kusimamia miradi mbali mbali ya ujenzi wa barabara iliyopangiwa. Aidha, Idara kupitia Mfuko wa Barabara itaendelea kuzitunza na kuzifanyia matengenezo barabara mbalimbali za mijini na vijijini Unguja na Pemba ili kuzifanya zipitike kwa muda wote kwa lengo la kuwarahisishia wananchi usafiri. Angalia kiambatisho 3B.

Mhe. Spika**,** kwa upande wa kazi za maendeleo, Wizara kwa kipindi cha mwaka 2011/2012 ilipanga kutekeleza jumla ya miradi 12 ya ujenzi wa barabara. Kwa mwaka 2012/2013 inakusudia kuendeleza miradi 10. Taarifa za utekelezaji wa miradi hiyo na fedha inazoombewa kwa 2012/13 ni kama ifuatavyo:

(i) Mradi wa Barabara Kuu za Zanzibar:

Mradi huu unaogharamiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) unahusisha barabara za Amani–Dunga yenye urefu wa kilomita 12.7, Mfenesini-Bumbwini yenye urefu wa kilomita 13.2 na madaraja 4 katika barabara ya Mahonda-Donge-Mkokotoni umekamilika kwa asilimia 99. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, fedha zilizopatikana ni Tsh 1,860,035,910 sawa na asilimia 169 ya makadirio.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013 mradi huu unaombewa jumla ya Tsh 1.5 bilioni kutoka Serikalini kwa ajili ya kumlipa mkandarasi na malipo ya fidia.

Mradi wa Barabara za Vijijini Kusini Pemba (South Pemba Rural Roads)

Mhe. Spika**,** mradi huu uliogharimiwa na Serikali ya Norway pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulijumuisha ujenzi wa barabara sita (6) za vijijini Kusini Pemba, zenye jumla ya urefu wa km 45 ambazo ni:
Mtambile–Kengeja-Mwambe (km 9.4)**,** Mtambile–Kangani (km 6.4), Mizingani-Wambaa (km 9.7), Kenya-Chambani (km 3.2), Chanjamjawiri-Tundaua (km 11) na Chanjaani- Pujini (km 5). Mradi huu umekamilika kwa asilimia 99 ambapo kazi zilizosalia za kuweka alama za barabarani zinaendelea kutekelezwa.

Hadi kufikia mwezi Machi 2012, fedha zilizopatikana ni Tsh 804,774,499 sawa na asilimia 94 ya makadirio.

Mradi wa Barabara tatu za Kaskazini Pemba

Mhe. Spika**,** mradi huu unaogharamiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (Saud Fund) unazihusisha barabara za Wete – Konde (km 15.0) na Wete – Gando (km.15.0) kwa awamu ya kwanza. Awamu ya pili itahusisha ujenzi wa barabara ya Wete-Chake 22.1km.

Mhe. Spika**,** kwa upande wa barabara ya Wete–Konde jumla ya km 14 zimeshajengwa kwa kifusi tabaka la pili (Sub base) na jumla ya kilomita 2 zimeshajengwa kwa kifusi tabaka la mwisho (base course). Aidha, kwa Barabara ya Wete-Gando jumla ya km 9.4 zimeshasafishwa kati ya hizo km 6 zimeshajengwa kwa kifusi tabaka la pili (sub base). Ujenzi wa nyumba kwa ajili ya wahandisi wasimamizi na wafanyakazi wengine pamoja na maabara umekamilika na kuanza kutumika.

Hadi kufikia mwezi Machi 2012, fedha zilizopatikana ni Tsh 1,320,716,918 sawa na asilimia 60 ya makadirio.

Mhe. Spika**,** utekelezaji wa mradi huu unakabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo kuchelewa kulipa fidia za nyumba, vipando, kuchelewa kuondoa miundo ya mabomba ya maji, nguzo za umeme pamoja na vikwazo vyengine ili kumpa mkandarasi eneo la kujenga. Aidha, kuchelewa kumlipa mkandarasi madai yake kwa wakati, mvua kubwa iliyonyesha kuanzia mwezi Septemba hadi Disemba 2011 na Mkandarasi kubadilisha wafanyakazi ni miongoni mwa changamoto zilizopelekea kutokwenda kwa kasi inayotakiwa utekelezaji wa mradi huu.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara inakusudia kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara hizo na kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu changamoto nilizozieleza hapo awali na jumla ya Tsh 3.5 bilioni zinaombwa kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mradi wa Barabara ya Wete-Chake
Mhe. Spika**,** mradi huu ni mpya na unagharimiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA) na Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (Saud Fund) na unalengo la kuijenga kwa kiwango cha lami barabara ya Chake-

Wete yenye urefu wa kilomita 22. SMT imeshatiliana saini ya mkopo wa USD 20 milioni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii.
Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara inakusudia kuanza kazi za ujenzi wa barabara hiyo na jumla ya Tsh 900 milioni zinaombwa kutoka Serikalini kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

Mradi wa Barabara ya Ole-Kengeja
Mhe. Spika**,** mradi huu unagharamiwa na Jumuiya ya Nchi zinazosafirisha Mafuta kwa Wingi Duniani (OPEC) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao una lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami barabara inayoanzia Ole hadi Kengeja yenye urefu wa kilomita 35. Tathmini za zabuni za ujenzi kwa barabara hiyo na usimamizi zimeshakamilika. Kutokana na gharama za ujenzi kuwa kubwa kulingana na fedha zilizotengwa, Wizara inaendelea na mazungumzo na mfadhili wa mradi huo juu ya uwezekano wa kutumia mfumo wa nguvu kazi (labour base) katika kutekeleza mradi huo, ambao utawezesha kujenga barabara yote kwa fedha zilizopo. Mfumo huu ndio uliotumika kujenga barabara sita za vijijini Kusini Pemba.
Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya Tsh 50 milioni zinaombwa kutoka Serikalini, kwa ajili ya gharama ndogo ndogo kwani gharama kubwa za mradi zitalipwa na mfadhili wa mradi huu OPEC.

Mradi wa Barabara za Vijijini Kaskazini Pemba:
Mhe. Spika**,** mradi huu unagharamiwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Marekani kwa kupitia Mfuko wa Changamoto ya Millenia (MCC). Mradi huu una lengo la kujenga kwa kiwango cha lami barabara 5 za Kaskazini Pemba zenye jumla ya km 35 ambazo ni:
Mzambarauni-Pandani-Finya (km 7.9), Bahanasa-Daya-Mtambwe (km 13.6), Chwale-Kojani (km 1.9), Kipangani-Kangagani (km 2.7) na Mzambarauni – Mapofu (km 8.9).
Hatua za utekelezaji zinaendelea kwa kazi za kusafisha barabara (earth works) na kuanza kuweka kifusi cha mwanzo.
Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya Tsh 50 milioni zinaombwa kutoka Serikalini.

Barabara ya Mgagadu-Kiwani
Mhe. Spika**,** mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na una lengo la kuijenga barabara ya Mgagadu-Kiwani yenye jumla ya km 7.6. Hadi Machi 2012 kazi za uwekaji kifusi tabaka la mwanzo na la pili kwa km 4 na ujenzi wa kalvati 5 umekamilika. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, fedha zilizopatikana ni Tsh 150,000,000 sawa na asilimia 50 ya makadirio.
Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara inakusudia kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara hii na jumla ya Tsh milioni 400 zinaombwa kutoka Serikalini.

Barabara ya Pale-Kiongele.
Mhe. Spika**,** mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na una lengo la kuijenga barabara inayoanzia Pale-Kiongele hadi Mkwajuni yenye urefu wa km 11. Hatua iliyofikiwa hadi sasa ni kukamilika kwa ujenzi wa daraja moja.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara inakusudia kuendeleza mradi huu na hakuna fedha zinazoombwa kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kutoka mfuko wa Serikali kwa vile ujenzi wake utagharamiwa kupitia Mfuko wa Barabara.

Barabara ya Mkanyageni-Kangani

Mhe. Spika**,** mradi huu umepangwa kutekelezwa mwaka wafedha 2012/2013 baada ya kukamilika kwa barabara ya Mgagadu-Kiwani na unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mradi una lengo la kuijenga barabara inayoanzia Mkanyageni hadi Kangani yenye urefu wa kilomita 6.5 kwa kiwango cha lami.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya Tsh milioni 100 zinaombwa kutoka Serikalini.

Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Amani-Mtoni (Benjamin Mkapa)

Mhe. Spika**,** huu ni mradi unaoendelea na una lengo la kujenga sehemu ya pili ya barabara ya Amani – Mtoni yenye urefu wa km 4. Hatua ya uwekaji kifusi tabaka la mwanzo na tabaka la pili kwa sehemu kubwa na ujenzi wa makalvati zimefanyika.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara inakusudia kuendeleza mradi huu na hakuna fedha zinazoombwa kutoka mfuko wa Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa vile ujenzi wake utagharamiwa kupitia Mfuko wa Barabara.

Mradi wa Upembuzi yakinifu wa barabara zinazoingia Mjini (Zanzibar Urban Entry Roads)

Mhe. Spika**,** huu ni mradi wenye lengo la kufanya upembuzi yakinifu, usanifu na utayarishaji wa makisio na zabuni kwa barabara 7 zenye urefu wa km 78.5. Mradi huu unagharamiwa na Benki ya Dunia na unazijumuisha barabara za Bububu-Mtoni-Kinazini-Malindi Port (km 19), Creek road-Mkunazini-Mnazi Mmoja (km 1.2), Tunguu-Fuoni-Magomeni-Kariakoo-Mkunazini (km 13.3), Welezo-Amani-Ng'ambo-Kariakoo (km 3.5), Mtoni-Amani-Kiembe Samaki (km 8.5), Uwanja wa Ndege-Kiembe Samaki-Kilimani-Mnazi Mmoja (km 7) na Bububu-Mahonda-Mkokotoni (km 31).

Hadi Machi 2012, Mshauri wa kazi hii amekamilisha upembuzi yakinifu, tathmini ya mazingira na fidia kwa watu watakaoathirika na mradi huu, utayarisha wa usanifu na zabuni za barabara husika, ambapo tayari ameshawasilisha rasimu ya mwisho ya ripoti ya usanifu na zabuni.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Mendeleo inakusudia kutafuta fedha kwa kupitia njia ya msaada na mkopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa mradi na unaombewa jumla ya Tsh 50 milioni kutoka Serikalini.

Mradi wa Barabara 3 za Vijijini Unguja

Mhe. Spika**,** huu ni mradi unaoendelea na unagharamiwa kwa pamoja baina ya Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mradi huu unazijumuisha barabara za Kizimbani-Kiboje (km 7.2), Koani-Jumbi (6.3) na Jendele-Cheju-Kaebona (km 11.7). Taratibu za kumpata Mshauri zimekamilika na taratibu za kumpata Mkandarasi zinaendelea.

Kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inakusudia kutekeleza mradi huu na unaombewa jumla ya Tsh 1.5 bilioni kutoka Serikalini.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013 Idara ya Ujenzi na Utunzaji Barabara inatarajia kukusanya jumla ya Tsh 6,000,000 na inaombewa jumla ya Tsh 1,458,500,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara inakusudia kukamilisha ujenzi wa barabara zilizosalia katika miradi mbali mbali. Jumla ya Tsh 8.050 bilioni zinaombwa kutoka Serikalini kwa utekelezaji wa mpango wa maendeleo katika sekta ya barabara (Kiambatisho 4).

Mhe. Spika,katika kutekeleza mpango wa Serikali wa kupambana na umasikini na kuishirikisha sekta binafsi Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara imeendelea na utaratibu wa kutoa baadhi ya kazi kwa kampuni binafsi, vikundi vya jamii na jumuiya zisizo za Serikali. Kwa sasa kazi zinazotolewa ni za ujenzi wa madaraja madogo madogo, ukataji majani, usafishaji wa misingi ya maji na usafishaji wa kalvati, matengenezo madogo madogo na kazi nyenginezo. Hatua hii inaendelea kujenga msingi mzuri wa utekelezaji wa sera ya ushirikiano wa sekta ya umma na sekta binafsi. Wizara katika mradi wake wa mageuzi ya mfumo wa taasisi inakusudia kuweka mikakati ya kujenga uwezo wa kampuni hizo ili hapo baadae ziweze kushiriki katika miradi mikubwa ya barabara.

Idara ya Usafiri na Leseni.

Mhe. Spika**,** Idara hii ina majukumu ya kusimamia usalama wa watumiaji wote wa barabara, kuendesha shughuli za ukaguzi wa vyombo vya moto, usimamizi wa mafunzo ya udereva, upasishaji madereva na walimu wa skuli za udereva, kusimamia utoaji huduma usafirishaji abiria na mizigo kwa njia ya barabara.

Aidha, Idara inasimamia na kuendesha Karakana kuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyoko Chumbuni na sehemu ya mitambo iliyoko Pemba.

Mhe. Spika**,** hadi kufikia mwezi Machi 2011 jumla ya vyombo vya moto 25,791 vilikaguliwa (Kiambatanisho Nam 5a). Aidha, Idara iliwafanyia mitihani ya nadharia na vitendo jumla ya madereva wanafunzi 5,725 waliohitimu katika skuli mbali mbali za udereva, kati ya hao 3,492 ni madereva wa magari na 2,233 ni madereva wa vyombo vya maringi mawili. (Kiambatanisho Nam 5 b).

Mhe. Spika**,** katika kipindi hicho Idara ilitoa ruhusa za njia kwa magari 1,990 Unguja na Pemba, kati ya ruhusa hizo magari ya shamba 602, daladala 396, private hire 427, taxi 139, magari ya wanafunzi 10, magari ya wafanyakazi 20 na magari ya mizigo 396.

Aidha, Idara imeendesha vipindi mbali mbali kuhusiana na usalama barabarani (elimu kwa umma). Idara ilizindua muongo (decade) wa masuala ya usalama barabarani na kuwashirikisha wadau mbali mbali wakiwemo wanafunzi na madereva.

Vile vile, Idara iliendelea na kazi ya uuzaji wa Bendera za Serikali. Idadi ya bendera za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizouzwa katika kipindi hicho ni 419 na za Muungano 193.

Mhe. Spika**,** Karakana Kuu ilizifanyia matengenezo jumla ya gari 445 katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012 ikiwa ni sawa na upungufu wa asilimia 19 ukilinganisha na gari 552 zilizotengenezwa katika kipindi kama hicho mwaka 2010/2011. Sehemu ya mitambo Pemba iliyafanyiwa matengenezo jumla ya magari 45 ikiwa ni upungufu kwa asilimia 73 ikilinganishwa na gari 156 zilizotengenezwa katika kipindi kama hicho 2010/2011.

Mhe. Spika**,** katika mwaka wa fedha 2011/12 Idara ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 280,600,000 na kutumia jumla ya Tsh 370,000,000 kwa kazi za kawaida.
Hadi Machi 2012, Idara ilikusanya jumla ya Tsh 224,299,500 sawa na asilimia 80 na iliingiziwa jumla ya Tsh 320,307,550 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 87 ya makadirio.

Malengo kwa Mwaka 2012/2013
Mhe. Spika**,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Idara itachukua hatua mbali mbali za kuimarisha usalama barabarani zikiwemo kuendelea kuwapatia elimu watumiaji wa barabara, na kuimarisha ukaguzi wa vyombo vya moto. Aidha, hatua zitachukuliwa za kuhakikisha kuwa Karakana Kuu ya Unguja na Sehemu ya mitambo Pemba zinaimarishwa kwa kupatiwa vifaa na wafanyakazi wenye ujuzi na teknolojia ya kisasa ya vyombo vya moto.

Mhe. Spika**,** kwa mwaka 2012/2013 Idara ya Usafiri na Leseni inatarajia kukusanya jumla ya Tsh 346,000,000 na inaombewa jumla ya Tsh 591,700,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

SEKTA YA USAFIRI WA ANGA
Mhe. Spika**,** Sekta ya Usafiri wa Anga ina majukumu ya kusimamia huduma za Usafiri wa Anga, kuimarisha usalama wa ndege, abiria na mizigo. Majukumu haya yanatekelezwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa mashirikiano ya pamoja na taasisi mbali mbali za Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania na sekta binafsi.

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar
Mhe. Spika**,** Baraza lako Tukufu katika mwezi Julai 2011 lilitunga Sheria Namb. 8 ya mwaka 2011 iliyoanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na Sheria Namb. 9 ya mwaka 2011 ya usimamizi wa viwanja vya ndege kwa maudhui ya kuimarisha huduma za usafiri wa anga Zanzibar.
Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaratibu na kusimamia maendeleo ya usafiri wa Anga Zanzibar pamoja na uendeshaji wa viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/12 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetekeleza kazi mbali mbali za kawaida za kuhudumia ndege, abiria na mizigo. Viwanja vya ndege vya Unguja na Pemba vimehudumia jumla ya ndege 39,997 ikilinganishwa na ndege 35,033 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho cha 2010/2011 ikiwa ni ongezeko la asilimia 14. Kati ya ndege hizo, ndege 34,086 zilihudumiwa katika kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume na ndege 5,911 zilihudumiwa katika kiwanja cha Pemba (Kiambatanisho Nam.6 a).

Mhe. Spika, Idadi ya abiria waliohudumiwa katika viwanja vya ndege vya Zanzibar ilikuwa ni 619,417 kuanzia mwezi Julai 2011 hadi Machi 2012 ikilinganishwa na abiria 510,942 waliohudumiwa katika kipindi kilichopita ikiwa ni ongezeko la asilimia 21. (Kiambatanisho Nam.6 b).

Kati ya abiria hao, abiria 574,382 walihudumiwa katika Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume na abiria 45,035 walihudumiwa katika Kiwanja cha Pemba. Aidha, abiria waliopita (*transit*) wamefikia 70,897. Takwimu hizo zinaonyesha kwamba kumekuwepo na ongezeko la idadi ya ndege na abiria waliohudumiwa ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka 2010/2011. Hii inatokana na kuimarika kwa miundombinu ya kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Abeid Amani Karume na kuimarika kwa sekta ya utalii na biashara ambapo watalii wengi wameendelea kuja hapa nchini kwa kutumia Usafiri wa Anga.

Mhe. Spika, Kwa upande wa mizigo (*freight*) jumla ya kilogramu 669,000 zilihudumiwa katika viwanja vyetu vya ndege vya Unguja na Pemba ikilinganishwa na kilogramu 560,804 zilizohudumiwa kipindi kilichopita.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Mamlaka ilipangiwa kukusanya jumla ya Tsh 1,210,410,000 na kutumia jumla ya Tsh 806,000,000 kwa kazi za kawaida.

Malengo ya Mamlaka kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2012/13 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaendelea kuimarisha huduma mbali mbali katika viwanja vyetu vya ndege kukidhi mahitaji ya watumiaji na matakwa ya kitaifa na kimataifa ya Usafiri wa Anga.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2012 Mamlaka ya viwanja vya ndege imekusanya jumla ya Tsh 1,694,444,560.95 sawa na asilimia 140 ya makadirio. Mapato haya yamekusanywa kutokana na ada za utuaji ndege kiwanjani (*Landing Fees*) kodi za ofisi (*Rents*) na mapato mengineyo na imeingiziwa jumla ya Tsh 1,514,053,329 kwa ajili ya matumizi ya kazi za kawaida sawa na asilimia 188. Ongezeko hili la makusanyo na matumizi limetokana na mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji viwanja vya ndege Zanzibar.

Mhe. Spika, Kwa upande wa kazi za maendeleo Wizara kupitia Mamlaka ya viwanja vya ndege ilipanga kutekeleza miradi 4 kwa mwaka wa fedha 2011/2012. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

i) Uendelezaji ujenzi wa Uzio

Mhe. Spika, Mradi huu unalengo la kujenga uzio wenye urefu wa km 6. Hadi kufikia mwezi Machi, 2012 jumla ya km 1.12 za uzio zimeshajengwa sawa na asilimia 19 ya lengo.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara inakusudia kuendeleza mradi huu kupitia mradi wa ujenzi wa maegesho na utanuzi wa njia ya kupitia ndege.

ii) Ujenzi wa Jengo Jipya la Abiria (*Terminal building*)

Mhe. Spika, Mradi huu una lengo la kujenga jengo jipya la abiria, maegesho ya ndege, maegesho ya magari pamoja na jengo la mitambo (*service building*) na uwekaji wa vifaa mbali mbali katika kiwanja cha kimataifa cha Abeid Amani Karume. Mradi huu unagharamiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kupitia Benki ya Exim ya China na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Mchango wa Serikali kwa mradi huu ulifanikiwa vizuri na hadi kufikia mwezi Machi 2012, jumla ya Tsh 1,495,467,949 sawa na asilimia 99 ya makadirio zilipatikana. Aidha, mkandarasi amekamilisha kazi za ujenzi wa "*steel structure*" ya jengo hilo na ujenzi wa "*structure*" ya jengo la vifaa na zana (*machine room*).

Mhe. Spika, Utekelezaji wa mradi huu ulikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwemo mapungufu katika mkataba wa ujenzi, mabadiliko ya usanifu wa jengo la abiria na mabadiliko ya mikonga ya kuhudumia ndege (*aerobridge*). Changamoto nyingine ni uhaba wa nafasi katika baadhi ya maeneo ya kutolea huduma katika jengo hilo.

Mhe. Spika, katika kukabiliana na changamoto hizo Wizara tayari imeshakubaliana na Mkandarasi kufanya mabadiliko ya usanifu wa baadhi ya maeneo ya jengo hilo pamoja na mikonga ya kuhudumia ndege kutoka daraja la D hadi daraja la E litakalowezesha kuhudumia ndege kubwa zaidi zinazotumia kiwanja chetu.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara inakusudia kuendeleza mradi huu na jumla ya Tsh 500 milioni zinaombwa kutoka Serikalini.

iii) Ujenzi wa maegesho na njia ya kupitia ndege (*extension of apron and taxiway*) uwanja wa ndege wa Kimataifa.

Mhe. Spika, Mradi huu unaendelea na una lengo la ujenzi wa sehemu ya maegesho (*apron*) na kuimarisha njia za kupitia ndege (*taxiways*) katika Kiwanja cha Ndege cha kimataifa cha Abeid Amani Karume. Mradi huu unagharamiwa na Benki ya Dunia na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wizara hivi sasa imetiliana saini mkataba wa ujenzi na usimamizi wa mradi huo. Kazi za ujenzi zinategemewa kuanza mapema mwezi Julai 2012. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, hakuna fedha zilizotolewa kutoka Serikalini.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara inakusudia kuendeleza mradi huu na jumla ya Tsh 500 milioni zinaombwa kutoka Serikalini.

iv) Uimarishaji wa huduma za Viwanja vya ndege

Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na unalengo la kufanya ukarabati wa mitambo ya umeme, matengenezo ya jengo la sasa la abiria, kujenga ofisi

za mashirika ya ndege, mikahawa na majengo mengine kwa huduma mbali mbali. Hadi kufikia mwezi Machi 2012, hakuna fedha zilizopatikana kutekeleza mradi huu.

v) Uimarishaji wa huduma za Uwanja wa ndege wa Pemba.

Mhe. Spika, mradi huu unagharamiwa na Serikali ya Mapinduzi pekee una lengo la kuweka taa katika barabara ya kurukia na kutulia ndege na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa huduma mbalimbali katika kiwanja hicho.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara inaomba jumla ya Tsh 900 million kugharamia mradi huu.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Wizara inakusudia kuendelea na utekelezaji wa miradi mbali mbali kwenye sekta ya usafiri wa Anga. Jumla ya Tsh 1.9 bilioni zinaombwa kutoka Serikalini.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Mamlaka imepanga kukusanya jumla ya Tsh 3,060,072,000 na kutumia jumla ya Tsh 3,060,072,000 kwa matumizi ya kazi za kawaida.

Mashirika ya Muungano (Sekta ya Usafiri wa Anga)

Mhe. Spika, Katika kipindi cha 2011/2012 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuratibu shughuli za usafiri na Mawasiliano kwa kushirikiana na mashirika ya Muungano yaliyopo Zanzibar, kama vile Mamlaka ya Usafiri wa Anga (*TCAA*) na Mamlaka ya Hali ya hewa Tanzania (*TMA*).

Mchango wa Sekta Binafsi

Mhe. Spika, sekta binafsi imeendelea kutoa mchango mkubwa katika kusadia juhudi za Serikali za kuendeleza na kuimarisha usafiri wa anga hapa Zanzibar. Mchango huu unaisaidia nchi yetu kwa kuingiza mapato yatokanayo na kodi mbali mbali na kutoa ajira kwa wananchi. Kwa mwaka 2011/2012 Kampuni mbali mbali za ndege za ndani na nje ya nchi ziliendelea kutoa huduma katika viwanja vyetu vya ndege. (Kiambatanisho Nam. 7).

VI. SEKTA YA USAFIRI WA BAHARINI

Mhe. Spika, Kama nilivyotangulia kusema kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya usafiri wa baharini Zanzibar kwa kuweka miundombinu ya bandari, kusimamia utoaji wa huduma za usafiri na kulinda usalama wa watu na mali zao pamoja na mazingira ya baharini yasichafuliwe. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini *ZMA*, Shirika la Bandari Zanzibar *ZPC*, Shirika la Meli, pamoja na kampuni za watu binafsi ambazo zimewekeza katika sekta hii.

MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Usafiri Baharini ina jukumu la kusimamia usalama wa vyombo, abiria na mizigo na biashara ya usafiri kwa ujumla wake katika biashara ya usafiri baharini. Majukumu hayo ni pamoja na kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni na vibali kwa wafanyabiashara wa shughuli zote za bahari Zanzibar, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ya baharini, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia nk.

Aidha, Mamlaka hudhibiti safari za baharini, uchunguzi wa ajali baharini, usimamizi wa maslahi ya mabaharia, pamoja na utoaji wa hati za kuongeza muda leseni za mabaharia.

Vile vile, Mamlaka inasimamia utekelezaji wa kanuni ya kimataifa ya ulinzi wa meli na bandari (*ISPS Code*) na uratibu wa shughuli za utafutaji na uokozi kwa maeneo ya Zanzibar.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012 Mamlaka ilisajili meli 24 zenye uzito wa jumla GRT 16,465.36 kwa usajili wa ndani (*Tanzania Zanzibar Registry*) na meli 100 zenye uzito wa jumla GRT 335,313.16 kwa usajili wa nje (*Tanzania Zanzibar International Registry*) (kiambatisho Nam. 8a).

Aidha, vyombo vidogo vidogo 27 vyenye uzito wa jumla ya tani 525 GT vilisajiliwa.
Katika kipindi hicho Mamlaka ilitoa vitabu vya ubaharia (*Discharge books*) 86 na vitambulisho vya kimataifa vya ubaharia (*seafarer's book*) 28.

Mhe. Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2012 Mamlaka ilikusanya jumla ya Tsh 375,813,964 sawa na asilimia 230 ya makadirio na imetumia jumla ya Tsh 104,000,000 sawa na asilimia 81 ya makadirio iliyopangiwa.

Malengo ya Mamlaka kwa mwaka 2012/2013.

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2012/13 Mamlaka imepanga kuunda muundo mpya utakaoendana na kazi zake pamoja na kuajiri wafanyakazi wenye taaluma, kuandaa kanuni zilizobaki za usafiri baharini pamoja na kuweka taratibu za kudhibiti mashirika na taasisi zinazotoa huduma baharini. Hatua hizo ni pamoja na kuwapatia leseni waendeshaji wa huduma hizo na kudhibiti shughuli zao. Aidha, Mamlaka itaimarisha ukusanyaji mapato kwa kupitia vyanzo vyake mbalimbali na kuongeza matawi mengine ya usajili wa kimataifa.

Vile vile, ushirikiano mzuri na imara baina ya Mamlaka na wamiliki wa vyombo vya usafiri baharini pamoja na washirika wengine wa masuala ya usafiri baharini utaendelea kuimarishwa.

Mhe. Spika, Mamlaka katika mwaka 2012/2013 itaanza kujitegemea na imejidhatiti kuimarisha usalama wa vyombo vya bahari Zanzibar kwa kuweka bajeti ya kutosha ya ununuzi wa vifaa vya ukaguzi wa meli, ufuatiliaji wa bandari zote za Zanzibar na kuhakikisha upatikanaji wa nyenzo za utendaji.

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Mamlaka imepanga kukusanya jumla ya Tsh. 1,856,301,381 na kutumia jumla ya Tsh 1,704,224,536 kwa kazi za kawaida.

SHIRIKA LA BANDARI

Mhe. Spika, Shirika la Bandari lina jukumu la kutoa huduma za uingizaji na utoaji meli katika bandari za Unguja na Pemba, ufungaji na ufunguaji wa meli kwenye gati, uangalizi wa alama za kuongozea usafiri wa meli (minara na maboya), uteremshaji na upakiaji wa bidhaa kwenye meli pamoja na vyombo vyengine vya usafiri wa baharini na usimamizi wa usalama ndani ya maeneo ya bandari hizo.

Vile vile, Shirika linawajibu wa kuhifadhi mizigo na utunzaji wake katika Bandari pamoja na kuvifanyia matengenezo madogo madogo vyombo mbali mbali vya usafiri wa Baharini kwa kutumia Karakana yake kuu ya Malindi.

Mhe. Spika, Shirika la Bandari limepewa jukumu la kuzitambua na kuzihakiki Bandari Bubu ziliopo Zanzibar ili kuandaa utaratibu mzuri wa udhibiti wake katika usafirishaji wa bidhaa mbali mbali kwa mashirikiano na taasisi nyengine.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, Shirika liliendelea na kazi zake za kutoa huduma mbali mbali. (Kiambatanisho Nam 9).

Kazi za kiufundi:

Mhe. Spika, Shirika katika kipindi hicho limefanya kazi mbali mbali za kiufundi zikiwemo matengenezo ya vyombo vya baharini vinavyomilikiwa na Shirika lenyewe, pamoja na vyombo vya kampuni binafsi vilivyohitaji huduma za Chelezo. Aidha, Karakana Kuu ya Shirika ilifanya kazi za uchongaji wa vipuri kwa ajili ya vitendea kazi vya bandarini pamoja na baharini. Shirika limeweza kuyafanyia matengenezo maboya yake manne kwa kuyawekea taa mpya zinazotumia nishati ya jua.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012, Shirika limetekeleza miradi ifuatayo:-

(i) Uimarishaji wa Bandari ya Mkoani

Mhe. Spika, Mradi huu ulikuwa na lengo la kuiimarisha Bandari ya Mkoani kwa kurekebisha eneo lililodidimia katikati ya gati. Hadi kufikia mwezi Machi 2012 matengenezo ya Gati ya Mkoani yamekamilika.

(ii) Ununuzi wa Tishali la Kuegesha Vyombo vya Abiria

Mhe. Spika, Lengo la mradi huu ni ununuzi wa tishali jipya la kuegeshea vyombo vya abiria ambalo litatumika wakati tishali kubwa linapokuwa Chelezoni.Tishali hilo limeshanunuliwa na linatumika.

Mhe. Spika, Mbali ya miradi niliyoitaja pia Shirika limeweza kununua kreni mbili kwa ajili ya kufanyia kazi bandarini na linakamilisha taratibu za kununua taa zinazotumia nishati ya jua kwa ajili ya minara ya kuongozea meli.

Mapato na Matumizi

Mhe. Spika, Katika kipindi cha 2011/2012 Shirika lilikadiria kukusanya jumla ya Tsh 9.3 bilioni kutokana na mauzo ya huduma zake mbali mbali. Hadi kufikia mwisho wa mwezi wa Machi, 2012 jumla ya Tsh 9.045 bilioni zilikusanywa ikiwa ni sawa na asilimia 97 ya makadirio. Aidha, jumla ya Tsh 5.5 bilioni zilitumika kwa kazi za kawaida ambapo ni sawa na asilima 84.6 ya makadirio ya matumizi kwa kipindi hicho.

Malengo ya Shirika kwa mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, Shirika la Bandari litaendelea kutekeleza majukumu yake kama kawaida.
Kadhalika, Shirika katika kipindi hicho linategemea kutoa huduma bandarini Unguja na Pemba, kwa kuhudumia jumla ya meli 175 za kigeni zenye uzito (GRT) wa tani 2.3milioni, Meli za ndani zipatazo 4,900 na majahazi 1,500 pamoja na kuhudumia tani 100,000 za mzigo mchanganyiko pamoja na makontena 52,000.

Mhe. Spika, Kwa upande wa miradi ya maendeleo Shirika linatarajia kuendelea na uimarishaji wa huduma na raslimali zake kwa kukamilisha miradi iliyoanzishwa mwaka wa Fedha unaomalizika ikiwa ni pamoja na ununuzi wa taa zinazotumia nishati ya jua kwa minara na maboya Unguja na Pemba na matengenezo ya sehemu ya kiungo cha gati ya Mkoani ilioathirika kutokana na mawimbi ya vyombo wakati wa kufunga gati.

Mhe. Spika, katika kipindi cha 2012/2013 Shirika limekadiria kukusanya jumla ya Tsh 16.5 bilioni katika kutekeleza malengo hayo Shirika limepanga kutumia jumla ya Tsh 9.72 bilioni kwa kazi za kawaida.

SHIRIKA LA MELI

Mhe. Spika, Shirika la Meli lina jukumu la kuendesha meli zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kutoa huduma za uwakala wa meli za kigeni zinazoingia katika bandari za Zanzibar. Kwa sasa Shirika linaendesha meli mbili za MT Ukombozi na MV Maendeleo na lina matawi mawili katika bandari za Dar es salaam na Pemba.

Mapato na Matumizi ya Shirika.

Mhe. Spika, Katika kipindi cha Julai 2011 hadi Machi 2012 Shirika lilikukusanya jumla ya Tsh 2.5 bilioni sawa na asilimia 81 ya makisio ya mwaka 2011/2012 na kufanya matumizi ya jumla ya Tsh 2.36 bilioni sawa na asilimia 84 ya makisio ya mwaka 2011/2012.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza katika bajeti yangu ya mwaka 2011/2012 Shirika bado linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo uchakavu wa meli zake unaopelekea kuharibika kwa meli ya M.V Maendeleo mara kwa mara, kuongezeka gharama za matengenezo na uagiziaji vipuri pamoja na upandaji wa bei za mafuta, uhaba wa wataalamu wa uendeshaji wa meli katika fani ya uhandisi na unahodha wa meli na idadi kubwa ya wafanyakazi wa Shirika.

Malengo ya Shirika kwa mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013 Shirika limepanga kujiimarisha zaidi katika utekelezaji wa majukumu yake kwa kutekeleza mambo yafuatayo:-

- Kuimarisha tawi la Dar es salaam kwa kulipatia leseni ya uwakala wa meli za kigeni zinazoingia katika bandari ya Dar es Salaam na leseni ya kutoa mizigo bandarini.
- Kusomesha wafanyakazi wa Shirika kozi za muda mfupi kwenye fani za uhandisi na unahodha wa meli.
- Kuajiri wafanyakazi wenye elimu ya IT, Masoko na kuajiri kwa mkataba wahandisi kwa kazi za melini.
- Kushirikiana na Serikali katika juhudi za upatikanaji wa meli mpya ya abiria ya Serikali kwa ajili ya kuhudumia usafiri baina ya visiwa vya Unguja na Pemba.
- Kukamilisha sheria ya Shirika la Meli na Uwakala kwa lengo la kuimarisha Shirika kujiendesha kibiashara.

Mhe. Spika, Katika mwaka wa fedha 2012/2013 Shirika linategemea kukusanya jumla ya Tsh 4.3 bilioni kutokana na vianzio vyake vya mapato na kutumia jumla ya Tsh 3.5 bilioni.

Mchango wa Sekta Binafsi katika Sekta ya Usafiri Baharini

Mhe. Spika, Sekta binafsi imeendelea kuchangia maendeleo ya sekta ya usafiri wa baharini hapa nchini. Hivi sasa kuna zaidi ya kampuni binafsi 24 ambazo zimewekeza katika usafirishaji wa abiria na mizigo kati ya Unguja na Pemba na baina ya bandari za visiwa hivi na bandari nyengine katika mwambao wa Afrika Mashariki. (Kiambatisho Nam. 8b**)**

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inatambua na kuthamini mchango wa sekta binafsi katika kujenga uchumi wa nchi yetu kwa kutoa huduma bora zenye kufanikisha sekta nyengine kiuchumi na kijamii, kuchangia pato la taifa na kutoa ajira kwa wananchi.

VII. SEKTA YA MAWASILIANO.

Mhe. Spika, Sekta ya mawasiliano inatoa mchango mkubwa katika kuimarisha huduma za kiuchumi na kijamii na inajumuisha utoaji wa huduma za mawasiliano kwa njia za posta, simu na huduma za teknolojia ya habari.

Idara ya Mawasiliano.

Mhe. Spika, Idara ina jukumu la kusimamia huduma za mawasiliano na masuala ya taasisi za mawasiliano za Serikali ya Muungano ziliopo Zanzibar. Idara pia ina jukumu la kuratibu na

kusimamia uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano na kudhibiti matumizi na utoaji wa huduma za teknolojia ya habari (IT).

Mhe. Spika, kwa mwaka 2011/2012 Idara iliendelea kutekeleza majukumu yake kama kawaida ikiwemo kutayarisha sera ya teknolojia ya habari na mawasiliano, kutoa ushauri na muongozo katika uwekaji wa miundombinu ya mawasiliano kama vile mkonga wa taifa, ujenzi wa minara ya simu, mabadiliko ya teknolojia na uwekaji wa anuani za makaazi ya simbo za Posta. Aidha, Idara ilifanya ukaguzi na usimamizi wa utumiaji wa minara ikiwemo ya simu na internet. Katika kipindi hicho jumla ya minara 28 kutoka makampuni mbali mbali yakiwemo Zantel, Airtel, Tigo, Vodacom, TTCL, na Chuchu FM ilikaguliwa na hatimae kupewa hati.

Malengo kwa Mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara itaendelea na utekelezaji wa malengo ya kuratibu na kufuatilia masuala ya sekta ya mawasiliano hapa Zanzibar, kuandaa sheria, kanuni na mpango mkakati wa matumizi ya teknolojia ya habari. Idara itakamilisha Sera ya Teknolojia na Habari na Mawasiliano, (ICT).Vile vile, kwa kushirikiana na wadau wengine Idara itaratibu zoezi la uwekaji wa Simbo za Posta (*Postal Code*) pamoja na kutoa elimu kwa wananchi na taasisi za umma juu ya matumizi na uhifadhi wa miundombinu ya mawasiliano.

Mhe. Spika, Kwa mwaka 2011/2012, Idara ilipangiwa kutumia jumla ya Tsh 103,000,000 na hadi Machi 2012 fedha iliyoingiziwa ni Tsh 67,000,000 sawa na asilimia 65 ya makadirio.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 Idara inaombewa jumla ya Tsh 175,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida.

Kampuni ya Zantel.

Mhe. Spika, Kampuni ya Zantel imeanzishwa hapa Zanzibar na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina hisa ya asilimia 18. Kampuni hiyo inatoa huduma za simu za mkononi Tanzania na inaendelea kuimarisha huduma zake kwa wateja kwa kuongeza vituo vya huduma Zanzibar. Mwaka 2011 Zantel imeongeza vituo kutoka 80 mpaka kufikia vituo 130, pia imeweka mtandao wa 3G katika minara 75 hapa unguja ambao unawawezesha wananchi kupata mawasiliano ya internet kupitia simu zao kwa kasi sana. Zantel imeanzisha huduma za teknolojia ya 3G ili kuwapatia wakaazi wa Zanzibar huduma bora na za kasi za data na internet na kutekeleza ahadi yake iliyoitoa mwaka jana.

Mhe. Spika, Katika mwaka 2011/2012 Kampuni ya Zantel imeendelea kushikilia rikodi yake ya kuwa mchangiaji nambari moja wa mapato kwa kulipa kodi mbali mbali Serikalini. Aidha, kampuni hii imechangia katika shughuli mbali mbali za kijamii. Zantel ni kampuni mojawapo ya simu ya kibinafsi inayoendelea kutoa ajira kwa wananchi wa Zanzibar ambapo mwaka jana imezindua kituo cha huduma kwa wateja kilichotoa ajira kwa vijana wasiopungua 75 hapa Zanzibar.

Taasisi za Muungano (Sekta ya Mawasiliano)

Mhe. Spika, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2011/2012 Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano itaendelea kuratibu masuala ya mawasiliano kwa kushirikiana na taasisi za Muungano zinazotoa huduma za mawasiliano, simu na posta zilizopo Zanzibar. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), Shirika la simu Tanzania (*TTCL*) na Shirika la Posta Tanzania (*TPC*).

Mhe. Spika, Napenda kuchukua nafasi hii kuzipongeza kwa dhati taasisi za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo hushirikiana kwa karibu zaidi na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Nachukua fursa hii kuziomba tuendeleze ushirikiano huo hasa kwa taasisi zilizopo chini ya Wizara za Uchukuzi, Ujenzi, Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia za SMT. Uhusiano na ushirikiano huo umesaidia sana kuzipatia ufumbuzi changamoto tulizokabiliana nazo.

Maombi ya fedha kwa mwaka 2012/2013

Mhe. Spika, kwa madhumuni ya kuiwezesha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kutekeleza majukumu yake na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii, naomba kutoa hoja kwamba, Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya Tsh 15.061 Bilioni kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kati ya fedha hizo, Tsh 5.111 bilioni kwa kazi za kawaida na Tsh 9.95 Billioni kwa kazi za maendeleo.

Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu kuruhusu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kukusanya mapato ya jumla ya Tsh 394,500,000 kutokana na vianzio mbalimbali vilivyomo ndani ya Wizara hii.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwako na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu na ustahamilivu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Ni matumaini yangu kwamba Baraza lako Tukufu litatoa mchango ambao utaisaidia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kutatua matatizo ambayo ilikumbana nayo katika kipindi cha mwaka 2011/2012 ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, Mafanikio ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ambayo nimeyaeleza katika hotuba hii ni matokeo ya ushirikiano wa wadau mbali mbali wa ndani na nje. Napenda kuchukuwa fursa hii kuzitambua, kuzishukuru na kuzipongeza Nchi, Jumuiya na taasisi zifuatazo kwa misaada yao muhimu katika kuendeleza sekta mbali mbali za Wizara hii.

Nchi hizo ni Jamhuri ya Watu wa China, Norway, Libya, Japan, Saudi Arabia, India, Misri, Marekani, Ujerumani, Oman na UAE. Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na Benki ya Dunia (*World Bank*), China Exim Bank, Jumuiya ya Nchi za Ulaya (*EU*), Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (*BADEA*), Mfuko wa Umoja wa

Maendeleo ya Kimataifa wa Nchi zinazosafirisha mafuta kwa wingi ulimwenguni (*OPEC Fund*), *SAUDI* Fund, *NORAD*, Mashirika ya Umoja wa Mataifa ya *UNDP, IMO, ICAO*.

Mhe. Spika, kadhalika, nachukua fursa hii kuyashukuru makampuni ya kibiashara ya kimataifa ambayo yamechangia katika sekta ya usafirishaji ikiwemo Oman Air, Kenya Airways, Ethiopian Airline, Air Uganda na kwa upande wa usafiri baharini *Maersk, MSC, UAFL, Emirates Shipping* na *CMA CGM* pamoja na Kampuni ya *DANAOS* inayotoa ajira ya Ubaharia kwa wananchi wa Zanzibar.

Wamiliki na watendaji wa vyombo vya usafiri baharini, usafiri wa nchi kavu (daladala) na anga tunawashukuru na kuwapongeza kwa dhati kwa mchango wao.

Mhe. Spika, niruhusu tena kupitia kwako kuwashukuru na kuwapongeza wamiliki wa ndani wa vyombo vya usafiri wa Bahari, Nchi kavu na Anga ambao wanashirikiana na Serikali katika kutoa huduma za usafiri.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Serikali na kwa kupitia Baraza lako Tukufu naomba kutoa wito kuwaomba wadau tuliowataja hapo juu na wengineo kuendelea kushirikiana na serikali katika kutoa huduma za usafirishaji.

Mhe. Spika, napenda nimalizie kwa kuwapongeza wafanyakazi wote wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kila siku licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali. Kadhalika, napenda kuwapongeza wafanyakazi wote walioshiriki katika maandalizi ya hotuba hii kwa kazi nzuri waliyoifanya, nawatakia utekelezaji mwema wa majukumu yao.

Mhe. Spika, shukurani za pekee zimwendee Mpiga Chapa Mkuu pamoja na Wafanyakazi wote wa Kiwanda cha Upigaji Chapa kwa kufanikisha uchapaji wa vitabu mbali mbali pamoja na uchapaji wa hotuba hii, na wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha utekelezaji wa kazi za wizara hii.

Naomba kuwashukuru wafanyakazi wote wa Taasisi za Serikali na Watu Binafsi pamoja na wananchi kwa jumla kwa kufanikisha kazi za maendeleo ya nchi yetu. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kufanya kazi kwa uaminifu, nidhamu na moyo wa kuipenda nchi yao. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hotuba yangu hii haitokamilika kama sijatoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi wa jimbo langu la Ole kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa na kunivumilia pale ninapokuwa mbali nao kutokana na majukumu mengine ya kitaifa yanayonikabili. Nakiri kwamba imani na heshima yao kwangu ni kubwa na ya kipekee. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwa madhumuni ya kuiwezesha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kutekeleza majukumu yake na malengo yaliyoelezwa katika hotuba hii. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu liidhinishe matumizi ya jumla ya shilingi bilioni 15.061 kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kati ya fedha hizi shilingi bilioni 5.11 kwa kazi za kawaida na shilingi bilioni 9.5 kwa kazi za maendeleo.

Aidha naliomba Baraza lako Tukufu kuruhusu Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 394 milioni 500 elfu kutokana na vianzio mbali mbali vilivyomo ndani ya wizara hii.

KASMA	**MATUMIZI HALISI 2010/2011**	MAKADIRIO 2011/2012	FEDHA HALISI Julai2011-Machi 2012			**%**	**Makisio 2012/2013**
			Mishahara/ Maposho	**Matumizi Mengineyo**	**Jumla**	**%**	
0301PEMBA	1,100,418,000	1,065,000,000	700,447,277	179,519,000	879,966,277	83	1,356,800,000
0401 MIPANGO	748,118,000	150,000,000	-	91,000,000	91,000,000	61	250,000,000
0501 MERITIME	-	128,000,000	-	104,000,000	104,000,000	81	-
0601 ANGA	763,418,000	806,000,000	480,000,000	1,034,053,329	1,514,053,329	187	-
0701 UUB	1,070,683,000	1,004,000,000	753,095,055	113,000,000	866,095,055	86	1,458,500,000
0801 LESENI	384,363,000	370,000,000	183,307,550	137,000,000	320,307,550	87	591,700,000
0901 UENDESHAJI	-	632,000,000	469,833,500	210,773,000	680,606,500	108	1,279,000,000
0100MAWASILIANO	-	103,000,000	-	67,000,000	67,000,000	65	175,000,000
JUMLA					**4,523,028,711**		

	4,067,000,000	**4,258,000,000**	**2,586,683,382**	**1,936,345,329**		106	**5,111,000,000**

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki. *(Makofi)*

KIAMBATANISHO NAM. 1
SEHEMU A

MUHUTASARI WA MAKADIRIO YA FEDHA KWA KAZI ZA KAWAIDA, MAENDELEO NA MAPATO KWA KIPINDI CHA JULAI 2010 HADI MACHI 2011 NA MAKISIO YA MWAKA 2012/2013

SEHEMU B.
MAPATO

KASMA	**MAPATO HALISI 2010/2011**	**MAKADIRIO 2011/2012**	**FEDHA ZILIKUSANYWA JULY-MACHI 2011/2012**	**ASILIMIA %**	**MAKISIO 2012/2013**
0301 PEMBA	100,032,007	98,980,000	87,628,623	89	42,500,000
0401 MIPANGO	87,100,408	-	-	-	-
0501 MARITIME	-	163,000,000	375,813,914	230	
0601 ANGA	1,350,513,435	1,210,410,000	1,694,444,561	140	-
0701 UUB	1,700,000	5,000,000	3,200,000	64	6,000,000
0801 LESENI	309,729,500	280,600,000	224,299,500	80	346,000,000
JUMLA	**1,849,075,350**	**1,757,990,000**	**2,385,386,648**	**136**	**394,500,000**

SEHEMU C
KAZI ZA MAENDELEO

KASMA	MATUMIZI HALISI 2010/2011	MAKADIRIO 2011/2012	FEDHA ZILIZOINGIZWA JULY-MACHI 2011/2012	ASILIMIA %	MAKISIO 2012/2013
0301 PEMBA	1,800,000,000	3,630,000,000	2,947,116,918	81.2	4,950,000,000
0401 MIPANGO	100,000,000	-	-	-	-
0601 ANGA	3,300,000,000	3,800,000,000	1,785,875,902	47.0	1,900,000,000
0701 UUB	3,900,000,000	1,957,598,000	1,602,999,263	81.9	3,100,000,000
JUMLA	**9,100,000,000**	**9,387,598,000**	**6,335,992,083**	**67.5**	**9,950,000,000**

KIAMBATANISHO Nam.2
WAFANYAKAZI WALIOPATA MAFUNZO KWA KIPINDI CHA 2011/2012

S/N	AINA YA MAFUNZO	MAHALA	MUDA (MIAKA)	IDADI
1.	Short course	Zanzibar		8
2.	Certificate in Record Management	Zanzibar	1	4
3.	Certificate in Human Resource	Zanzibar	1	2
4.	Diploma in Records Management	Zanzibar	2	3
5.	Diploma in Public Administration	Zanzibar	2	1
6.	Diploma in Human Resource	Zanzibar	2	4
7.	Diploma in Statistics	Dar es Salaam	2	1
8.	Diploma in Accountancy	Dodoma	2	2
9.	Diploma in Auto Body Repair	Zanzibar	2	1
10.	Bachelor of Science in Information, communications Technology.	Zanzibar	5	3
11.	Bachelor of Art in Economics	Zanzibar	3	1
12.	Bachelor of Art in Social Science	Dar es salaam	3	1
13.	Bachelor of Science in Engineering	Dar es salaam	3	1
14.	Master in International Transport and logistics Management	Misri	2	3
15.	Master of Arts in Economics	China	3	1
16.	Master in Public Administration	India	2	1

23.	Master in Transport Management.	DSM	2	1
17.	Certificate in Procurement	Zanzibar	1	1
19.	Diploma in Human Resource	Dar College	2	3
21.	Bachelor of Arts	Zanzibar	3	1
22.	Bachelor of Science in Engineering	Mbeya	3	1
				43

KIAMBATANISHO Na. 3A
BARABARA ZILIZOFANYIWA MATENGENEZO KUPITIA FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA 2011/12
A. UNGUJA
Matengenezo ya kawaida (routine maintenance)
Matengenezo haya yanajumuisha kazi za udhibiti wa majani, usafi wa mitaro, usafi wa culvert na barabara, utunzaji wa alama na michoro, uzibaji wa mashimo kwa barabara za lami na za kifusi. Barabara zilizofanyyiwa matengenezo ni:-

S/N	BARABARA	KAZI ILIYOFANYWA
1.	Bububu –Mndo, Kwanyanya – Mkanyageni, Mwera meli 6-Mfenesini	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance)
2.	Kitundu – Ndagaa, Koani – Machui – Kitumba, Kidimni- Kitope	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance)
3.	Pongwe –Matemwe, Tunguu – Upenja, Mkwajuni-Nungwi, Mkwajuni- Mtemwe	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance)
4.	Kinyasini-Kiwengwa, Kipilipili-Pongwe, Mahonda –Donge – Mkokotoni	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance)
5	Mahonda-Kinyasini-Mkokotoni,Njia nne-Bambi, Dunga - Chwaka	
5.	Jozani-Charawe-Ukongoroni	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance)
6.	Mazizini – Fumba, Paje- Michamvi, Kitogani –Paje	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance)
7.	Tunguu – Makunduchi, Tangi la maji- Mtende, Paje-Makunduchi, Unguja ukuu- Kaebona,Kibuteni-Kizimkazi.	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance)

B. PEMBA

S/N	BARABARA	KAZI ILIYOFANYWA
1.	Ole-Konde,Chake-Wesha,Chanjaani-Mkoani,Chake – Wete,Konde-Ngezi, Chanjaani-Macho manne,Mbuguani-Mkoani Port.	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance)
2.	Ole-Kengeja/Ole-Vitongoji,Kilindini-Micheweni,Mkoani-Ng'ombeni-Skuli,Mkoani-Makombeni,Bogoa-Michenzani	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance).
3.	Mkanyageni-Shidi,Kijangwani-Birkau,Mtambile-Mwambe,Mtambile-Kangani	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance)
4.	Chake – Wete, Chake – Wesha, Chanjaani – U/Ndege, Bogoa – Michenzani, Mbuguani – Mkoani Port, Konde –	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance).

	Ngezi, Kilindini – Micheweni, Machomanne – Vitongoji	
5.	Wesha – Mkumbuu, Konde – Msuka, Bwagamoyo – Kele na Ole – Konde.	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance)
6.	Chwale-Mzambarau Takao	Matengenezo ya kawaida (Routine maintenance)

Matengenezo ya muda maalumu (Periodic Maintenance)

S/N	BARABARA	KAZI ILIYOFANYWA
1	Mwanakwerekwe-Nyumba mbili-Mpendae-Nyumba mbili-Soko la Mchina –Mbuyu mnene (Unguja)	Imejengwa kwa kiwango cha lami
2	Kiashange-Kijini-Muyuni,Kijitoupele-Nyarugusu (Unguja)	Kiwango cha kifusi
3	Kinazini-Malindi (Unguja)	Imejengwa kwa kiwango cha lami
4	Weni-Wete, Ikulu- Chake Street (Pemba)	Imejengwa kwa kiwango cha lami

Matengenezo ya Sehemu Korofi (Spot improvements)

S/N	BARABARA	KAZI ILIYOFANYWA
1	Bububu-Mahonda (sehemu ya kihinani na Polisi Mfenesini) (Unguja)	Imejengwa kwa kiwango cha kifusi
2	Ole-Konde (Pemba)	Imejengwa kwa kiwango cha kifusi

Matengenezo ya Madaraja/Kalvati na mitaro ya Maji.

S/N	BARABARA	KAZI ILIYOFANYWA
1	Mwanakwerekwe-Kiembesamaki (Unguja)	Ujenzi wa mtaro
2	Kitundu-Ndagaa (Unguja)	Ujenzi wa kalvati
3	Ole-Konde	Ujenzi wa mtaro

Matengenezo ya dharura (Emergency).

S/N	BARABARA	KAZI ILIYOFANYWA
1	Kiboje mabonde ya Mpunga, Bungi ndani,barabara ya mnazi mmoja-Uwanja wa ndege eneo la kilimani, Mikunguni-M/Njugu,kwa pweza-Kwa alimsha,Magereza eneo la kilimani na barabaraya makadara-Kwa Abas Hussein (Unguja)	Matengenezo ya dharura kuziba viraka,kujenga kwa kifusi n.k
2	Ujenzi wa makalvati ya Gombani na barabara ya Finya-Kicha (Pemba)	Ujenzi wa makalvati

KIAMBATANISHO NAMB. 3B

BARABARA ZITAKAZOFANYIWA MATENGENEZO KUPTIA FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA 2012/2013

A UNGUJA

S/N	**BARABARA**	Target (km)
1	Bububu - Mndo	3.937
2	Kwanyanya-Mkanyageni	3.076
3	Regezamwendo-Mfenesini	14.272
4	Kitundu-Ndagaa	5.5
5	Amani -Dunga	12.743
6	Koani - Machui - Kitumba	5.5
7	Kidimni- Kitope	19
8	Pongwe - Matemwe	20.4
9	Kinyasini - Tunguu	26.757
10	Mkwajuni - Nungwi	19
11	Upenja - Kiwengwa	8.313
12	Kipilipilini - Pongwe	14
13	Mahonda - D/Mkokotoni	13.519
14	Njianne - Bambi	6.5
15	Mfenesini-Bumbwini	11.821
16	Kinazini - Bububu	7
17	Bububu - Mahonda	21
18	Mahonda-K/Mkokotoni	15
19	Mazizini - Fumba	17.823
20	Kitogani - Paje	11.601
21	Paje - Michamvi	17
22	Mnazimmoja - U/ndege	3
23	Mazizini-Chukwani/U/ndege	9
JUMLA		**285.762**

C. MATENGENEZO YA SEHEMU KOROFI		**ANNUAL ESTIMATES**
	BARABARA	Target km
1	Mtegani-Mtende (Earth works)	0.3
2	Upenja - Kiwengwa (earth works)	1.3
3	Ndagaa - Kitope (Earth works)	0.6

4	Kwamchina mwanzo/jang'ombe jctn improvement (m2)	
5	Mwanakwerekwe - Tunguu mwisho (earth works)	0.5
JUMLA		**2.7**
	MATENGENEZO YA MUDA MAALUM	**MAKISIO**
	BARABARA	Target km
1	Kinazini - Malindi (Kerbs, walkways/drifts)	1.00
2	Kivunge - Mkokotoni (Earth works)	4.00
3	Mkwajuni - Mshelishelini (Earth works)	2.00
4	Malindi jct - Bwawani Hotel (Earth works)	0.27
JUMLA		**7.27**

!

	MADARAJA/KALVATI	
		ANNUAL ESTIMATES
		Target No
1	Bububu - Mahonda road	20
2	Matengenezo ya kalvati	6
3	Kiongele Kalvati No2.	1
4	Bububu-Mndo (Kidichi)	1
5	Kinazini-Bububu (kalvati mpya Mshelishelini)	2
JUMLA		**30**

F	**MITARO YA MAJI**	
	BARABARA	**ANNUAL ESTIMATES**
		Target km
1	Bububu - Mfenesini (Kihinani)- stone pitching	1.8
2	Magereza-Kilimani juu+Migombani	0.36
3	Kilimani-Znz Airport Road	1

4	Mkwajuni - Nungwi	0.5
5	Bububu-Mndo	2
6	Mitre drain excecavation at Bububu/Kijichi (Bububu junction)	0.3
7	M/kwerekwe- K/samaki drainage	2
8	Regezamwendo-Mndo	7
JUMLA		**14.96**
	KAZI ZINAZOHUSIANA NA USALAMA BARABARANI	**ANNUAL ESTIMATES**
		Target [km]/No
1	Speed Bump in Numbers	6
2	Road Marking in kilometers	5
3	Road Sign	15
4	Painting round about (M/kwerekwe)	1

B - PEMBA
MATENGENEZO YA KAWAIDA

SN	**BARABARA**	ANNUAL ESTIMATES
		Target km
1	Ole – Konde	38
2	Madenjani - M/Takao	5.5
3	Chajaani - Mbuguani(Mkoani)	28
4	Mtuhaliwa - Chokocho	8.8
5	Machomane - Vitongoji	7
6	Chanjaani - U/Ndege	5.5
7	Chake Chake - Wesha	8
8	Mtambile - Kangani	6.4
9	Chanjamjawiri - Tundauwa	11.0
10	Chanjaani - Pujini	5.0

11	Kenya - Chambani	3.2
12	Mtambile - Mwambe	9.4
13	Mizingani - Wambaa	9.4
14	Chake Chake - Wete	30
15	Konde - Kiuyu cha Manda	3.5
16	Chanjaani - M/Manne	4
17	Mbuguani - Mkoani Port	2
18	Kilindini - Micheweni	6
14	Mkoani - Ngo'mbeni school	0.5
15	Mkoani - Makombeni	5
16	Bogoa - Michenzani	3
17	Mkanyageni - Shidi	2.2
	JUMLA	**201.40**

UZIBAJI VIRAKA

SN	BARABARA	MAKISIO Target m^2
1	Chake - Chake - Wete	600.00
2	Ole - Konde	200.00
3	Kilindini - Micheweni	150.00
4	Madenjani - M/Takao	300.00
5	Chake - Chake - Mkoani	650.00
6	Konde - Kiuyu cha Manda	150.00
7	Chanjaani - M/Manne	150.00
8	Chanjaani - U/Ndege	120.00
9	M/Manne - Vitongoji	100.00
10	Mtuhaliwa - Chokocho	100.00

11	Mkoani - Makombeni	100.00
	JUMLA	**2,620**

MATENGENEZO YA KAWAIDA (UN PAVED)

SN	BARABARA	MAKISIO Target km
1	M/Kwale - Pembeni	2.30
2	Gombeume - Hindi - jojo	2.00
3	Wawi - Vikunguni	6.40
4	Kukuu - Kangani	2.00
5	Micheweni - Kiuyu	6.20
6	Shidi - Mwambani	1.00
7	Penjewani - M/Kiuyu	2.30
8	Ole - Vitongoji	7.00
9	Kijangwani - Birikau	3.00
10	Micheweni - Sh/Mjini	1.90
	JUMLA	**34.10**

MATENGENEZO YA MUDA MAALUM (UN PAVED)

SN	BARABARA	ANNUAL ESTIMATES Target km
1	Finya - Kicha	6.40

2	Wesha - Mkumbuu	4.00
3	Msitu wa Ngezi	1.00
4	Kiuyu kwa Manda - Ngezi Makangale	2.00
5	Wawi - Mgogoni	2.00
6	Matangini - Kilindi	1.70
	JUMLA	**17.10**
B	**MATENGENEZO YA KOROFI (PAVED)**	
SN	BARABARA	MAKISIO Target km
1	Chanjaani Mbuguani	0.30
2	Chake - Wesha	0.90
	JUMLA	1.20
C	**MATENGENEZO YA MUDA MAALUM (PAVED)**	
SN	BARABARA	MAKISIO Target km
1	M/Manne - Melitano	2.00
2	Ole - Konde	4.00
	JUMLA	**6.0**
D	**MATENGENEZO YA MADARAJA NA KALVATI**	
SN	BARABARA	MAKISIO Target No
1	Chake - Mkoani	

		1.00
2	Finya - Kicha	5.00
3	Matangini - Kilindi	2.00
E	**(BOX CULVERTS)**	
SN	BARABARA	ANNUAL ESTIMATES Target No
1	M/Mmoja - Shangafu	1Box
2	Mkia wa Ng'ombe	1Box
F	**MITARO YA MAJI**	
SN	BARABARA	MAKISIO Target km
2	Ole - Konde	0.40
3	Chake - Mkoani	0.40
	JUMLA	**0.80**
G	**Road sign**	
SN	BARABARA	MAKISIO No
1	Ole - Konde	20.00
2	Chanjaani - Mbuguani	20.00
3	Madenjani - M/Takao	10.00
	JUMLA	50.00
H	**Line Marking**	
		km Target

1	Chanjaani - Mbuguani	2.5
	JUMLA	**2.50**

KIAMBATANISHO Na. 4
MPANGO WA MAENDELEO 2012/2013

NA.	**UJENZI**	**UREFU (km)**	**MFADHILI**	**BAJETI YA SMZ (Tsh)**	**RUZUKU/ MKOPO (Tsh)**
1.	**Ujenzi wa barabara 3 za Pemba** Wete – Gando (13.6) Wete – Konde (15.1) Wete – Chake (24)	52.7	SMZ/BADEA /SAUD FUND	3,500,000,000.	7,290,000,000
2	**Ujenzi wa barabara 3 za Pemba** Wete – Chake *(mradi mpaya)*	24	SMZ/BADEA /SAUD FUND	900,000,000	5,000,000,000
3.	Ujenzi wa barabara ya Mgagadu-Kiwani	7.6	SMZ	400,000,000	
4.	Ujenzi wa barabara ya Mkanyageni - Kangani	6.5	SMZ	100,000,000	-
5.	Ujenzi wa barabara ya Ole – Kengeja	3.5	SMZ /OPEC	50,000,000	-
6	Upembuzi yakinifu wa barabara za vijijini-Unguja (Matemwe – Muyuni,Kichwele-Pangeni,Njia nne-Umbuji-Uroa,Jozani-Charawe-Ukongoroni-Bwejuu naMkwajuni-Kijini) *(mradi mpaya)*	48	AfDB	-	1,900,000,000
7.	**Ujenzi wa barabara kuu za Unguja** Amani – Dunga (12.7) Mfenesini – Bumbwini (13.2)	25.9	SMZ/ AfDB	1,500,000,000	-
8	Barabara zinazoingia mjini		Benki ya Dunia	50,000,000	-

9	Ujenzi wa barabara 3 Vijijini -Unguja Barabara ya Koani – Jumbi (6.3) Barabara ya Kizimbani – Kiboje (7.2) Barabara ya Jendele – Cheju - Kaebona (11.7)	25.2	SMZ/BADEA	1, 500,000,000	8,000,000,000
10	Ujenzi wa barabara za vijijiniKaskazini Pemba (Mzambarauni-Pandani – Finya,Bahanasa-Daya-Mtambwe,Chwale-Kojani naKipangani-Kangagani)	35	SMZ/MCC	50,000,000	23,015,000,000
	JUMLA NDOGO			**8,050,000,000**	**45,205,000,000**
11	Ujenzi na utanuzi wa maegesho na njia za kupitia ndege.		SMZ/WB	500,000,000	40,000,000,000
12	Ujenzi wa jengo jipya la abiria A.AKIA		SMZ /EXIM CHINA	500,000,000	35,200,000,000
13	Uimarishaji huduma uwanja wa Pemba		SMZ	900,000,000	-
14	Mradi wa mabadiliko ya mfumo wa taasisi		AfDB		2,000,000,000
	JUMLA NDOGO			**1,900,000,000**	**77,200,000,000**
JUMLA KUU				**9,950,000,000**	**122,405,000,000**

KIAMBATANISHO Nam. 5 a
UKAGUZI WA VYOMBO VYA MOTO KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2011 HADI MACHI 2012

AINA YA VYOMBO	**IDADI YA VYOMBO VYA MOTO VILIVYOKAGULIWA**					
	UKAGUZI WA KAWAIDA		UKAGUZI WA SHAKA		UKAGUZI WA AJALI	
	UNGUJA	PEMBA	UNGUJA	PEMBA	UNGUJA	PEMBA
GARI	11,270	950	732	42	526	25
MOTOR	10,309	1,726	9	2	191	9

CYCLE						
JUMLA	**21,579**	**2,676**	**741**	**44**	**717**	**34**

Kiambatanisho Nam 5 b

TAKWIMU ZA WAOMBAJI WALIOJARIBIWA KUENDESHA VYOMBO VYA MOTO

AINA YA MADEREVA	**WALIOJARIBIWA KUENDESHA**			**WALIOFAULU KUENDESHA**			**WALIOFELI KUENDESHA**		
	Gari	M/cycle	Jumla	Gari	M/cycle	Jumla	Gari	M/cycle	**Jumla**
Unguja	2,890	1,397	4,287	2,176	1,154	3,330	711	246	**957**
Pemba	602	836	1,438	382	690	1,072	139	227	**366**
Jumla	**3,492**	**2,233**	**5,725**	**2,558**	**1,844**	**4,402**	**850**	**473**	**1,323**

KIAMBATANISHO Nam. 6 b

IDADI YA ABIRIA WALIOHUDUMIWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI 2011 HADI MACHI 2012

KIWANJA	**IDADI YA ABIRIA 2010/11**		**JUMLA**	**IDADI YA ABIRIA 2011/12**		**JUMLA**
	INTER	**DOMESTIC**		**INTER**	**DOMESTIC**	
UNGUJA	213,638	262,585	476,223	266,753	307,629	574,382
PEMBA	28	34,691	34,719	-	45,035	45,35
JUMLA	**213,666**	**297,276**	**510,942**	**266,753**	**45,035**	**619,417**

KIAMBATANISHO.7

KAMPUNI ZA NDEGE ZILIZOTUMIA KIWANJA CHA NDEGE CHA ABEID AMANI KARUME KWA MWAKA 2011/2012

S/NO	**JINA LA KAMPUNI**	**VITUO**	**NCHI**

			INAYOTOKA
1	Precision Air	Dar, Kilimanjaro, Mombasa, Nairobi	Tanzania
2	Coastal Travel	Zanzibar, Dar, Arusha	Tanzania
3	Zanair	Zanzibar Dar Arusha	Tanzania
4	Kenya Airways	Nairobi Dar	Kenya
5	Ethiopia airways	Addis-Ababa	Ethiopia
6	Air Uganda	Entebbe	Uganda
7	540 Aviation	Mombasa	Kenya
8	Blue panorama	Milan-Malpensa	Italy
9	Air Italy	Milan-Malpensa	Italy
10	Eurofly	Milan-Malpensa	Italy
11	Condor	Frankfut-Mombasa	Germany
12	Tui Airline	Brassoul	Belgium
13	Travel Service	Budapest	Hungary
14	Neos Air	Milan	Italy
15	Onetime Air	Johannesburg	South Africa
16	Oman Air	Muscat	Oman

KIAMBATANISHO Nam. 8a

ORODHA YA MELI ZILIZOSAJILIWA CHINI YA USAJILI WA NDANI (LOCAL REGISTRY) KIPINDI CHA JULAI 2011 – MACHI 2012

NAM	JINA LA MELI	UZITO (GT)
1	bn 103	1282
2	b 09	1282
3	svs dampier	244.25
4	svs monck	244.25
5	svs swallow	54.89
6	svs squirrel	48.87
7	svs raleigh	169
8	svs gilbert	84
9	tuna best	545
10	venesa	3421
11	condore	943
12	raptor (ex penton salvor)	991
13	svs morgan	863
14	comarco 272	1246.52
15	comarco 271	1246.52
16	buraq 111	248.19
17	svs cochrane	439
18	svs hawkins	168
19	hercules	705.87
20	faraday	45.00
21	svs kidd	136

22	titan	144
23	sinbad	375
24	cso centurion	1539
	J U M L A	**16,465.36**

MELI ZILIZOSAJILIWA CHINI YA USAJILI WA "TANZANIA ZANZIBAR INTERNATIONAL REGISTER OF SHIIPPING" KIPINDI CHA JULAI 2011 – MARCH 2012

NAM	JINA LA MELI	UZITO (GT)
1	lady jana ex lady jawa	9896
2	burcini	1860
3	khalil ex anna 1	43.7
4	waleed ex anna 2	365
5	chance	2580
6	gulf river	1939
7	mohammed r.m	3010
8	retaj	1404
9	fastrex	1946
10	ocean star ii	481.65
11	stark	3960
12	nawal iii	2222
13	amal o	3046
14	amal star	5202
15	malak trader	1892
16	just mariam	2970
17	sea mate	70
18	onega	3988
19	el hussain	7533
20	mto	794
21	shaanxi henan 3	1047
22	venus	5930
23	al-husseiny	289.56
24	silver	297
25	kayla ex sea lion	235
26	hala b	1623
27	huang he 22	656
28	wutaishan anhui 44	1016
29	al- hussein i	94.67
30	abu yasser ii	281
31	blue rose	2717
32	gold star	2438

33	mohamad prince	4926
34	chalenger 2	117
35	afros	463
36	al safa	1918
37	apadana	487
38	maha -b	1770
39	italia	2265
40	venezia	2610
41	toma	71
42	maria f	2441
43	al zeina	2465
44	croatia	2319
45	spania	2265
46	thekkady	483
47	al naser	5976
48	thalassa	989
49	navistar	1841
50	ali-m	3345
51	ikarous	3676
52	dover 1	484
53	laquna	3754
54	armony	1690
55	mathew i	659
56	baiyanqdian	1884
57	mazaya iv	359.96
58	navisky	1997
59	med glory	2300
60	hesen moon	3080
61	lady sarah	1952
62	al batoul	1773
63	abs i	221
64	abs ii	224
65	al nibras	1649
66	bai shun	499
67	liberty	920
68	nadeen	9020
69	sibel j	2862
70	cpt.ahamad 1	2123
71	lady soso	1849
72	gulf city	1949
73	marzuk	2592
74	siraj	2356
75	seagull-k	4908
76	lady rasha	1777

77	Al marwa	652
78	Shaikh 1	160
79	Ali 1	150
80	contester m	2749
81	malmo	8328
82	amal neptune	3898
83	nura	298
84	siam varich	794
85	kj 6	288
86	med prince	4543
87	deema	121
88	al rabee	1494
89	audrey rose	197.62
90	barhom ii	1939
91	osman prince	10733
92	manouchehr 1	60
93	saba 2	375
94	salis	25391
95	tandis	27681
96	pardis	25391
97	armis	25391
98	parmis	25391
99	don juan	1220
100	caroline	2933
	JUMLA	**335,313.16**

Kiambatanisho 8b

S/No	**JINA LA KAMPUNI**
1.	Azam Marine Co. Ltd
2.	Coastal Fast Ferries
3.	Sea Star Co. Ltd
4.	JAK Enterprises Co. Ltd
5.	Al-Ghubra/Visiwani/Mkunazini Shipping Ent.
6.	Seven Seas Marine Services
7.	Fast Ferries Co. Ltd
8.	Sahara line Ltd/ MAS Shipping

9.	Zanzibar Shipping Corporation
10	Zanzibar Port Corporation
11	African Shipping corp. Ltd
12	Cecibell Securities Inc.
13	Haidery Fishstock Co. Ltd
14	Quest Marine
15	Hammy Distributors and Services Ltd
16	Seagull Sea Transport Co Ltd.
17	Omar Sharif Nour
18	Tanga Petroleum Co. Ltd
19	Global Marine Services Ltd
20	Zams Traders Ltd
21	Feisal Said Noor and Mohammed Adanor
22	Nazir Lodhi
23	Marine Transport Co. Ltd
24	Kenya Marine Contractors (EPZ) Ltd.

KIAMBATANISHO Nam. 9

HUDUMA ZA MELI

S/N	AINA YA MELI (CHOMBO)	KIPINDI		ONGEZEKO/ PUNGUZO %
		JULAI 2010 – MACHI 2011	JULAI 2011-MACHI 2012	
1.	Meli za Nje/Uzito wake (GRT)	134/ 1,250,018.49	116/1,489,109	-13.40/+19.3
2.	Meli za ndani	4,245	4,181	-1.5
3.	Mzigo wa Majahazi	2,261	2,285	+1.50

HUDUMA ZA MIZIGO

S/N	AINA YA MZIGO/ABIRIA	KIPINDI		ONGEZEKO/ PUNGUZO %
		JULAI 2010 – MACHI 2011	JULAI 2011-MACHI 2012	
1.	Mzigo mchanganyiko	91,528	61,494	- 33
2.	Makontena	26,842	30,683	+14.3
3.	Mafuta	38,261	32,638	-15
4.	Mzigo wa majahazi	40,279	75,079	+86.4
5.	Abiria wa ndani	1,575,392	1,595,189	+1.26
6.	Abiria wa kigeni	2,075	824	-60.29

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na kuungwa mkono, ikimaanisha sasa ijadiliwe. Nimshukuru Mhe. Waziri kwa kuanzia na hotuba nzuri hii ambayo amewasilisha kwa kiasi cha muda wa saa 1:15. *(Makofi)*

Sasa tumsikilize Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, Mhe. karibu. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, naomba kusoma Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii adhimu, kutanguliza shukrani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia kwa mara nyengine tena kukutana hapa katika Baraza letu, tukiwa katika hali ya uzima na afya, kwa lengo la kuwatumikia wananchi wetu na taifa kwa ujumla.

Aidha napenda nikushukuru wewe binafsi Mhe. Spika, kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, ili kutoa maoni ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2012/2013.

Mhe. Spika, kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi napenda kutoa mkono wa pole kwa wananchi wote wa Zanzibar pamoja na Tanzania kwa ujumla kufuatia ajali ya kuzama kwa meli ya M.V *Skagit* iliyotokea tarehe 18/07/2012 karibu na Kisiwa cha Chumbe. Tunamuomba Mweyezi Mungu awalaze pema peponi wale wote waliopoteza maisha yao na awape nafuu

majeruhi wote walionusurika katika ajali hiyo, tunawaomba wananchi wawe na moyo wa subira katika kipindi hichi kigumu.

Mhe. Spika, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwa mashirikiano mazuri na ya dhati waliyoipatia Kamati yetu wakati wa kuipitia bajeti ya wizara hii, lakini pia hata katika kazi za kawaida za Kamati hii wakati wa ufuatiliaji shughuli za kawaida za wizara, nathubutu kusema tumepata mashirikiano ya kutosha. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nachukuwa nafasi hii kumpongeza kwa dhati aliyekuwa Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii Mhe. Rashid Seif Suleiman kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kufuatia kujiuzulu kwa Mheshimiwa Hamad Masoud Hamad aliyekuwa Waziri wa Wizara hii. *(Makofi)*

Sambamba na pongezi hizo Kamati yetu inamasikitiko makubwa sana kumkosa Mhe. Rashid Seif Suleiman katika Kamati yetu kutokana na mchango wake mkubwa aliokuwa akitoa katika shughuli za Kamati. Hata hivyo tuna matumaini kwamba Mhe. Rashid Seif Suleiman ataendeleza mashirikiano hayo kwa Kamati kitika wadhifa wake huu, hasa kwa kuzingatia kwamba wizara anayoitumikia ni miongoni mwa Wizara mbili ambazo Kamati yetu inazifanyia kazi. *(Makofi)*

Aidha nachukuwa nafasi hii kumkaribisha Mhe. Marina Joel Thomas kwa kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, Kamati imefarajika sana kupata Mjumbe mpya amabae tunaamini ataisaidia sana Kamati katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mhe. Spika, sina budi pia kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, pamoja na Makatibu wa Kamati hii kwa kuonesha ushirikiano mzuri katika kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa ya kusimamia utekelezaji wa Wizara mbili zinazosimamiwa na Kamati hii. Mhe. Spika, naomba niweke msisitizo wa shukrani zangu kwa kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk - Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
3. Mhe. Subeit Khamis Faki - Mjumbe
4. Mhe. Salma Mussa Bilali - Mjumbe
5. Mhe. Shawana Bukhet Hassan - Mjumbe
6. Mhe. Marina Joel Thomas - Mjumbe
7. Ndg. Aziza Wazir Kheir - Katibu
8. Ndg. Abdalla Ali Shauri - Katibu

Mhe. Spika, baada ya kutoa shukran za dhati, sasa naomba uniruhusu nianze kutoa Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka fedha 2012/2013 kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na mambo mengine ndio iliyokabidhiwa jukumu la kuendeleza miundombinu na utoaji wa huduma za usafiri na mawasiliano ya nchi yetu, kupitia idara na taasisi mbali mbali zilizo chini ya wizara hii.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:

Mhe. Spika, Idara ya Mipango Sera na Utafiti ina jukumu la kupanga, kuratibu, kusimamia na kutathmini utekelezaji wa sera, mipango na utafiti wa sekta ya usafiri na mawasiliano. Kamati imefarajika kupokea taarifa ya Idara hii kwamba imeendelea na mchakato wa matayarisho ya Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Barabara, Sheria ya Shirika la Meli na Uwakala pamoja na Uandaaji wa Sera ya Teknologia ya Habari na Mawasiliano. Nimatarajio ya Kamati kwamba katika mwaka wa fedha 2012/2013 Idara itakamilisha kazi hizo, ili kuongeza ufanisi na kuweka muongozo sahihi wa uendeshaji wa shughuli za taasisi hizo.

IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI:

Mhe. Spika, Idara ya Utumishi na Uendeshaji ni Idara muhimu katika kusimimia uendeshaji wa kazi za ofisi na maslahi ya wafanyakazi, ikiwa ni pamoja na kuwapatia mafunzo ya aina mbali mbali watumishi wake. Mhe. Spika, Kamati yetu inasikitika kupokea malalamiko kwamba baadhi ya wafanya kazi wa ngazi za chini hasa wale ambao wameajiriwa zamani hawajanufaika na marekesbisho ya viwango vipya vya mishahara.

Hali hii inajitokeza kutokana na utaratibu uliotumika *"formular"* katika kuwapandishia mishahara watumishi wa Serikali, utaratibu ambao umezingatia zaidi viwango vya elimu. Hivyo baadhi ya wafanya kazi wa zamani licha ya uzowefu wao wa kazi wa muda mrefu hawakuweza kunufaika na mabadiliko hayo.

Mhe. Spika, kwa kuwa suala hili linaratibiwa na Wizara ya Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tunaiomba Serikali kupitia Wizara hii kuangalia tena utaratibu huo, ambao umetumika katika kuweka viwango vya mishahara, ili kuondoa malalamiko na kuweza kumnufaisha kila mfanyakazi.

Mhe. Spika, Kamati yetu inasisitiza kuwa ni muhimu kwa Idara hii kuhakikisha inawapatia wafanyakazi wake maelekezo ya kazi zao "*Job descriptions"* pamoja na kuhakikisha wafanyakazi wanafanya kazi kwa mujibu wa mpango mkakati wa Wizara *"Action Plan"*. Kwa kuwa imekuwa ni kawaida kwa watumishi wengi wa Serikali kufanya kazi kwa mazowea tu badala ya kujiwekea mipango sahihi ambayo itaweza kuwapa muongozo wa kuweza kujitathmini katika kutekeleza kazi zao za kila siku.

Aidha Kamati yetu inasisitiza umuhimu wa wafanyakazi kuwa wabunifu katika kutekeleza kazi zao, badala ya kusubiri kazi zije kwenye meza ziwatume.

IDARA YA UJENZI NA UTUNZAJI BARABARA:

Mhe. Spika, Idara hii ni muhimu sana katika kurahisisha shughuli za kiuchumi na kijamii kwa wananchi na taifa kwa ujumla. Kamati yetu inapenda kuipongeza kwa dhati Idrara hii kwa jitihada zao wanazozichukuwa katika kuhakikisha suala la miundombinu ya barabara linakuwa katika hali nzuri, kwa kusimamaia ujenzi pamoja na utengenezaji wa barabara za mjini na vijijini.

Aidha Kamati yetu inaiomba Idara iendelee na jitihada zake za kuziimarisha barabara zetu, ili kero zinazowakabili wananchi katika sekta ya usafiri wa barabara ziondoke na hatimae kuwasaidia wananchi katika shughuli zao kiuchumi na kijamii.

Mhe. Spika, Kamati yetu inatoa wito kwa Serikali kupitia Idara hii kuhakikisha inasimimia vyema mikataba ya Makampuni ya Ujenzi wa Barabara na kuhakikisha kwamba barabara hizo zinajengwa na kukamilika kwa wakati na kwa kiwango kinachostahiki, ili ziweze kudumu kwa muda mrefu.

Pia Kamati yetu inasisitiza suala la ujenzi wa mitaro ya pembeni mwa barabara lazima lizingatiwe, kwakuwa mitaro hiyo ni muhimu sana katika kuziweka barabara zetu katika kiwango bora na kuzifanya zidumu kwa muda mrefu.

Mhe. Spika, mara nyingi kumekuwa na malalamiko kwa wananchi ambao maeneo yao yanachimbwa vifusi kutolipwa fidia za mazao yao au wakati mwengine kulipwa kiasi kidogo sana cha fedha ambacho hakilingani na thamani ya eneo linalochukuliwa.

Sambamba na hilo pia kumekuwa na matatizo kwa baadhi ya makampuni hayo kuchimba vifusi kinyume na makubaliano, ambapo mara nyingi makampuni hayo huchimba vifusi kwa kina kirefu sana, hali ambayo husababisha uharibifu wa mazingira bila ya kuzingatia kufukia sehemu wanazochimba. Hivyo Kamati yetu inatoa wito kwa Serikali kupitia Idara hii kuhakikisha wanasimamia makubaliano yaliyomo kwenye mikataba ya wakandarasi hawa, ili kuona miradi hiyo haileti athari kwa wananchi.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine Kamati yetu inatowa wito kwa Serikali kuhakikisha inakamilisha mapema sehemu ya mchango wake wa fedha katika miradi ya ujenzi wa Barabara, kwa kuwa mara nyingi miradi huchelewa kukamilika kutokana na Serikali kuchelewa kutowa fedha, hali hii hupelekea kuzidi kwa gharama za ujenzi, lakini pia ni kuvunja mkataba wa makubaliano na wakandarasi hao.

Mhe. Spika, Kamati yetu pia inatowa wito kwa Idara hii kuzingatia mipango ya muda mrefu wakati inapojenga barabara kwa kuziwekea alama za pembezoni *“becon”* mwa barabara ambazo zitaonyesha mipaka ya eneo la barabara hali hii itasaidia kupunguza uvamizi wa ujenzi karibu na barabara hizo.

IDARA YA USAFIRI NA LESENI:

Mhe. Spika, Idara ya Usafiri na Leseni inajukumu zito la kuhakikisha usalama wa watumiaji wa barabara, ukaguzi wa vyombo vya moto, usimamizi wa mafunzo ya udereva na utoaji wa huduma za usafirishaji abiria na mizigo. Kuna kila sababu ya kuwepo kwa mashirikiano ya karibu kati ya idara hii na Jeshi la Polisi kutokana na ukweli kwamba shughuli za Idara hii kwa kiasi kikubwa zinategemea msaada wa jeshi la Polisi.

Mhe. Spika, Kamati yetu inasikitika na haijaridhishwa kabisa na hali ya Karakana Kuu ya Serikali, kwakuwa karakana hiyo haijaweza kutekeleza kazi zake za kuhudumia vyombo vya

serikali kama ilivyokusudiwa, miongoni mwa sababu za tatizo hilo ni uchakavu wa vifaa na uhaba wa wataalamu.

Hivyo kamati yetu inatowa wito kwa Serikali katika mwaka wa fedha 2012/2013 kuipa umuhimu Karakana hii ili iweze kutoa huduma kwa vyombo vya Serikali. Hali hii itasaidia kupunguzia mzigo mkubwa unaobebwa na Serikali wa gharama ya kutengeneza vyombo hivyo, lakini pia itasaidia kuviweka vyombo vya Serikali kuwa katika hali ya usalama zaidi iwapo vitatengenezwa katika Karakana ya Serikali.

Mhe. Spika, Kwa kuwa Idara hii ndiyo yenye jukumu la utoaji wa leseni za vyombo vya moto, kazi ambayo hivi sasa inafanywa na Bodi ya Ukusanyaji wa Mapato (*ZRB*). Kamati yetu inatoa wito kwa serikali kuangalia uwezekanao wa kulirejesha jukumu hilo kwa Idara ambayo kisheria ndiyo yenye mamlaka hiyo, pia itaisaidia Idara hii kuwa na nguvu ya kujiendesha kutokana na uwezo itakaopata kupitia ukusanyaji wa mapato.

Aidha Kamati yetu inatowa wito kwa Idara hii kuvifanyia ukaguzi vyombo vya serikali kama ambayo inavifanyia ukaguzi vyombo vya binafsi. Kwa upande mwengine Kamati yetu inatoa wito kwa Idara kuweka utaratibu mzuri wa ukaguzi wa Magari, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wananchi kwamba ukaguzi unaofanywa barabarani unawapatia usumbufu sana abiria kutokana na magari hayo kusimamishwa kwa muda mrefu bila kuzingatia hali na shughuli walizo nazo abiria hao. Hivyo Kamati inapendekeza ni vyema ukaguzi huo ukafanywa vituoni ambapo gari zinakuwa hazina abiria.

MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE:

Mhe. Spika, Kamati yetu inampongeza kwa dhati Mkurugenzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege pamoja na watendaji wake, kwa namna wanavyojitahidi kuleta mabadiliko katika Kiwanja cha Ndege cha *"Karume International Airport"* ili kiwe na hadhi ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na kutekeleza maelekezo na mapendekezo ya Kamati yetu ambayo imekuwa ikiyatowa kila inapotembelea eneo hilo kwa lengo la kuongeza ufanisi na ubora unaostahiki.

Mhe. Spika, kiwanja cha ndege ni sehemu muhimu sana kwa uchumi wa nchi lakini pia hata kwa kuweka taswira nzuri ya nchi, ikiwa kitakuwa katika hadhi inayokubalika kimataifa. Hivyo tuna kila sababu ya kuimarisha huduma za viwanja vyetu vya ndege ili viweze kutoa huduma za kiushindani na ambazo zinakubalika kimataifa.

Mhe. Spika, suala la usalama katika kiwanja cha ndege ni muhimu sana, Kamati yetu inapongeza juhudi zinazoendelea za kukizungushia uzio kiwanja cha *"Karume International Airport"*. Aidha, Kamati inatoa wito kwa Mamlaka kukamilisha ujenzi wa uzio huo sehemu iliyobakia, ikiwa ni pamoja na kulipia fidia wananchi walio bakia, ili kiwanja kiwe na usalama wa uhakika kwani hivi sasa baadhi ya wananchi hutumia maeneo ya ndani ya kiwanja hicho kwa shughuli zao binafsi.

Mhe. Spika, Kamati yetu imesikitishwa mno na hali ya uharibifu wa mazingira unaofanywa katika eneo la kiwanja hicho kwa kuchimbwa kifusi bila kuzingatia athari za kimazingira. Hivyo, Kamati inatoa wito kwa taasisi zinazohusika kushirikiana na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege

kudhibiti hali hii ikiwemo Idara ya Mazingira, tukiamini kwamba wananchi wanaochimba kifusi wamepewa kibali cha kufanya hivyo na mamlaka inayohusika na utoaji wa vibali vya uchimbaji kifusi.

Mhe. Spika, Kamati inaipongeza kwa dhati Serikali kupitia Wizara ya Miundombinu kwa hatua ya kuanzisha ujenzi wa jengo jipya la abiria *"Terminal II"* ambalo kimsingi likikamilika litaondosha usumbufu wa msongomano wa abiria pamoja na kukiweka kiwanja chetu katika haiba nzuri zaidi.

Jambo la msingi ambalo Kamati yetu inaisisitiza kwa Serikali kuwa makini katika kusimamia mradi huo ambao bilashaka utaligharimu taifa fedha nyingi. Hivyo, ni muhimu kuzingatia malengo ya muda mrefu katika ujenzi wa mradi huo na kuhakikisha kuwa ujenzi huo unakuwa katika kiwango kinachostahiki.

Mhe. Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa hivi sasa inakusanya baadhi ya mapato ikiwemo mapato ya utuaji ndege na kodi za majengo, sehemu kubwa ya mapato yatokanayo na *"service charges",* yanakwenda Serikalini.

Kwa kuwa imekuwa Mamlaka badala ya Idara, suala la kuipa nguvu mamlaka hii katika ukusanyaji wa mapato yanayopatikana viwanja vya ndege ni la msingi sana ili iweze kujiendeleza na kujitegemea kikamilifu kama ilivyo dhana ya Mamlaka. Hivyo tunaomba Serikali iipe Mamlaka hii uwezo zaidi wa kukusanya mapato.
Sambamba na hilo kwakuwa katika viwanja hivyo kuna taasisi nyengine za Serikali ambazo hazilipi kodi na ambazo zinakusanya mapato kama vile Idara ya Uhamiaji, na kwakuwa taasisi hizo zinatumia huduma za Mamlaka zinazotolewa kiwanjani hapo, ni vyema kwa taasisi hizo zikaanza kulipia kodi kwa Mamlaka ya Viwanja vya Bdege, ili kuipa uwezo zaidi Mamlaka katika ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba Kamati inatoa wito kwa Serikali kulipa uzito unaostahiki suala la kukiwekea taa za kuongozea ndege, kiwanja cha ndege cha '*Pemba Airport'* katika bajeti ya mwaka 2012/2013 kwakuwa tatizo hili limekuwa la muda mrefu bila ya kupatiwa ufumbuzi. Mhe. Spika, suala hili ni muhimu sana kwa usalama wa ndege zianazotua kiwanjani hapo.

Ikumbukwe kwamba taa za kuongezea ndege sio tu muhimu kuziwezesha ndege kutua wakati wa usiku lakini pia zinaweza kutumika hata katika hali ya dharura wakati hali ya hewa inapochafuka sana, zinaweza kutoa msaada mkubwa katika kuziongoza ndege kutua bila ya matatizo. Kamati inasisitiza tena kutekelezwa kwa suala hili kwani imechoka kupatiwa maandishi ya kutia moyo kuhusiana na suala hilo.

MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI:

Mhe. Spika, Kamati yetu imepokea taarifa kwamba katika bajeti ya mwaka 2012/2013 Mamlaka ya Usafiri Baharini, imeandaa mpango wa kujiimarisha kiutendaji ikiwemo suala la kununua vifaa vya kisasa katika kuhakikisha usalama wa vyombo na ufanisi wa kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha na kuijengea uwezo mamlaka hii, ili iweze kusimamia vyema ulinzi na usalama wa vyombo vya baharini hasa kwa kuzingatia matukio ambayo yamekuwa yakitokea mfululizo na kugharimu maisha ya watu wengi pamoja na mali nyingi ikiwemo ajali ya kuzama kwa M.V Fatihi, Mv. *Spice Islanders*, pamoja na M.V *Skagit* ambayo imetokea tarehe 18/07/2012.

Kwa upande mwengine Kamati yetu inatowa wito kwa Mamlka hii kuhakikisha kwamba wanaweka vyombo vya dharura vya uokozi *"Speed Boat"* ambazo zitaweza kutoa huduma za haraka za uokozi mara tu taarifa za hitilafu au kuzama kwa chombo zinapopatikana. Kwa kuwa kumekuwa na imani kwamba miongoni mwa sababu zinazopelekea kushindwa kuokolewa kwa abria wengi wakiwa hai ni kutokuwepo kwa vyombo maalum na vya uhakika vya uokozi ambayo vimewekwa tayari *"stand by"* kwa ajili ya shughuli hiyo.

Aidha, tunaiomba Mamlaka hii izidi kujitangaza, ili ieleweke shughuli zake inazozifanya kwakuwa hivi sasa wengi kati ya wananchi hawailewi vizuri Mamlaka hii pamoja na shughuli zake inazozifanya.

Mhe. Spika, tunaamini Tume iliyoundwa na Mhe. Rais kuchunguza ajali ya M.V *Skagit* itatekeleza kazi zake kwa uadilifu, pia tuna imani kwamba baada ya matokeo ya uchunguzi huo wale watakaobainika kuhusika katika kutokea kwa ajali hiyo kwa namna moja au nyengine kwa kushindwa kuwajibika au kwa kukiuka taratibu watachukuliwa hatua za kisheria.

SHIRIKA LA BANDARI:

Mhe. Spika, Kamati yetu inazitambua na kuzithamini juhudi zinazofanywa na Shirika la Bandari katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku za uingizaji na utoaji wa meli katika bandari zetu. Hata hivyo, uwezo wa Shirika hili ni mdogo ukilinganisha na Bandari za jirani kama vile Mombasa na Dar es Salaam. Uwezo wa bandari yetu kwa sasa ni kuhudumia meli moja tu ya mizigo kwa wakati mmoja kutokana na udogo wa bandari yetu na uhaba wa vifaa.

Licha ya changamoto hizo zinazowakabili Kamati inapenda kuupongeza kwa dhati uongozi wa Shirika la Bandari kwa jitihada zao wanazozifanya za kutoa na kupakia mizigo kwa haraka. Pia nalipongeza Shirika kwa kukamilisha ununuzi wa *"creane"* mbili za kubebea mizigo ikiwa ni sehemu ya mpango wake wa mradi wa ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi bandarini, bilashaka kupatikana kwa *"creane"* hizi kutasaidia kuharakisha uteremshaji na upakiaji wa mizigo kwenye meli.

Mhe. Spika, Kamati inaiomba Serikali kuharakisha mpango wa ujenzi wa bandari mpya ya Mpiga duri (Maruhubi) ili kuongeza uwezo wa Bandari yetu kuweza kuhudumia meli nyingi kwa wakati mmoja, na kuweza kuhimili ushindani wa kibishara, kwakuwa hivi sasa harakati za meli zimeongezeka sana, ni vyema na sisi tukaongeza uwezo wa bandari yetu kuhudumia meli hizo. Kutokana na kuchelewa kwetu huenda tukakosa soko la meli hizo na hatimae zikaamua kuhamia bandari nyengine za jirani, hali hii italeta athari kubwa kwa uchumi wa nchi yetu.

SHIRIKA LA MELI

Mhe. Spika, nchi yetu imekuwa na tatizo la muda mrefu la Serikali kutokuwa na meli ya uhakika kwa ajili ya kusafirishia abiria hususan usafiri baina ya kisiwa cha Pemba na Unguja, mara kwa mara tumekuwa tukisikia ama kushuhudia matatizo ya kuharibika ama kuzuiliwa kwa meli kutokana na ubovu wa meli hizo.

Mhe. Spika, Kamati yetu inapenda kumpongeza kwa dhati Mhe Rais wa Zanzibar kwa kuonesha kuguswa sana na ajali ya M.V Skagit, na kutowa agizo kwa Afisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kutafuta fedha katika bajeti ya mwaka 2012/2013 kwa ajili ya ununuzi wa meli ya abiria. Tunatarajia kwamba Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano watatekeleza vyema agizo hilo ili kusaidia kuliondoa tatizo hili. Kwa hakika wananchi wetu wamekuwa wakisumbuka sana kutokana na kutokuwepo kwa usafiri wa uhakika na wa kuaminika.

Aidha, Kamati yetu inatoa wito kwa Serikali wakati wa mchakato wa upatikanaji wa Meli, wazingatie aina ya meli hiyo isiwe ya kibiashara sana yaani *"too cormmacial"* badala yake iwe ya kihuduma zaidi yaani *"service oriented"* ambayo itaweza kukidhi huduma za usafiri kwa mujibu wa mazingira ya nchi yetu.

IDARA YA MAWASILIANO

Mhe. Spika, Sekta ya Mawasiliano ni sehemu moja muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi pamoja na kurahisisha shughuli za Kijamii kwa njia tofauti. Kamati imesikitishwa sana kuona harakati zinazoendelea nchini za uwekaji wa mkonga wa mawasiliano kwa ajili ya mradi wa *"E-government"* kwa kuchimbwa kando kando ya barabara wakati hou huo Serikali ikijuwa kwamba malengo yake ni kuzitanua barabara, ambapo mkonga huo utakuwa ndani ya sehemu ya barabara hizo. Kinachosikitisha zaidi ni kwamba taasisi zote mbili hizi yaani ya Idara ya Mawasiliano pamoja na Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara - UUB, zote zipo chini ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, sisi wajumbe wa Kamati kwa kuwa si wataalamu wa masuala hayo tungeweza kushawishika kusema kwamba kwa kitaalamu uwekaji wa nyaya hizo pembozoni mwa barabara inakubalika na hakuna athari inayoweza kutokea, lakini kinachotupa hofu ni kwamba tayari tumeshaanza kupokea malalamiko kutoka upande mmoja kuhusu nyaya hizo kuwekwa pembezoni mwa barabara, hali hii inaonesha kwamba pande mbili hizi hazikukaa pamoja zikakubaliana namna bora ya kulitekeleza suala hili. Sula la kujiuliza, Jee ikiwa taasisi mbili za Wizara moja zimeshindwa kuwa na mashirikiano, Vipi taasisi nyengine za Wizara mbili tofauti zitaweza kufanya kazi kwa mashirikiano?

Mhe. Spika, hali hii si ya kubeza kwani mara nyingi tunafeli na kupoteza fedha nyingi za umma katika kutekeleza miradi yetu kutokana na mipango mibovu tunayofanya, ingawa waswahili husema "*maji yakisha mwagika hayazoleki"* lakini bado tunayo nafasi ya kufikiria namna ya kupunguza athari inayoweza kutokea baadae kutokana na tatizo hili kwa taasisi zinazo husika kukaa pamoja na kulifikiria suala hili.

HITIMISHO

Mhe. Spika, Ili Wizara iweze kutekeleza malengo yake na kutoa huduma bora kwa wananchi, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu, waipokee, waichangie na baadae kuipitisha bajeti ya Wizara kwa mwaka 2012/2013 jumla ya T.sh 15.061 Bilioni, zikiwemo T.sh 5.111 Bilioni kwa kazi za kawaida na T.sh 9.95 Bilioni kwa kazi za maenedeleo.

Mhe. Spika, sasa napenda kutamka kwamba kwa niaba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Kojani, naiunga mkono hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2012/2013.
Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa kuniruhusu kuwa mtu wa kwanza leo kuchangia hotuba hii Mhe. Waziri wa Miundombinu. Bila ya kupoteza muda nataka nianze na ukurasa wa 19.

Mhe. Spika, ukurasa wa 19 naomba nizungumzie Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara. Mhe. Spika, Wizara hii ya Miundombinu kupitia Idara yake hii ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara ndiyo yenye jukumu ya kuwapatia wananchi huduma bora za usafiri wa barabara kwa kuendeleza ujenzi na utunzaji wa barabara. Hili ndio jukumu la Wizara hii kupitia Idara yake ya Ujenzi na Utunzaji wa barabara.

Katika hili kwanza nataka nioneshe masikitiko yangu kidogo kwa barabara ya Ole/Kengeja. Mheshimiwa mradi huu unatajwa miaka mingi. Kama utafanya *reference* kwenye vitabu vya bajeti si chini ya miaka minne sasa tunataja barabara hii. Lakini maendeleo ya mradi huu bado hayaridhishi kabisa. Sijui kuna usiri gani ndani ya barabara hii mpaka ikawa mpaka leo bado mradi huu haujafika hatua ya kuridhisha.

Barabara hii ni muhimu sana kwa sababu ni barabara inayowaunganisha Wapemba wa Kaskazini na Wa Kusini kupitia ukanda wa Mashariki, kwahali ambapo kuna dhiki kubwa sana ya barabara. Hata zile barabara ndogo ndogo zilizojengwa basi haziwezi kukidhi mahitaji ya wananchi wanaokaa ukanda huu wa Mashariki ya Kisiwa cha Pemba. Nilikuwa namuomba sana Mhe. Waziri atuletee maelezo yatakayowaridhisha wananchi wa maeneo haya. Maana yake mpaka leo mradi huu tumaambiwa, naomba nisome kidogo hapa, ukurasa wa 25 wa kitabu cha Mhe. Waziri naomba Mhe. Spika, uniruhusu ninukuu kidogo.

> "Kutokana na gharama za ujenzi kuwa kubwa kulingana na fedha zilizotengwa, Wizara inaendelea na mazungumzo na mfadhili wa mradi huo juu ya uwezekano wa kutumia mfumo wa nguvu kazi yaani (*labour base)* katika kutekeleza mradi huo, ambao utawezesha kujenga barabara yote kwa fedha ziliopo"

Yaani fedha ziliopo hazikutajwa lakini inaashiria kwamba fedha ni kidogo. Unataka kutumia mfumo zile za *feeder roads* 6 za Kusini Pemba.

Mhe. Spika, mimi si mtaalamu lakini barabara zile hazina maisha marefu na mimi kama Mwakilishi wa wananchi hata kama nawakilisha jimbo la Chonga lakini nawakilisha wananchi wote wa Zanzibar. Barabara hii ndefu sana ina kilomita 35, mimi sioni kama ni busara kutumia teknolojia ile isiyokuwa na uhakika, mimi naichukulia teknolojia ile mpaka leo kwa hapa kwetu

ni ya majaribio. Haidhuru Waziri aliyeondoka madarakani hivi karibuni aliitetea sana teknolojia ile. Lakini kwa ninavyoona maana zile barabara tayari zipo zimejengwa, na ninaziona zinavyoendelea kubomoka kila siku. Sidhani kama ni busara kutumia teknolojia ile, kujenga barabara hii ya kilomita 35, ni mradi mkubwa. Nilikuwa nadhani serikali ihangaike kutafuta pesa lakini wajenge barabara ile kwa lami ya kawaida, sio lami ile ya kupikwa kwa mikono ya wananchi.

Mhe. Spika, katika idara hii naomba pia niendelee kusikitika kwa sababu katika jimbo langu bado huduma hii ya barabara ni hafifu sana, hata kama tulipata huo mradi mmoja wa barabara inayotoka Tundauwa mpaka Pujini ya teknolojia hii ya kukoroga lami kwa mikono, lakini kuna vijiji vingi vyenye wakaazi wengi ambao kwa kweli hawana hata ile huduma ya barabara ya fusi katika jimbo langu.

Niseme ni bahati mbaya kila ninapochangia suala hili kwa kweli jawabu ninalolipata kwa kweli nakuwa siridhiki, lakini naichukulia ni jawabu nimepewa tu. Leo naomba sana wananchi wa Jimbo la Chonga wanisikie jawabu ambayo naipata kila mwaka kuhusu barabara zao. Vijiji vinavyohusika naomba nivitaje, kuna kijiji cha Mgelema, Ngomeni, ambayo Ngomeni ndio nyimbo yangu kila mwaka naiimba, Matale, Mtimbu, Kilindi, Mwachawa, Kibaridi na kadhalika, humu mote hamna huduma ya barabara. Lakini ninapoulizia suala hili huwa najibiwa kitaalamu. Naambiwa barabara inategemea kigezo cha *population* iliopo kwenye kijiji.

Mhe. Spika, naomba sana wananchi wa jimbo la Chonga wanisikie kwa hilo. Kwamba ikiwa watu wanaoishi katika kijiji hicho haifikii kwenye vigezo ambavyo vinatakiwa watu wajengewe barabara basi huko barabara haiwezi kupelekwa. Hiyo ndiyo jawabu ninayoipata. Mimi huwa najiuliza hivi kwani watu wakiwa wachache jamani hawana haki ya huduma, kama wafadhili hawataki serikali si ijipange. Kuna mfuko wa barabara ule unachangiwa na kila raia wa nchi hii, hata kama anakaa ndani ya mikarafuu peke yake lakini si anachangia. Kwa nini usitumike mfuko ule basi angalau kila mwaka ukanipatia kipande cha kilomita 3 tu kutoka mfuko wa barabara, si mtakuwa mmeshawasaidia wananchi wa jimbo la Chonga. Itafika siku itakuwa hawa wananchi wameshapata huduma.

Lakini ukisema hakuna uwezekano wala hakuna vigezo wananchi wanaendelea kuteseka. Hii hali itakwenda mpaka lini. Najionea aibu sana Mhe. Spika, kuwa ni Mwakilishi katika Baraza lako tukufu miaka 20 sasa napigania barabara hii na hakuna maendeleo yaliyofikiwa. Naona aibu sana na wala sina cha kuwambia wananchi wangu. Sasa naomba ndani ya barabara hizi nilizozitaja naomba sana Mhe. Waziri apange apangue na mfuko wake wa barabara lakini japo vipande viwili nivipate, hasa kipande cha barabara hii cha Matele. Maana hata ukiangalia ikiwa ni vigezo vya watu basi kutoka Changaweni kuelekea Matele kuna wakaazi pale hawapungui thalathini elfu, halafu unakuja kusema hawatimii kigezo, basi hicho kigezo ni watu wangapi hebu tuambiwe.

Mhe. Spika, nitakuwa mgumu kidogo kupitisha fungu la Idara hii kama sitoahidiwa angalau barabara zangu mbili zitatengenezwa. Hili naomba niliseme kabisa.

Halafu katika Idara hii naomba nikumbushe, niliwahi kuzungumza mara moja kwamba matuta yaliyowekwa katika barabara ya kutoka Mazizini kuja Mbweni, yale matuta hayafai na

hayawasaidii wananchi. Maana matuta yanawekwa kwa ajili ya kulinda usalama wa wananchi. Lakini matuta haya hayasaidii huu usalama wa wananchi wala hayamsaidii dereva. Maana yake nimeshawahi kuwashuhudia madereva wanapita kwa *speed* yao hiyo hiyo wanayoitaka wao wenyewe. Wanayachupa yale matuta wanakwenda zao na wala hawapunguzi mwendo. Sasa wanaumiza gari zao lakini na ule usalama unaokusudiwa haupatikani.

Niliwahi kutoa rai mara moja matuta yale bora yaondolewe yaweke matuta yale makubwa ambayo dereva hata afanye nini hathubutu kulipita kwa kasi. Nakumbuka Waziri akatoa ahadi kwamba anakusudia kuomba fedha kwa ajili ya kufanya marekebisho ya matuta yake. Lakini sijaona hizo fedha, kwa hivyo namuomba Waziri aliyekuwepo sasa hivi naomba akija anieleweshe vizuri.

Halafu kuna hichi kibarabara cha kutoka Baraza la Wawakilishi kwenda Uwanja wa Ndege. Hichi kibarabara ni hatari. Kibarabara hichi hakina matuta lakini kimejaa ma-*cross* mengi Mhe. Spika. Madereva wa sasa hivi wengi wao hawana busara, wanapita hichi kibarabara kwa *speed* kubwa. Kuna hatari siku moja tukaja tukashuhudia maafa. Naomba sana Idara hii iweke alama ya kuwataka madereva wapunguze mwendo, waweke *speed* maalum. Asiruhusiwe mtu kwenda *speed* zaidi ya hiyo. Ikiwezekana waweke tuta.

Mhe. Spika, halafu *round about* kwa Mchina, inafaa paangaliwe, pale pahali ni hatari sana. Pale hapana *round about* pana makutano ya njia zinapishana njia pale, lakini hapana *round about*. Unafika pahali unajiuliza hivyo mie nitapita vipi hapa huna hakika na maisha yako kama dereva, wala mpita njia kwa miguu. Kwa hivyo, mimi nilikuwa naomba sana Idara hii ifikirie kuweka *round about* pale angalau pawe na utaratibu wa gari kuweza kupita vizuri.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nataka niende kidogo Uwanja wa Ndege, hii nafikiri ni Idara ya Usafiri wa Anga. Uwanja wa Ndege uliokuwepo Pemba zamani tulikuwa tukiuita Karume Air Port, lakini sasa hivi nafikiri ina jina jengine ambalo wao wenyewe watapanga. Lakini kwa kifupi ule uwanja umedumaa, maendeleo ya uwanja ule bado hayaridhishi kabisa. Waheshimiwa Wajumbe tumepiga makelele muda mrefu sana kuhusu taa za uwanja ule. Nashukuru nimeona humu tufungue ukurasa wa 49 wameweka shilingi milioni 900 kwa ajili ya kuweka taa.

Mhe. Spika, lakini pamoja na kuweka taa ule uwanja unahitaji kuendelezwa, ile njia ya kurukia ndege, mazingira yaliyokuwepo pale ni machafu, jengo lile halitoshi kabisa. Hatujaona hasa mradi wowote pale. Tulisikia unatajwa tajwa nilikuwa nadhani kwenye kitabu hichi ningekutia mradi wa kuuendeleza hasa Uwanja wa Ndege wa Pemba lakini sikukuta. Nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri hili alizingatie.

Nikitoka hapo niende kwenye mamlaka ya usafiri wa Baharini. Hii iko ukurasa wa 44. Mhe. Spika, naomba uniruhusu kidogo ninukuu majukumu ya mamlaka hii. Uzuri wenyewe Mhe. Waziri kaeleza vizuri sana humu.

> “Majukumu hayo ni pamoja na kusimamia shughuli za ukaguzi na usajili wa meli, utoaji wa leseni na vibali kwa wafanyabiashara wa shughuli zote za bahari Zanzibar, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira ya baharini, utoaji wa hati na vitambulisho vya mabaharia.

Aidha Mamlaka hudhibiti safari za baharini, uchunguzi wa ajali baharini, usimamizi wa maslahi ya mabaharia, pamoja na utoaji wa hati za kuongeza muda leseni za mabaharia.”

Hii mamlaka ina jukumu kubwa sana.

Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa sana, nchi yetu imeshuhudia majanga mengi. Kwa mfano MV. Fatihi ilizama pale bandarini. Msiba mwengine mkubwa sana MV Spice Islander, na hata juzi ile iliyozama MV Skagit. Mimi fikra zangu tunapounda Mamlaka au Taasisi yoyote ya Serikali na tukaipa dhamana ya jambo maana yake wanaoajiriwa mle ni watu wenye taaluma ya jambo lile. Kama ni hivyo basi serikali ikishakuwaajiri wataalamu wa namna ile serikali ina tabia ya kuwaamini wale wataalamu.

Maana yake kwamba wafanye majukumu yao halafu wao watoe taarifa serikalini, serikali iziamini taarifa zile na izifanyie kazi. La kusikitisha Mhe. Spika, Mamlaka ya Usafiri wa Baharini kutakuwa na mazingira mawili, kama haina waalamu waliobobea katika fani zao au kama wapo ni wala rushwa. Lakini haiwezekani hata siku moja mameli haya mabovu yakawa yanafanya kazi.

Mhe. Spika, siku iliyozama MV. Fatihi mimi nilikwenda pale Bandarini. Aliyekuwa Mkurugenzi wa Bandari Mhe. Mustafa Aboud Jumbe wakati ile meli imejifunikiza alipanda juu ya ule mgongo wa meli akawa ana nyundo anajaribu ku-*test* lile bati lililojengewa ile meli. Kila alipokuwa anapiga nyundo kama aliyetia kwenye tope iliyo laini nyundo ilikuwa inakwenda zake ndani. Maana yake nini? Maana yake kwamba ile meli ilikuwa ni mbovu sana.

Ukiangalia historia siku zote tunapata matatizo namna hii. Kwa hivyo mameli haya ni mabovu. Sasa kama ni mabovu hii Mamlaka kazi yake nini? Mtu anakuja na meli lake bovu huko lilikotoka lishakuwa kondeni analileta Zanzibar, akifika hapa Mamlaka hii ambayo sisi tunaiamini ina wataalamu wanakwenda kuikagua wanasema inafaa kutembea na wanaiambia serikali kwamba hii meli iko salama na inafaa kutembea. Kumbe meli ukilipiga nyundo, nyundo inazama kama iliyo ndani ya tope.

Mhe. Spika, mazingira haya kwa kweli yanatupa wasi wasi sana. Mimi nadhani kuna haja ya kufanya mageuzi makubwa katika wataalamu hawa tulionao. Wataalamu hawa wanaidanganya serikali. Mazingira yanaonesha kwamba wanakula rushwa. Maana kama meli ni bovu kwa nini husemi kama meli ni bovu lisiruhusiwe kutembea. Lakini ukishakatiwa chochote unaiambia serikali meli hii inafaa, keshokutwa inakwenda kuwazamisha watu. Mhe. Spika, tutamalizika.

Hii ya mwisho tukimshuhudia Mhe. Waziri akijiuzulu hapa. Sasa kama Mamlaka hii itaachwa kama ilivyo basi na huyu aliyewekwa na yeye ajitayarishe kuna siku moja atajiuzulu naye vile vile. Kwa sababu ya wafanyakazi wasiokuwa waaminifu.

Mhe. Spika, ilipozama MV Spice Islander ile meli ilikuwa na *process* ndefu mpaka kuzama. Mawasiliano ya wale wananchi waliokuwemo mule na watu wengine yalikuwa ya muda mrefu sana. Watu walikuwa wanapiga simu kwa watu waliokuwepo juu huku na kuwambia jamani tupo huku. Vyombo vya watu wa Nungwi walitoka mpaka pale kwenye maeneo ya pale walipozama. Lakini usiku ulikuwa mkubwa hakuna kilichokuwa kikiashiria chochote cha kuonesha kama meli

ipo hapa. Mpaka meli ikamalizika kuzama ikaua watu waliokufa. Hakuna uokozi uliokuwa umefanywa isipokuwa wavuvi wa pale Nungwi walikuwa na mashua zao za kutosha za kuweza kuwaokoa wale watu.

Kwa sababu meli ilishindwa kutoa ishara yoyote kwamba tupo hapa. Meli gani hiyo ya kuiruhusu itembee katika bahari na ichukue watu. Tunaambiwa ingawa mie si mtaalamu lakini tunaambiwa kwamba meli inakuwa na vifaa ikianza kupata ajali kwanza inatoa mawasiliano kwa vyombo vyote vilivyokuwa wanavifahamu. Halafu kuna dude sijui linaitwa *parachute* wanapiga juu lile linakuwa na muangaza mkubwa. Kwa hivyo vyombo vilivyokuwepo pale karibu wanajua kwamba ile ajali ipo pale wanakimbilia.

Sasa unakwenda kusajili meli mambo hayo huyatizami inakuwaje, kama si rushwa ni kitu gani. Kama Mhe. Waziri angelinishauri ningelimwambia usijiuzulu. Kwa sababu yeye hakuwa na kosa waliokuwa na kosa ni watu wa Mamlaka hii, walisajili mameli mabovu. Nadhani Mhe. Spika, serikali itaunda Tume ya Kuchunguza labda, kama kuwa watu wa kuwajibishwa hawa ni wa kwanza, kuliko hata Waziri. Maana Waziri anapokea ripoti kutoka kwa watu hawa na wale ni wataalamu. Maana ya kugawa *section* katika wizara maana yake nini? Kwamba kila mtu unayempa seksheni yake maana yake unampa mtu ni mtaalamu akupe taarifa za ile seksheni na wewe uzifanyie kazi. Sasa kama walimpa *wrong information* kosa lake Waziri ni nini?.
Mhe. Spika, tunaomba sana haya yasitokee tena.

Mhe. Spika, naomba niende Shirika la Bandari kidogo, mwaka 2011/2012 walikisia au walikadiria kukusanya bilioni 9.3 lakini mwaka huu wamekadiria kukusanya bilioni 16.5. Sasa mimi hapa napata mashaka kidogo. Kwa sababu hili walilokadiria mwaka uliopita katika makusanyo yao halisi haikutimia ilipungua kidogo. Lakini mara hii wamekadiria jambo kubwa mara mbili ya ile kwa vigezo vipi. Naomba sana Mhe. Waziri atwambie kama mara hii wamejipanga vipi Shirika la Bandari kuweza kukushanya bilioni 16 badala ya bilioni 9 .3 walizokadiria mwaka uliopita, wakifikia mimi nitawapongeza sana.

Mwisho Shirila la Meli nalo pia walikadiria kukusanya milioni 2.5 mwaka uliopita. Kati ya hizi wakakusanya asilimia 81 tu. Yaani hawakufikia lile lengo. Lakini mara hii wamefanya *twice* ya hizo, vigezo vyao vya kuweza kufikia milioni 4.3 ni vigezo gani walivyoviona wakati hata meli hawana. Naomba sana Mhe. Waziri akija anipe ufafanuzi ili niweze kuwa na matumaini kwamba Shirika la Meli kwamba kweli linaweza kukusanya bilioni 4.3.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo na kwa sababu muda wako umekuwa mchache kidogo naomba nikubali hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Uchukuzi, lakini baada ya kupata jawabu zitakazoridhisha wananchi wa barabara ya Ole/Kengeja na wananchi wa Pemba kuhusu Uwanja wao wa Ndege, pamoja na wananchi wa jimbo la Chonga kuhusu barabara zao za ndani. Mhe. Spika, ahsante.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa ya kutoa mawazo yangu kuhusiana na bajeti hii ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehma kutufikisha siku ya leo tukiwa hai na kuweza kujadili jabeti ya Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu, huku juzi tu tukiwa tuna

msiba mkubwa mwengine. Sasa sisi tuliobaki kuwa hai hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutubakisha kuwa hai.

Aidha nadhani nitakuwa mchache wa shukurani kama sikutumia fursa hii kukushukuru wewe kutupatia nafasi pamoja na kumpongeza Mhe. Rashid Seif Suleiman kuwa Waziri mpya wa Wizara hii. Vile vile kumsifu na kumpongeza Mhe. Hamad Masoud Hamad kwa kitendo chake cha ujasiri. Nasema ni kitendo cha ujasiri kwa sababu ni historia kwa Zanzibar tangu mwaka 1964 hatujawahi kuona kama kitu alichokifanya Mhe. Hamad Masoud Hamad, laiti ningelikuwa *Vice Chancellor* wa Chuo chochote Kikuu cha nchi hii basi ningemtunuku digirii ya heshima katika mambo ya siasa *(Political Science).* Hongera sana Mhe. Hamad Masoud Hamad.

Mhe. Spika, naomba nije moja kwa moja katika ukurasa wa 44 na 46 wa hotuba ya Mhe. Waziri kuhusiana na usafiri wa Baharini. Mhe. Spika, Zanzibar ina visiwa viwili vikubwa yaani kisiwa cha Unguja na Pemba; mbapo visiwa hivi masafa yake ni karibu maili ishirini na mbili na nusu kutoka pembe moja hadi pembe ya kisiwa chengine. Huku ikiwa imezungukwa na visiwa vidogo vidogo vyengine pembeni kama vile Kojani, Fundo, Uzi, Tumbatu na kadhalika.

Mhe. Spika, kutokana na taswira ya nchi hii ya Zanzibar ni dhahiri kwamba suala la usafiri wa baharini linahitajika kwa kiasi kikubwa. Serikali iliyopo madarakani ingehitajika kuwa makini mno katika kuhakikisha kwamba usafiri wa uhakika unapatikana katika bahari. Lakini la kusikitisha hizi awamu za sasa jambo hili hawalitilii maanani.

Mhe. Spika, mimi sijapata kuona kauli ya serikali inayotia matumaini ya kupatikana meli ya serikali hapa. Nilichokiona katika ukurasa wa 43 Mheshimiwa naomba ninukuu kauli ya serikali ambayo kuwa haina matumaini. Maana tumaambiwa tusubiri hotuba ya bajeti ya Wizara ya Fedha ndio tutaona. Angalau na huku basi tungewekwa rehani kidogo roho zetu. Inasikitisha Mheshimiwa.

Mhe. Spika, kama kuna kitu ambacho hakitaki kuchezewa ni roho ya mtu. Kwa sababu baada ya utafiti wa kina na upembuzi yakinifu nimeona kwamba hawa hawa wataalamu katika nchi mbali mbali wanamudu kufanya viungo vingi bandia, ukikatika mkono utatiwa mkono wa bandia, ukikatika mguu utatiwa mguu wa bandia, lakini roho bandia sijawahi kuiona Mheshimiwa. Kwa hivyo, mtu yeyote anayecheza na roho basi mtu huyu anahitaji na yeye yake itolewe, mtu yeyote ambaye anapelekea roho yake itoke basi na yeye anahitajika yake itoke kwa sababu hakuna roho bandia. Miguu bandia iko, mikono iko lakini roho bandia haiku hili ni tatizo Mheshimiwa. Mimi nadhani serikali yetu bado inataka tuendelee kufa kwa bahari jambo ambalo ni tatizo sana.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kwamba watu kama Mzee Thabit Kombo Jecha na serikali yao ya Awamu ya Mwanzo na Mzee Abeid Amani Karume waliweza kuzi-*manage* meli zetu wakatununulia meli, akaja Mzee Jumbe Mwinu akatununulia meli, leo tulipoingia hizi awamu za huku meli tunaziuza, pesa hatuonyeshwi, hatununui nyengine sasa sisi tutamtegemea baharesa mpaka lini jamani.

Waheshimiwa mimi nadhani sasa wakati umefika, juzi nilisema laiti ingelikuwa ili upate meli unahitaji afe mwakilishi mmoja hapa basi mimi roho yangu ningekubali nipewe dakika tano nishahadie niuliwe halafu Wazanzibari wapate meli wasafirie, lakini haipatikani kwa roho

inapatikana kwa pesa. Laiti ingelikuwa meli inahitaji maneno humu sisi ni matajiri sana wa maneno kila mtu tungempa yake meli akawa anayo lakini sasa sisi ni masikini serikali imekuwa kaidi katika hili Mhe. Spika. Serikali imekuwa kaidi na waone kwamba wao ni dhamana.

Kiongozi yoyote Mhe. Spika, ni dhamana, ni mas-uul na atajibu kwa Mwenyezi Mungu amemshughulikia vipi raia wake. Mimi nadhani serikali ihakikishe kwamba usafiri wa meli unapatikana tena wa kudumu, haiwezekani hata siku moja kwamba awamu ya mwanzo wanunue mameli, awamu ya pili wanunue meli wanunue na boti faiba kutoka visiwa vidogo vidogo kusafiria watu sisi tushindwe, nyinyi wataalamu bwana.

Hata Mzee Karume skuli hakusoma masikini kamudu kutuwekea meli, Mzee Aboud Jumbe huku kuna safu nzima ma-*PhD*, Madaktari matokeo yake zile meli za Mzee Karume nyengine zinafanyiwa ma-*scraper* hapa za Afrika na Jamhuri ziko kule Wete zinafanyiwa ma-*scraper*, hii aliyotununulia Mzee Jumbe Maendeleo hatujui iwapi, ya Mapinduzi imeuzwa hizo pesa hatuzijui ziko pahali gani Yailahi Yarabi toba Mungu wangu, sasa hivi tunawania baharesa tu sisi anunue, anunue; tatizo shike shike na mwenyewe nyuma, wao wawekeze na sisi tuwe tuna yetu. Hilo moja.

Jengine Mhe. Spika, mbali na uzembe huu wa kuruhusu na kusajili mameli mabovu kama alivyozungumza mwenzangu, kuna mambo hapa yanaweza yakasababisha maisha ya binadamu kupotea hivi hivi kienyeji, wamesema hapa wanao mpango wa kukarabati minara na maboya kwa kutumia *solar*. Hivi tunavyozungumza Mhe. Spika, mnara wa Matumbilini hauwaki kabisa, kama kuna kitu muhimu katika usafiri wa mambo ya bahari basi ni minara na maboya, huu karibu mwaka wa nne mnara wa Matumbilini hauwaki na mpaka juzi *turning* boya iliyopo pale Mkoani ilikuwa haiwaki eti leo nilipozungumza na Mhe. Naibu Waziri kanambia sasa inawaka sijui vipi ndio nataka nipige simu huko nyumbani nisikilize hii *turning* boya inawaka au haiwaki.

Sasa Mhe. Spika, mambo kama haya lazima tuchukue tahadhari mapema kwamba meli iwe ni nzima lakini kama haina kitu cha kuwaelekeza wanaweza wakasababisha ajali. Juzi juzi hiyo Meli ya Maendeleo iliingia kwenye fungu kwa sababu hilo *turning* boya lilikuwa haliwaki. Kepteni akaiingiza meli huko roho mkononi watu wakawa wanataka kuruka na kutaka kupoteza maisha. Sasa katika hili mambo madogo madogo Mhe. Spika, lazima serikali iwe *serious* kuyafanyia ukarabati kabla hayajasababisha hasara kubwa, gharama ya kulitengeneza lile boya ni gharama gani ambayo hata robo ya roho ya mtu haifiki gharama yake, leo mnataka kutupotezea watu chungunzima kwa kibora kimoja tu cha pale Mkoani, tatizo. Jamani serikali kaidi sana hii.

Jengine Mhe. Spika, tuje katika suala zima la usafiri wa anga na hapa nitazungumzia kidogo katika uimarishaji wa uwanja wa ndege pale Pemba. Mhe. Spika, Pemba ni sehemu ya Zanzibar hili lazima tukubali na Wapemba ni Wazanzibari sawa sawa na Wazanzibari wowote wale. Kwa vile ile *National Cake* inatakiwa keki ya taifa ya nchi hii ya Zanzibar iwe *evenly distributed* sawa sawa igawiwe. Sasa hakuna awezae kufanya sawa mimi nakubali zaidi ya Mwenyezi Mungu lakini kuna mambo madogo madogo lazima tujitahidi kwamba tuwe tunayagagwa karibu sawia. Huu ni mwaka wa ngapi waziri anatwambia nataka kuweka taa ili ndege ziweze kutua usiku pale, mwaka zaidi ya watano nyimbo ni hiyo wakati huku kuna Uwanja wa Ndege wa *Karume International Airport* mimi naunga mkono upanuliwe si kwamba napinga, lakini sasa wakati tunapanua uwanja huku wale Wapemba nao angalau tuwatilie zile taa pale angalau wakipindwa

na mshipa usiku uweze kuita kidege kidogo kije kikuchukue kikupeleke kwenye *CT-Scan*, palke Pemba hapana *CT-Scan*, Pemba hapana *ICU*.

Sasa sisi tulikuwa tukizungumzia tu kwamba ule uwanja ni muhimu kuna uhai na umauti, kuna ugonjwa na uzima, leo wakati mnapanua uwanja wa ndege huu wa Unguja kuweka ndege za kimataifa kule kile kihelikopta hakithubutu kutua usiku, mtu kapindwa na mshipa akae mpaka asubuhi, mtu kaanguka mkarafuu hivyo hivyo na kutwa tunaanguka mikarafuu sisi huku tukiwa hatuna hata *CT-Scan,* aibu ni kuwabagua Wazanzibari.

Siku moja Mhe. Spika, kuna Mwenyekiti wa *CUF* wa Wilaya ilikuwa ni kwenye mwezi huu kama Ramadhani iliyopita tu, aligongwa na vespa ikabidi madaktari hawawezi kumtibu pale, Marehemu Moh'd Shafi Said, hawawezi kumtibu kwa sababu aliumia vibaya na ilikuwa ni wakati wa jioni sana, mimi nikampigia ndugu yangu mmoja hapa ana ndege yake ndogo uchwara ikabidi sasa tatizo atatua vipi usiku, huku na huku tukaomba kwa nguvu ikabidi akachukuliwa magharibi kwa tabu ndege kuruka haiwezi. Sasa jamani si mtaendelea kutuuwa na sisi Wapemba kwa taa tu. Kuna miradi ya trilioni huku inafanywa taa tu inatumia shilingi ngapi ile ni *biasness*, wale wanalipa kodi kama kawaida na wao. Wapemba walioko Nguuni, walioko Vitongoji, walioko Uwandani, Kiwani wanalipa sawa sawa na jamaa wa Rahaleo hapo tusiwabague lazima Serikali ya Umoja wa Kitaifa mlete *National Unity* msiwe *biase*.

Mhe. Spika, ikiwa sikuambiwa kwamba taa zitatiwa lini hapa basi nitaweka mguu kwenye kifungu hiki, niambiwe tarehe fulani tutafunga taa sisi pale, kinyume na hivyo basi mimi nazuia kifungu.

Mhe. Spika, sasa niende katika usafiri wa nchi kavu. Mhe. Spika, katika mpango huu wa serikali yetu nzuri ya Umoja wa Kitaifa ya Kupunguza Umasikini nakuongeza Kipato basi kumewaagiza wananchi wetu wawekeze maisha yao katika sekta mbali mbali zikiwemo za kilimo. Kama kuna wakulima wazuri, kama kuna wakulima ambao wanakijua kilimo basi ni wananchi wa Jimbo la Wawi. Na kwa kweli Mhe. Spika, wananchi wa Jimbo la Wawi katika Kijiji cha Vikunguni, kijiji cha Ng'ambwa, Kibokoni, Uwandani hawa wanatoa mazao kama ndizi, embe, tungule kwa wingi mno.

Lakini jambo la kusikitisha Mhe. Spika, barabara hawana hawa *feeder road,* jambo la kusikitisha Mhe. Spika, barabara ya kutoka Mkaani-Uwangani kule ambako kunazalishwa tungule kwa wingi mno hadi kupitia Vikunguni mpaka Mjengo wa Banda mpaka *Starling Mace* ya jeshi pale haipitiki, tungule zetu hulazimika kuanguka humo majiani huku zikitumbuka hata kama una debe mbili basi hata ukifika una nusu debe. Haya uondoaji wa umasikini utatokea hapo, wakati wewe kile unachotaka kukipeleka katika Soko la Chake Chake hakifiki kwa sababu ya kutokuwa na barabara.

Mhe. Spika, watu wa Vikunguni na Ng'ambwa wanazalisha ndizi mno na hili soko la Unguja Mjini linachangiwa karibu asilimia 20 na ndizi kutoka katika Jimbo la Wawi tena katika kijiji cha Vikunguni na Ng'ambwa, lakini masikini nyingi hatuna pa kuzipitishia. Kutoka Vikunguni barabara kuja Skuli ya Ng'ambwa mpaka Gombani haipitiki ndizi zinaiva njiani huku yakioza tu wakati walaji hapa wapo, wakati walaji Chake Chake wapo. Sasa umasikini huu mpaka lini.

Mimi nadhani Mhe. Spika, Waziri mpya wa Miundombinu aiangalie barabara ya kutoka kwenye Kware Uwandani kupitia Vikunguni pale na kuja zake Skuli ya Ng'ambwa mpaka Gombani uwanja wa mpira mpya pale ahakikishe anaifanyia ukarabati kusudi tuweze kupunguza umasikini na kujiongezea kipato Yailahi Yarabi toba Mungu wangu tusaidie. Hilojengine.

Mhe. Spika, nikija hapa hapa kwenye *UUB* hawa wajenzi wa barabara. Mhe. Spika, mimi nadhani wizara baada ya kwishajenga barabara baada ya Wizara hii ya Miundombinu kwishajenga barabara kadhaa wa kadhaa katika visiwa vyetu hasa pale Pemba fusi sana wanachukua kule kwetu Vitongoji. Mhe. Spika, kama utakwenda Vitongoji hivi sasa Makaani Allahu Akbar, mazingira yalivyoharibiwa na *UUB* ni hatari. Kuna mashimo basi kuipitisha hiyo Kalama nayo itazama tena mle, mana wamechimba mpaka yameingia maji chumvi. Juzi hapa nikamtaka waziri twende na nimeshamkatia tiketi ya ndege naibu waziri akakataa akaone mwenyewe.

Sasa Mhe. Spika, katika hili mimi nadhani Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ina jukumu kubwa mno la kurudisha mazingira pale ambapo wanayachafua baada ya kuchimba kifusi. Kwa mfano, sisi watu wa Vitongoji sasa hivi kule hatupati kulima maweni kwa sababu wamekokoa, wamechimbua vifusi mashimo wameacha vile vile, mimi nadhani wangeshirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake kusudi wakaweza kurudisha yale mazingira waliyoyaharibu.

Mhe. Spika, nadhani nimalizie hapa haka kwamba nashukuru kuwa kuna taasisi binafsi katika mamlaka ya usafiri wa anga hizi zinatusaidia sana, zinasaidia na zinatoa ajira kwa wananchi wetu. Juzi hapa mimi nilijenga hoja kwamba hapa katika uwanja wa kimataifa wa Karume kuna mchezo ambao tunauhisi unaweza ukatuathiri. Juzi nilikuwa nazungumza na kijana mmoja akanambia *ZAT* pale wameajiri zaidi ya vijana 200 *airport*, nilipojaribu kusema siku hiyo nikaambiwa kwa sababu ile wewe ni ya jamaa yenu Raza sijui vipi, mimi sisemi hivyo, mimi ninachojali ni wazalendo, wawekezaji wazalendo. Sasa Mhe. Spika, hapa wanakuja watu wa serikali kutubabaishia maneno sijui *ZAT* hawana hivi, hawana hivi, hawajatimiza masharti, sisi tunaridhika na *ZAT* kwa sababu wameajiri vijana wetu, sasa kama mtawaleta *port* pale sidhani kama wanaweza wakatuchukulia.

Mhe. Spika, wale Wataliana pale wamechukua watu kutoka Kenya, pia wanachukua watu kutoka Arusha kwenye sekta za utalii leo hawa jamaa wa *ZAT* hapa *Airport* wanajali ndugu zetu wa damu watoto wetu hawana ajira wavute unga jamani. Mimi nadhani waziri na wewe liangalie hilo na baadae uone kwamba *ZAT* wana nia na wananchi wao na wala hatusema hivi kwa sababu kuna Raza pale, tuliisema hii kabla Raza hajaingia humu ndani, wala mimi sina habari hasa kama Raza ana-*share* kwenye *ZAT*, sina nimesikia humu humu ndani. Lakini ninachojua ni kwamba *ZAT* wana vijana wetu pale wamewaajiri zaidi ya 200 kwa hivyo, hatuwezi sisi kuachia ajira 200 zikaenda hivi hivi tu.

Ahsante Mhe., Spika, naunga mkono hoja pale nitakapopata maelezo kwamba taa zitawekwa lini *airport* pale Pemba na ule mnara wa Matumbilini utawaka lini. Nitaunga mkono baada ya kupata maelezo hayo ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Tunawashukuru Waheshimiwa Wajumbe, sasa tuahirishe shughuli zetu hadi kesho tarehe 02/08/2012 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 9:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 02/08/2012 saa 3:00 asubuhi)